

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 11 Mei, 2017

(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, Kiongozi wa Upinzani Bungeni.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kumuuliza Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Bunge kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 63(2), ndicho chombo kikuu chenye mamlaka na wajibu wa kuisimamia na kuishauri Serikali. Katika Bunge hili, Bunge la Kumi na Mabunge mengine kadhaa, Bunge limekuwa linatoa Maazimio kadhaa kuitaka Serikali itoe taarifa na Serikali imekuwa inaahidi kutoa taarifa, lakini taarifa nyingi ambazo ni Maazimio ya Bunge yamekuwa hayatekelezwi na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna Maazimio ya Bunge kuhusiana na Tokomeza mpaka leo Serikali haijaleta majibu. Kuna Maazimio ya Bunge kuhusiana na *ESCROW* na *IPTL*, Serikali mpaka leo haijatoa majibu. Kuna Maazimio ya Bunge kuhusu mabilioni ya Uswis, Serikali mpaka leo haijatoa majibu na Maazimio mengine mengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu unaliambia nini Bunge na unaliambia nini Taifa. Wewe kama Kiongozi wa Serikali Bungeni, utapenda kusema kwamba Serikali inalidharau Bunge ama Serikali haina majibu ya kutoa? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, Mbunge wa Hai na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nikuhakikishie kwamba Serikali inaheshimu sana Mhimili wa Bunge na inathamini sana maamuzi ya Mhimili huu wa Bunge na tutaendelea kushirikiana na Mhimili wa Bunge katika kupata ushauri na namna nzuri ya kuendesha Serikali kwa mapendekezo ambayo yanatolewa na Waheshimiwa Wabunge kupitia chombo cha Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua vikao kadhaa huko awali kumekuwa na Maazimio yanayoitaka Serikali ilete maelezo, lakini baadhi ya maeneo ambayo yanatakiwa kuletwa hapa ni yale ambayo yanahitaji uchunguzi wa kina na uchunguzi huu unapokamilika ndipo unapoweza kuletwa Bungeni.

Sasa yapo ambayo tunaona upo umuhimu wa kuyaleta ni pamoja na hayo uliyoyasema, nataka nikuahidi kwamba haya ambayo umeyatamka kwenye maeneo yanayogusa Wizara kadhaa ambazo zinatakiwa kuleta taarifa nitafanya ufuatiliaji, pale ambapo tutakuwa

tumekamilisha uchunguzi wetu, nitayaleta kwa utaratibu ambao Bunge utakuwa umetoa maelekezo yake. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, swali la nyongeza.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu yake, ni ukweli usiopingika kwamba pale muda unapotumika au unapopita sana bila majibu hata *status* kutolewa katika Bunge, hoja hiyo huonekana kwamba imeffia umuhimu na ulazima wake.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na kwamba umetoa ahadi ya kwamba Wizara zitashughulikia, unaweza ukatoa *a firm commitment* kwamba katika Bunge hili, kabla Bunge hili la Bajeti halijaisha, Serikali itapitia *Hansard* na kumbukumbu zote zinazohusiana na Maazimio yaliyopita ya Bunge halafu Serikali itoe *status report* na naomba itambulike hapa kwamba *status report* siyo lazima ndiyo iwe ripoti ya uchunguzi ya mwisho, angalau ituambie jambo hili limefikia hapa, limefanyiwa kazi moja, mbili, tatu, bado tutaletewa katika hatua ya baadae.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalau Bunge lipewe *status* ya Maazimio kadhaa ambayo ni mengi kwa kweli, ambayo yameshaazimiwa na Bunge hili, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu ya hiyo nia njema ya Serikali, unaweza ukatoa *commitment* hiyo? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimeeleza awali kwamba masuala yote haya yanagusa maeneo mengi sana ambayo yanatakiwa ufuatiliaji wa kina na baadae

nileeza kwamba kila tukio linagusa Wizara kadhaa, kwa hiyo siwezi kusema kwamba katika Bunge hili nitakuja kuleta taarifa hiyo mpaka pale ambako nitakutana na Wizara, nijue wamefikia hatua gani, pia tutakutana na Mheshimiwa Spika ili tujue utaratibu mzima wa namna ya kupata hizo *Hansard* na kufanya mapitio. Tukijiridhisha na tukiona kwamba jambo hilo sasa linafaa kuletwa Bungeni na kwa kuwa liliazimiwa na Bunge, basi tutafanya maamuzi ya pamoja ya kuleta Taarifa hiyo Bungeni. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea sasa na orodha. Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, swali kwa Waziri Mkuu.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa umakini na utendaji wake na kilichonivutia zaidi anapotoka hapa akienda ofisini kwake haifiki hata dakika, watu anaokutana nao njiani anasalimiana nao ni jambo la kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri bila kujali itikadi ya chama. Ninakupongeza sana, mara nyingi huwa nikikaa nje pale na nikienda kunywa chai ninakuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakaribiwa na Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kama wiki mbili tu panapo majaaliwa tukifika, hali ya kusikitisha ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, sukari inahitajika kwa wingi matumizi yake. Hata wananchi wa Ruangwa na Peramiho wanahitaji sukari. Mwenyezi Mungu alitupa mtihani wa mvua, viwanda vyetu vya ndani havikuweza kuzalisha sukari ya kutosha na uchunguzi au harufu niliyoipata tunahitaji kama tani laki moja na ushee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kusikitisha kwa taarifa niliyo nayo ni kuwa mmetoa vibali vya tani 30,000 na baya zaidi kuna msemo Waislamu husema nguo ya Ijumaa hufuliwa Alhamisi na mvua hii pengine isikauke. Sasa hawa mliowapa vibali, sukari yao navyotegemea hata ikifika

Ramadhani itakwisha, itawasaidia nini wananchi? Mnatumia utaratibu gani kuwapa vibali hawa watu, wanarudia ndiyo wale wale au na wengine? Kuna *formula* gani ili kuokoa hatua hii.

Mheshimiwa Waziri Mkuu uko tayari kuleta watu angalau mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani wakaingiza sukari kwa kipindi hiki ili kuokoa hii hali na janga hili lilivyo? Hii sukari mliyowapa vibali hata ikifika Ramadhani itakwisha, itasaidia nini kwa wananchi? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jaku, umeshauliza maswali manne tayari hapo uliposimama. Kwa hiyo, naomba umpe nafasi Mheshimiwa Waziri Mkuu aanze kujibu moja baada ya lingine.

Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jaku, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, najua amezungumza mengi na yaliyotengeneza maswali mengi sana. jambo la msingi alilotaka kuzungumza hapa ni kupungua kwa sukari na mahitaji ya sukari nchini kwa sasa. Napenda niwathibitishie Watanzania kwamba Serikali iko macho na inajua maeneo gani yanahitaji kuboreshwa kulingana na mahitaji ambayo yanahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala la sukari ni kweli nchi yetu hatuna uzalishaji wa kutosha wa sukari kutosheleza mahitaji ya Watanzania. Katika mwaka wa kilimo, mahitaji ya sukari nchini ni zaidi ya tani 420,000, lakini uzalishaji tulionao hapa nchini ni tani 320,000; kwa hiyo tunakuwa na mapungufu ya sukari inayohitajika ya tani laki moja na ikiwezekana zaidi kwa sababu ya ongezeko la watumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka tunao utaratibu wa kuagiza sukari na mwaka huu pia tumesahafanya hilo, tumeshaagiza sukari na mwaka huu tumeagiza sukari

tunataka tuagize sukari ya tani 131,000 kwa mujibu wa takwimu zilizofanyiwa utafiti na Bodi ya Sukari, kati ya hizo tayari tumeshaagiza tani 80, kati ya tani 80 tayari zimeshaingia tani 35 na nyingine ziko bandarini. Hizi tani 35 tumeshaanza kuzigawa kwenye maeneo yote ya nchi ili ziweze kufika kwa wananchi ziweze kusaidia kupunguza gharama na bei.

Mheshimwa Naibu Spika, pia kwa kuwa, tunakabiliwa na Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambapo watumiaji ni wengi, utaratibu wa kuagiza sukari zaidi kufikia malengo umeshaandaliwa. Watanzania tushirikiane kuwasih wafanyabiashara ambao sasa hivi wamepandisha bei bila sababu na hii inaumiza sana Watanzania kwa sababu bei zilizopandishwa hazina umuhimu wowote kwa sababu uzalishaji tulionao na hii sukari pengo tunavyoleta nchini inataka tu bei zile ziendelee kuwa ambazo zinaweza kuhimilika na Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko mikakati ya kuongeza uzalishaji kufikia malengo. Natambua tuna viwanda vinne, *Kagera Sugar*, *Kilombero*, *TPC* na *Mtibwa*, tuna kiwanda cha tano kilichoko Tanzania Visiwani, Mahonda navyo pia vinasaidia uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa tatizo la kuagiza sukari nje ya nchi, tumejiwekea utaratibu wa kukutana na wafanyabiashara wenye viwanda na kuwasih kuongeza uzalishaji na tumeona jitihada kadhaa ambazo zinafanywa na wazalishaji. Bahati nzuri sana wiki moja iliyopita nilikuwa Mkoani Kilimanjaro, nimepata nafasi ya kutembelea kiwanda cha *TPC* ambacho kimeonesha mafanikio makubwa ya uzalishaji zaidi. Mwaka jana walizalisha tani 100,000 na sasa wameongeza tani 20,000, kwa hiyo, sasa hivi wamefikia uwezo wa kuzalisha tani 120,000 na msimu huu wa kilimo wataongeza tani nyingi zaidi, hivyo hivyo na viwanda vingine kama *Kilombero* na *Mtibwa Sugar*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilipofanya ziara Mkoani Manyara, nilitembelea *Manyara Sugar*, kwa hiyo viwanda vingi vinaendelea kujengwa na sasa tunakamilisha taratibu

za kuanza ujenzi wa kiwanda cha sukari Mkoani Morogoro kuna eneo la Mbigiri kwa ushirikiano na Magereza pia na eneo la Mkulazi ambalo linaandaliwa na Taasisi ya *NSSF* na *PPF* kwa pamoja na wawekezaji ambao pia wako tayari kutuunga mkono katika uzalishaji wa sukari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaondoe mashaka Watanzania kwamba sukari ipo na wakati wa Ramadhani sukari ya kutosha itakuwepo wala hakuna sababu ya kuongeza bei, tutafanya hivyo na pia ufuatiliaji kuona bei haziongezeki ili kuwakera Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jaku naona umesimama, ulishauliza maswali manne tayari na yote Mheshimiwa Waziri Mkuu ameyajibu, sasa inabidi watu wengine pia wapewe nafasi. Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Naibu Spika, utakuwa haujanitendea haki.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kumuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nchi yetu imekuwa na sera nyingi sana, sera ambazo mara nyingi utekelezaji wake ama ni pungufu au hazitekelezwi kabisa. Sera hizi mara zote kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi zimekuwa zikirudiwa rudiwa mara nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo swali langu litaenda kwenye Sera ya Maji ya mwaka 1991 ambayo lengo kubwa ilikuwa wananchi wetu waweze kupata maji kwa umbali wa mita 400, utekelezaji wa sera hii mpaka ifikapo mwaka 2002, siyo hivyo tu, Julai 2002 hiyo baada ya ile sera kuwa hajafikiwa, ikafanyiwa mapitio tena, ikatambua kwamba maji ni uhai, maji ni siasa, maji ni uchumi, vilevile ikaingizwa rasimu ya kwamba maji na mazingira.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mpaka leo hii wananchi wetu wamekuwa na janga kubwa la maji. Ni nini kauli ya Serikali juu ya utekelezaji wa sera hii? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri kwamba sera hiyo tunayo na huo ndiyo msisitizo wetu na hata bajeti ambazo Waheshimiwa Wabunge huwa mnazipitia kila mwaka zinalenga kufikia hatua hiyo. Nataka niwahakikishie kwamba pamoja na mipango ya Serikali ya usambazaji wa maji, pamoja na kutenga bajeti ambazo tunazo huku ndani, bado tunapata tatizo kubwa nchini la kupatikana kwa vyanzo vya kutosha vya maji vinavyoweza kutosheleza kusambaza maji kwa kiwango ambacho tumejiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ni malengo na malengo yetu tunataka tuyafikie, tunapata changamoto kwenye utekelezaji kama ambavyo nimeeleza. Sasa hivi nchi imekumbwa na uharibifu mkubwa sana wa mazingira na nimelieleza mara kadhaa. Maeneo haya yamesababisha kukosekana upatikanaji wa maji na miradi mingi ambayo inatakiwa itekelezwe ni ya gharama kubwa kwa sababu inatakiwa tufuate maji kwenye umbali mkubwa ambapo gharama zake ni kubwa, hiyo sasa inakuja kugongana na mahitaji pia ya bajeti. Waheshimiwa Wabunge sasa hivi tuko kwenye Bajeti ya Maji ambayo mnaendelea kujadili na kushauri Serikali na Serikali kwa usikivu tulionao tutaendelea kuwasikiliza na kuyachukua yale yote muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutumia nafasi hii kuwasihia Waheshimiwa Wabunge tushirikiane sana katika kuhakikisha mazingira yetu nchini yanalindwa ili tuwe na vyanzo vya kutosha, Serikali imudu kuchimba visima hata vya urefu wa kati au urefu mfupi ili kuweza kumudu kusambaza maji kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa ambalo tunalipata sasa ni hilo la kukosekana kwa vyanzo sahihi vya maji. Lakini pia nitumie nafasi hii kuwasihi Watanzania, tuendeele kuvitunza vyanzo vyetu vya maji ili Serikali isitumie gharama kubwa kutafuta mradi ambao maji yake hayatoshi na kama unayapata ni ya muda mfupi kwa sababu huku juu kote kuko kweupe na jua linavyopiga maji yote hukauka.

Kwa hiyo, nataka nikuhakikishie kwamba Ilani yetu inayosema katika kipindi cha miaka mitano tunataka tufikie hatua fulani, tutaitekeleza. Serikali ya Awamu ya Tano sasa tuna mwaka mmoja na tunaomba ridhaa yenu mwaka wa pili wa utekelezaji, mpaka kufikia mwaka 2020 kama miaka mitano ya ahadi zetu, tunatarajia sehemu kubwa ya nchi kwenye vijiji, kata na miji mikubwa tuwe tunapata maji kwa kiwango ambacho tumejiwekea *commitment* kwenye sera ya kufikia mita 400 kila mmoja aweze kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumemuona Makamu wetu wa Rais, Mama Samia Suluhu akipita kuzindua miradi mingi sana, naomba sasa mtupitishie bajeti yetu ambayo tunajidili hapa ili tuendeele kutoa huduma za maji. Tunajua tuna changamoto, inaweza kuwa fedha kidogo lakini tutaendelea kuwa na miradi mingi sana ambayo tutaifungua. Juzi tumefungua mradi mkubwa sana Tabora, unaotoa maji Shinyanga, Ziwa Victoria, tunasambaza Tabora na Wilaya zake zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea na miradi mikubwa kama hiyo, tutaendelea kuzungumza na marafiki zetu ambao pia tunapata miradi ili tuweze kusambaza miradi hii kwenye vijiji na kwenye umbali ambao tumeuweka kwenye sera yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kuchauka swali fupi la nyongeza tafadhali.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante kwa majibu yanayotia matumaini, lakini umeainisha kwamba tatizo kubwa tulilionalo ni tatizo la vyanzo vya maji. Je, Serikali haioni sasa imefikia wakati wa kuvuna maji ambayo maji mengi kwa mfano, wakati wa masika kama sasa hivi, maji mengi yanapotea hakuna namna yoyote ya kuvuna hayo maji ili iwe ni chanzo mbadala cha maji? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya mipango ambayo tunayo ni ya uchimbaji wa mabwawa kwenye maeneo ambayo tunadhani tunaona kwamba kuna utirishaji wa maji hasa msimu wa mvua.

Pili, tumeendelea kutoa elimu kwa Watanzania kuzitumia mvua na maji ambayo yanatiririka, kuweza kuyaweka pamoja ili yawe akiba yetu ya kuweza kupata maji na kusambaza kwenye vijiji. Mpango huo upo pia hata kwenye bajeti umeona mipango wa uchimbaji mabwawa maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Kuchauka, wewe unatoka Liwale ni jirani yangu na ninapafahamu Liwale, iko miradi mingi sana tu ya kuchimba mabwawa, lakini jambo la kusikitisha ni kwamba juzi nilikuwa nazungumza na Mkurugenzi wako akiripoti kwamba kuna mvua nyingi, mabwawa mengi yameharibiwa, kwa hiyo tuahitaji tena kutenga fedha za kutengeneza mabwawa yako pale, jambo hili nalo tunalifanya karibu maeneo yote ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika nasihi na ninatoa wito kwa Halmashauri zote za Wilaya nchini kuhakikisha kuwa tunatumia vizuri mifereji iliyopo na mvua ambazo sasa zinaisha mwishoni, pia hata msimu ujao wa mvua kuweza kujenga mazingira ya kukusanya maji yanayotiririka, wenye nyumba za bati na nyumba zote watumie mvua hizi kupata maji na kuyaweka mahali ili tuweze kuyatumia kipindi cha ukame, kwa kufanya hilo tutakuwa tumepunguza ugumu wa upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaahidi Waheshimiwa Wabunge na Watanzia wote Serikali itaendelea na mipango yake ya kuhakikisha kwamba tunamtua ndoo Mama ili aweze kufuata maji kwa umbali mfupi na hasa ule umbali ambao tumejiwekea kwenye sera wa usiozidi mita 400. Ahsante (*Makofi*).

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kunti Majala swali kwa Waziri Mkuu kwa kifupi tafadhali.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunapoingia kwenye chaguzi vyama pamoja na wagombea huwa wanawaahidi wananchi ili waweze kuwaamini na kuweza kuwapa nafasi katika nafasi mbalimbali wanazogombea. Mnamo tarehe 5 Oktoba, 2015 mgombea Urais kupitia Chama cha Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli akihutubia katika uwanja wa Barafu Manispaa ya Dodoma alikutana na mabango mbalimbali ya wananchi wa Manispaa ya Dodoma wakilalamikia suala la *CDA* na mgombea Urais Mheshimiwa John Pombe Magufuli aliwaahidi wakazi wa Manispaa ya Dodoma endapo watampatia kura za kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jukumu lake la kwanza ni kuifuta *CDA*.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakazi wa Manispaa ya Dodoma wanapenda kujua ni lini ahadi hii ya Mheshimiwa Rais itakwenda kutekelezwa? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kunti, Mbunge wa Dodoma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli alipokuwa anafanya ziara

maeneo mbalimbali amekuwa akitoa ahadi kadhaa. Nataka nirudie kusema tena kwa Watanzania kwamba ahadi ambazo Mheshimiwa Rais ameziahidi tutajitahidi kuzitekeleza kwa kiasi kikubwa ikiwemo na uboreshaji wa Mji wa Dodoma, pia moja ya ahadi yake ilikuwa ni kwamba katika awamu yake hii kufikia mwaka 2020 atahakikisha Serikali inahamishia Makao yake Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ikiwa ni moja kati ya mambo ambayo aliyaaahidi na tumeyatekeleza, mbili kwa kuwa tayari Serikali imehamia Dodoma lazima sasa tuandae utaratibu wa uboreshaji wa mazingira ya Mji wa Dodoma ili utawala wake, uendeshaji uweze kuwa rahisi ikiwemo na kupitia sheria mbalimbali zilizoionda *CDA*, kuzifanyia mapitio na kuziboresha ili tuweze kuachana na *CDA* tuwe na mfumo ambao utatoa nafasi kubwa ya kukaribisha watu wa kawaida, wawekezaji na kuitumia ardhi iliyopo kwenye Manispaa katika kuwekeza au vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa nikiri kwamba kwa Sheria ya *CDA* huwezi kuleta mwekezaji hapa kwa sababu ni *CDA* pekee ndiyo imepewa ardhi hii na wao ndiyo waliopewa hati na ardhi Makao Makuu. Kwa hiyo wao wasingeweza kutoa hati kwa wananchi wanaojenga au wanaowekeza hapa, ili kuwapa nafasi wananchi kuwa na hati ya umiliki wa ardhi lazima tufute Mamlaka ya *CDA* ili tuweze kutumia Sheria ya Ardhi katika kutoa ardhi iliyopo hapa ili tuweze kukaribisha wawekezaji na uboreshaji wa mpango ambao sasa tumeukamilisha kuhamia Makao Makuu Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nikutoe wasiwasi kwamba sasa tunafanya mapitio na Mheshimiwa Rais ameshatoa maagizo Tume imeshaundwa inafanya mapitio ya namna bora ya kuifuta *CDA* lakini kupitia sheria zilizoiondwa *CDA*, hiyo ndiyo hatua ambayo tumeifikia na katika kipindi kifupi tutakuwa tumeshatoa taarifa. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kunti Majala swali la nyongeza.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: heshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mkiwa bado kwenye huo mchakato wa kwenda kupitia sheria na mambo kadha wa kadha, hata wewe pia unafahamu kuwa changamoto kubwa iliyopo baina ya wakazi wa Manispaa ya Dodoma na CDA, nini tamko lako kwa CDA kuhusiana na bomoabomoa zinazoendelea bila wananchi hao kulipwa stahiki zao?

Jambo la pili, endapo hamtakamilisha huo mchakato, mnawaambia nini Watanzania wa Manispaa ya Dodoma kwamba ahadi iliyotolewa ilikuwa ya uongo na kuwarubuni Watanzania ili mpate kura *then* muwapotezee? Kama msipofanya hivyo mnawaambia Watanzania wasiwachague tena kwa sababu mmekuwa na ahadi za uongo zisizotekelezeka? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimwambie usiwe na mashaka ya utekelezaji wa Ilani zetu na kwamba umeanza kutanguliza majibu ya wananchi msiwachague tena hilo siyo lako, wewe subiri tutekeleze ahadi zetu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote wa Mkoa wa Dodoma wakiwemo na wananchi wa Manispaa, jambo muhimu hapa ni kufanya maboresho ya Mji wa Dodoma ambako ni Makao Makuu ya Serikali. Kama ambavyo nimeeleza kwenye maelezo yangu ya msingi kwamba tayari Tume imeshaundwa wanaendelea kuharakisha zoezi hilo la kuhakikisha kwamba tunaondoka kwenye sheria iliyounda CDA ili kurudi kwenye sheria tuweze kuifanya CDA iweze kufanya kazi zile ambazo zitampa mwananchi haki ya kuweza kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo swali ambalo limesema

wale ambao wanabomolewa na CDA, sasa hili ni lazima tufanye mapitio CDA utaratibu wanaoutumia, wanabomoa kwa ajili ya nini na je, maeneo hayo na wale wanaobomolewa wanatakiwa kupata stahili ya namna gani. Kwa sababu sheria tuliyonayo inamtaka popote ambako unataka kupatumia kwa kuondoa mali ambayo mwananchi amewekeza lazima uilipie fidia.

Kwa hiyo sheria ipo, lazima tuone tufanye mapitio tuone CDA sasa wanaendesha *operation* wapi na wanalipa au hawalipi ili tuweze kujua kama hawalipi kuna sababu gani za msingi za kutolipa, lakini haki ya kulipwa ipo pale na ninaamini CDA ipo ofisini kwangu, kwa hiyo nitafanyia mapitio halafu nitakupa taarifa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Ulega swali la fupi.

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kupata fursa hii ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hapo nyuma kidogo Serikali ilitoa agizo kwa nia njema kabisa ya kutaka kutunza na kuboresha mazingira yetu, agizo lenyewe lilitutaka wananchi maeneo mbalimbali katika nchi kuhakikisha kwamba mwishoni mwa wiki tunafanya usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, jambo hili ni jema sana na sisi wananchi tulilipokea vizuri sana katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Jambo hili limesababisha kero na usumbufu mkubwa kwa wananchi, hasa kwa kufungwa huduma muhimu wakati wanapokuwa wanazihitaji, huduma kama vile vituo vya afya, zahanati hata mahospitalini asubuhi ya siku ya Jumamosi wananchi wamekuwa hawapati huduma ipasavyo, migahawa pia katika maeneo ya miji imekuwa ikifungwa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, je, Serikali ipo tayari sasa kutoa ama kuboresha agizo hili ili wananchi wale waendele

kupata huduma ipasavyo wakati huu wa asubuhi wa mwisho wa wiki?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka msisitizo wa nchi yetu kuwa safi kwenye maeneo tulimo, kwenye makazi, maeneo ya jumuiya, maeneo ya utoaji huduma ili kuifanya nchi kuwa safi kama ambavyo sasa tunaona maeneo kadhaa yana usafi unaoridhisha lakini bado tunatakiwa tuongeze nguvu. Utaratibu ambao tumeutoa ni kwamba tumekubaliana nchi nzima kila Jumamosi moja ndani ya mwezi mmoja kadri Mikoa ilivyojipangia au Wilaya ilivyojipangia ni kwamba Watanzania wote lazima tujihishe kwenye usafi wa maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika makazi yetu lakini na maeneo ya jumuiya kama vile vituo vya mabasi, hospitali na maeneo mengine. Utaratibu unaendelea, Mheshimiwa Mbunge ameomba kujua utaratibu unaotumika na baadhi ya maeneo wa kufunga maeneo muhimu, nasi tumesisitiza kwamba viongozi wa maeneo hayo ambao wanatambua kwamba eneo hili ni la utoaji huduma za jamii ambao ni muhimu, waweke utaratibu mzuri wa namna ya utoaji huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu suala la usafi ni kuanzia saa 12.00 na tumesema angalau mpaka saa 4.00 asubuhi, kwa hiyo ni kwa saa manne tu. Kama eneo hilo linaweza kuvumilika kusitisha kwa muda fulani ili kuruhusu kufanya usafi ni vizuri, lakini kama eneo hilo lina mahitaji makubwa ya utoaji wa huduma basi Mkuu wa Wilaya, Mwenyekiti wa Kijiji na viongozi wa maeneo hayo waweke utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi wanaosimamia zoezi hili waangalie umuhimu wa utoaji huduma wa maeneo ya jumuiya kama ni lazima yafungwe kwa saa manne hayo au vinginevyo ili kuruhusu kufanya usafi. Kwa mfano maeneo

ya hospitali hatuwezi kuyafunga hili eneo lazima liwe wazi wakati wote kwa sababu tunazo dharura zinaweza kutokea wakati wowote. Hivyo muhimu zaidi ni kuweka utaratibu wa usafi wake kwanza kabla ya siku ya Jumamosi ili Jumamosi huduma ziweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya migahawa yenyewe wakati wote yanatakiwa yawe safi hata bila kuwa na Jumamosi, ni muhimu zaidi wale waendesha migahawa wahakikishe maeneo hayo yanafanyiwa usafi vizuri na siku ile ya Jumamosi kama kiongozi wa eneo hilo anaona kuna umuhimu wa eneo hilo kutofunga ili shughuli ziendelee basi tujiridhishe kwamba eneo hilo liko safi, kwa vile usafi ule unajumuisha wananchi wote kwa pamoja kutoka kwenye eneo hilo, watumishi wa eneo hilo waingie kwenye usafi kwa pamoja ili waweze kushiriki kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu zaidi ni kiongozi wa eneo hilo kuona umuhimu wa eneo hilo na mahitaji yake, aweke utaratibu mzuri kwa ajili ya kufanya kazi bila kuzuia huduma nyingine kuendelea. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ulega muda wetu wa maswali kwa Waziri Mkuu umekwisha, kwa hiyo utatuwia radhi kwa swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana. *(Makofi)*

Katibu.

NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na maswali ya kawaida na tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na.185

**Matatizo yanayowakabili watu
wenye Ulemavu Vijijini**

MHE. AMINA S. MOLLEL aliuliza:-

Masuala ya watu wenye ulemavu kwa kiasi kikubwa yanazungumzwa na kushughulikiwa katika maeneo ya mijini na kusahau maeneo ya pembezoni ambapo kuna watu wa jamii hiyo.

Je, Serikali ina mpango gani kuhusu watu wenye ulemavu waishio vijijini ambapo matatizo yao ni mengi na makubwa kulingana na jamii inayowazunguka?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto zinazowakabili watu wenye ulemavu waishio vijijini, kwa kutambua hilo Serikali imefanya ugatuaji wa shughuli zinazohusu watu wenye ulemavu kwenda katika Serikali za Mitaa. Serikali inaendelea kuzijengea uwezo Halmashauri na watoa huduma wengine ili kutatua kero zinazowakabili watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kulingana na Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Namba 9 ya mwaka 2010, imeelekeza kuanzisha Kamati za Baraza la Huduma na Ushauri kwa Watu Wenye Ulemavu kuanzia ngazi ya kijiji/ mtaa hadi ngazi ya taifa, ambazo zitasaidia utoaji huduma kwa watu wenye ulemavu. Katika kusimamia utekelezaji wa

matakwa ya sheria hii, Serikali imewaagiza Makatibu Tawala wote wa Mikoa kusimamia uanzishwaji wa Kamati za Mikoa, Halmashauri, Kata na Vijiji kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu maana ndiko walipo watu wengi wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe rai kwa jamii kuanzisha vyama vya kiraia vikiwemo Vyama vya Watu wenye Ulemavu ambavyo vimekuwa vikifanya kazi kwa ukaribu na wenye ulemavu hadi vijijini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amina Mollel swali la nyongeza.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa matatizo makubwa yanayowakabili watu wenye ulemavu hasa waishio vijijini ni umaskini uliokithiri kwa jamii hii. Mbali ya Serikali kutoa maagizo kwa Halmashauri kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri.

Je, Serikali sasa ina mkakati gani kuhakikisha kwamba inapunguza umaskini kwa kundi hili la watu wenye ulemavu ambalo liko nyuma?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, sababu kubwa kama nilivyoeleza inayopelekea watu wenye ulemavu kuwa na maisha duni ni pamoja na kutozingatiwa kwa mahitaji yao wanayoyapendekeza katika ngazi mbalimbali wakati wa bajeti.

Pamoja na hizo sababu mambo hayo yanapuuzwa, kwa kuwa bajeti ya Serikali bado kusomwa; je, Serikali haioni muhimu sasa wa kuangalia uwezekano wa kutenga fedha kwa Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu ambao katika bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu haukutengewa hata shilingi, sasa tuangalie ni kwa jinsi gani basi tutatenga fedha ili tuweze kusaidia kundi hili? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Sheria Namba 9 ya mwaka 2010 inazitaka Mamlaka za Mikoa kusimamia uanzishaji wa Kamati za Walemavu kwenye Mikoa, Halmashauri, Kata na Vijiji na tulishaagiza kama alivyosema kwenye jibu la msingi Naibu Waziri Mheshimiwa Mavunde, lakini nichukue nafasi hii sasa kutaka nitoe agizo kwa Wakuu wa Mikoa wote kuhakikisha kwamba Kamati hizi sasa tuwape *deadline* ndani ya miezi mitatu kuanzia siku ya leo ziundwe hizi Kamati, Wakuu wa Mikoa wahakikishe Kamati hizi zinaundwa katika Mikoa, Halmashauri, Kata na Vijiji na zaidi ya hapo tutachukua hatua kwa sababu maagizo mengine kama haya yana umuhimu mkubwa kwa sababu yanazaa tena mafanikio mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Mheshimiwa Mbunge hapa anauliza katika bajeti hajaona kitu chochote kilichotengwa kwa ajili ya ulemavu, pamoja na kwamba sekta mbalimbali zinashughulika na jambo la walemavu na kwamba suala la ulemavu ni suala mtambuka, lakini sisi kama Mamlaka ya Serikali za Mitaa tunatafakari maombi makubwa yaliyoletwa wakati wa mjadala wa bajeti ya Wizara yangu ambapo maoni mengi ikiongozwa na Mheshimiwa Ikupa alisema wanaomba basi angalau asilimia mbili ya *own source* ya makusanyo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa iwekwe kwa ajili ya Walemavu na hili ni jambo ambalo tumeliafiki kwa hatua za awali, lakini tutaendelea kullitafakari kuona namna gani tunalitekeleza. Sasa inawezekana pia likatekelezwa vizuri endapo Kamati hizi sasa zitaundwa katika *level* hizi zote za Mkoa, Wilaya, Kata, Halmashauri na Vijiji. Zikiwepo hizi Kamati ndiyo rahisi kutekeleza hata huo mgawanyo wa hiyo asilimia mbili ya makusanyo ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, nikubaliane kabisa kwamba Serikali tuko tayari na tutahakikisha kwamba tunalisimamia jambo hili vizuri kabisa. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA AJIRA NA WENYE ULEMAMU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Simbachawene kwa jibu la nyongeza namba moja lililokuwa linahusu Kamati kwa mujibu wa Sheria Namba 9 ya mwaka 2010 ya Huduma za Walemavu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongeze majibu ya ziada kwa swali la nyongeza namba mbili linalohusu Mfuko wa Walemavu ambao nao unazingatia Sheria Namba 9 ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anasoma bajeti yake na kuhitimisha hoja yake hapa ndani, alilieleza Bunge lako Tukufu kupitia utaratibu ambao tumejiwekea wa Vikao vya Baraza la Watu Wenye Ulemavu ambalo sasa limeanza kufanya kazi. Tumeanza pia kufanya kazi ya kufanya mapitio ya kuona ni namna gani Serikali inaweza kushughulikia pia mfuko huo wa watu wenye elemavu, vilevile kushirikiana na nguvu hizo nyingine ambazo zimesemwa mbele ya Bunge lako Tukufu ambazo zinaweza zikasaidia watu wenye elemavu wakapata fursa sawa na watu wengine wote katika nchi yetu ya Tanzania, kupitia mifuko mbalimbali ambayo imeanzishwa na mingi ikiwa inasimamiwa na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kuwa suala hili linafanyiwa kazi kwa kina sana na linaratibiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ndani ya ofisi yake na tutaendelea kulifanyia kazi ya kutosha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Desderius Mipata.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, walemavu wanakabiliwa na changamoto nyingi sana na mara nyingi changamoto

hizi hubaki zinawakabili wanafamilia, ikitokea bahati mbaya familia ikawa na uwezo mdogo sana, shida huwa kubwa. Je, Serikali iko tayari kuwapa walemavu wote nchini msamaha wa matibabu kama ilivyo kwa wazee, wakiwemo watu wenye ulemavu wa ngozi ambao matibabu yao huhitaji utaalumu wa kibingwa zaidi?

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Saleh huwa hakuna taarifa saa ya kuuliza swali, ni saa ya kuchangia. Sasa nitakuruhusu kwa sababu swali lenyewe linakuhusu na wewe.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, sawa ninachotaka kusema, najua kwamba hakuna utaratibu wakati huu, lakini nilitaka kusahihisha, siyo watu walemavu, siyo *polite and correct language*, unasema watu wenye ulemavu.

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa kutukumbusha na taarifa zetu za Bunge ziandike hivyo kwa usahihi. Mheshimiwa Waziri wa Afya.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mijibu wa Sera ya Afya ya mwaka 2002 inatambua makundi ambayo yanatakiwa kupata msamaha wa matibabu, ikiwemo watu wenye ulemavu wasio na uwezo, maana siyo kila mtu mwenye ulemavu hana uwezo. Watu wenye ulemavu wasio na uwezo hao wanaweza wakapata huduma za matibabu bila malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba kwa wazee siyo wazee wote hawana uwezo, tunao wazee humu ni Wabunge wana uwezo. Kwa hiyo, sera inasema wazee wasio na uwezo, naomba hili lieleweke wazi kwa watoa huduma wote. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Sawa. Waheshimiwa Wabunge

tumepata maswali marefu na majibu marefu pia, kwa hiyo tutaendelea na Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba sasa aulize swali lake.

Na. 186

Barabara za Mitaa Mji wa Kahama Kujengwa kwa Kiwango cha Lami

MHE. SALOME W. MAKAMBA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Rais aliyoitoa wakati wa kampeni kwa wananchi wa Jimbo la Kahama Mjini ya kujenga kwa kiwango cha lami kilometa 10 za barabara za mitaa ya Mji wa Kahama?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya kwanza ya utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais ilikuwa ni kuzitambua barabara zitakazojengwa kwa kiwango cha lami katika Halmashauri ya Mji wa Kahama ambayo imekamilika. Ujenzi huo utahusisha barabara ya Mama Farida yenye urefu wa kilometa 1.305; barabara ya Phantom - Majengo yenye urefu wa kilometa 5.214; barabara ya Malunga Mashineni - Mwamvua yenye urefu wa kilometa 1.852, barabara ya Nyihogo - Namanga yenye urefu wa kilometa 0.6, barabara ya Florida - Stendi ndogo yenye urefu wa kilometa 0.829 na barabara ya Royal ya Zamani - Stendi Ndogo yenye urefu wa kilometa 0.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara hizo utafanyika kwa awamu ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018, zimetengwa shilingi 603,604,733 kwa ajili ya

kujenga barabara yenye urefu wa kilometa moja kwa kiwango cha lami. Vilevile, kupitia fedha za Mfuko wa Barabara, zimetengwa shilingi 320,000,000 kwa ajili ya ukarabati wa barabara za lami zenye urefu wa mita 800 katika Mji wa Kahama.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Waziri umetuaminisha kwamba mmetupatia shilingi milioni 600 kwa ajili ya kujenga barabara na pia mmetupa shilingi milioni 320 kwa ajili ya kukarabati barabara hizi. Mheshimiwa Waziri barabara ya Phantom-Majengo, ni barabara ya muhimu kweli na barabara hii inachangia pato la Halmashauri kwa asilimia 25. Barabara hii ina urefu wa mita tano na tunasema tunataka tufanye Serikali ya viwanda, kule kuna viwanda vidogo vidogo vya mazao ya mpunga na mahindi.

Mheshimiwa Waziri, hauoni kama kuna umuhimu wa kuingiza barabara hii katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha ili tuweze kutekeleza mpango huu wa Tanzania ya viwanda kwa kuendelea kuzalisha na magari yaweze kupita? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Ushetu, Mheshimiwa Waziri mmetenga shilingi milioni 181 tu kwa ajili ya barabara na tena ni kwa ajili ya ukarabati tu wa barabara, lakini nikufahamishe kwamba kule hakuna barabara hata moja ya lami, barabara zote ni za vumbi na fedha mliyotenga ni kidogo na ile ni Halmashauri mpya. Unawaambia nini Watanzania wa Ushetu, watawezaje kupata barabara nzuri za lami ilihali mmewatengea fedha kidogo namna hii, nini mpango wa Serikali kwa Halmashauri hii mpya? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome kwenye swali lako la nyongeza ya kwanza, kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawasawa ni mita tano au ulimaanisha kilometa ama ulimaanisha kitu gani, hebu weka vizuri ili watu wa kumbukumbu waweke sawa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nilimaanisha kilometa tano.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, Mji wa Kahama kimkakati tunafahamu na ndio maana hata ninyi katika Mji wa Kahama mlikuwa mnapeleka maombi kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi kwamba Mji ule sasa uwe Manispaa kwa kadri unavyokua. Ukiangalia barabara ya Phantom - Majengo ina kilometa 5.2 ni barabara ya kimkakati ina jukumu kubwa sana, ndiyo maana tumesema mwaka huu tumeanza kutenga fedha hizo. Hata hivyo, unafahamu Mji wa Kahama siyo barabara hii tu ndiyo tunaanza kujenga, kuna miundombinu ya barabara za lami pale zilikuwa zinaendelea na mimi nilifika pale miezi michache iliyopita kuja kukagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu letu kubwa tunajua kwamba eneo hili ni eneo la mkakati, kama Serikali tutafanya kila liwezekanalo, lakini siyo Mji huu peke yake. Serikali tumejipanga kuna ahadi za Mheshimiwa Rais katika maeneo mbalimbali, hivi sasa ukiangalia katika Halmashauri mbalimbali, juzi Mheshimiwa Rais alikuwa kwa ndugu yangu pale Mheshimiwa Mbowe, alikuwa akiangalia miundombinu ya barabara. Pia nchi nzima hata kwa Mzee Lubeleje kule Mpwapwa kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tunachotaka kufanya ni kwamba ndani ya miaka mitano tufanye mabadiliko makubwa sana katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa katika ujenzi wa barabara za lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaondoe hofu Waheshimiwa Wabunge, siyo kwa Mji wa Kahama peke yake isipokuwa katika miji mbalimbali katika Halmashauri zetu hizi tutahakikisha ujenzi wa barabara za lami hasa kutumia fedha za *World Bank* ambayo Serikali imechukua *commitment* ya kutosha kubadilisha miji yake yote iweze kubadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninyi ni mashahidi

mnaifahamu sasa hivi, Halmashauri za Miji nyingi sasa hivi na Manispaa zimebadilika katika suala la ujenzi wa barabara za lami TAMISEMI imeamua kufanya hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu eneo la Ushetu kama ulivyosema ni kwamba tunafahamu Ushetu ni Halmashauri mpya na ndiyo maana, ndugu yangu hapa Mheshimiwa Elias Kwandikwa kila siku anapambana na Jimbo lake la Ushetu, kama unavyopambana Mheshimiwa Mbunge hapa. Naomba kuahidi kwamba kwa kutumia Mfuko wa Barabara, nikuahidi tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo tutahakikisha maeneo ya Ushetu na maeneo mengine tutaweka nguvu za kutosha na hasa hizi Halmashauri mpya tutaweza kuzifungua ili wananchi kule waweze kupata huduma wajisikie huru kama wananchi wenzao wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Mheshimiwa Waziri Mji wa Ifakara ni Halmashauri mpya, kutokana na upya wake bado ni changa. Barabara zetu bado ziko katika *level* ya tope, kutokana na mvua hizi ambazo kule zinanyesha barabara zinaharibika sana. Sisi kama Halmashauri tunajaribu kuziwekea vifusi lakini kwa sababu ni Halmashauri mpya, hatuna fedha za kutosha kuweza kujenga lami.

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia Halmashauri ya Mji wa Ifakara, Halmashauri ambayo ni mpya ili iweze kuboresha barabara zake, ziweze kuwa katika kiwango cha lami?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nafahamu Kilombero na maeneo mengine, naomba niwape pole Wabunge wote kwa sababu nikijua wazi kwamba kipindi hiki mvua zinanyesha, barabara nyingi sana katika maeneo yetu zimeharibika vya kutosha. Ndiyo maana katika bajeti yetu ya mwaka huu, tuliyoipitisha tumetenga karibuni shilingi milioni 247 mwaka huu wa fedha 2017/2018 ili kuhakikisha tunafikia maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa sitaki kutoa *commitment* ya uwongo kusema kesho Kilombero pale Ifakara tutakuja kujenga barabara za lami, itakuwa ni uwongo. Kikubwa zaidi tutaangalia jinsi gani tutafanya kwa bajeti iliyopo sasa, kwa sababu tunakwenda awamu kwa awamu. Tulikuwa na miji mikuu, tumeenda na manispaa, tunaenda katika halmashauri za miji, tunaangalia jinsi gani tutafanya kwa sababu kila barabara zingine zinawekewa kifusi ili barabara iweze kupitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *commitment* ya Serikali ni kuhakikisha wananchi wake wanaweza kufikiwa, wanaweza kusafirisha mazao yao na hata kusafiri sehemu zingine, hii ni *commitment* ya Serikali. Hivyo, tutajitahidi kufanya kila liwezekanalo bajeti iliyotengwa katika eneo hilo tutaisimamia vizuri, kwa sababu changamoto kubwa ni usimamizi wa bajeti katika maeneo yetu wakati mwingine. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, leo naona unapata maswali mawili asubuhi.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tatizo la Mji wa Kahama kama sahihi kabisa alivyozungumza Mheshimiwa Naibu Waziri linafanana kwa njia moja au nyingine na ahadi za Rais alizotoa wakati wa kampeni, ni kweli Rais wakati wa kampeni alitoa ahadi ya kujengea Halmashauri ya Wilaya ya Hai kilometa tano za lami katika Mji wa Hai katika kipindi chake cha uongozi. Na ni kweli kwamba hivi majuzi Rais alivyokuwa katika ziara kwenye Mkoa wetu wa Kilimanjaro aliulizwa kuhusu ahadi yake na Rais akauliza vilevile Halmashauri imegawiwa fedha kiasi gani katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya Mfuko wa Barabara. Taarifa ambazo Rais alipewa ni fedha ambayo ilikuwa imepangwa kwenye bajeti ambayo ni shilingi bilioni 1.3 lakini hiyo fedha haijapokelewa kwa sababu haijatolewa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba Rais aliagiza kwamba TAMISEMI wakafanye uchunguzi, nakaribisha sana TAMISEMI mkafanye uchunguzi, lakini ukweli ni kwamba fedha pekee ambayo ilishapokelewa ni kama shilingi bilioni 300 ambayo ni lazima mtambue kwamba Wilaya ya Hai ina zaidi ya kilometa 200 za barabara zinazoteleza za milimani ambazo ni lazima zifanyiwe *routine maintenance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri ni wewe kutoa *commitment* ya kwenda kufuatilizia alichokizungumza Rais, lakini vilevile kukumbushia ahadi ya Rais ya kilometa tano za Halmashauri ya Wilaya ya Hai katika Mji wa Hai, bado ni muhimu sana kwa sababu Mji unakuwa kwa kasi na una zaidi ya wakazi 50,000 ambao kwa kweli hawana hata robo kilometa ya lami katika Mji wa Hai ukiacha barabara ya kwenda Arusha. Mheshimiwa Waziri naomba *commitment* yako.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni na hata baada ya kampeni amekuwa akiahidi kufanya mambo mbalimbali hasa anapooni maeneo fulani yana matatizo. Katika eneo la barabara ametoa ahadi maeneo mbalimbali ikiwemo Kasulu kilometa sita na hapa Mheshimiwa Mbowe anasema kilometa tano na hasa barabara za milimani, lakini ameahidi maeneo mengi, Waheshimiwa Wabunge wana ahadi na wana kumbukumbu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, kwamba ahadi za Mheshimiwa Rais zitatekelezwa na kwa sababu bado tunao muda na tutaangalia kama utaratibu mzuri ni wa kuzingatia wakati wa bajeti zetu lakini nafahamu mnafahamu kwamba bajeti zetu huwa zina ukomo, kwa hiyo tutajaribu kuangalia namna ya *modality* nzuri ya kuweza kutekeleza hili tukimshirikisha aliyeahidi.

Pia nitoe rai tu kwa wenzangu kwamba wakati tunaposimamia ahadi za Mheshimiwa Rais pia tuwe tunakumbuka kuishi naye vizuri na kumheshimu. Ahsante sana. (Makofi)

Na. 187

Hitaji la Gari la Wagonjwa - Nsimbo

MHE. RICHARD P. MBOGO aliuliza:-

Vifo vya mama na mtoto vinachangiwa na huduma hafifu ikiwemo ukosefu wa usafiri hasa gari la kubebea wagonjwa (*ambulance*).

Je, ni lini Serikali itatoa gari la wagonjwa kwa Jimbo la Nsimbo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Nsimbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo ina jumla ya vituo vya afya vitatu. Kituo cha Afya cha Katumba, Kituo cha Afya cha Kanoge na Kituo cha Afya cha Mtisi vinavyohudumiwa na gari moja la wagonjwa. Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo ina upungufu wa magari mawili. Kwa kuzingatia changamoto hiyo, Halmashauri imetenga jumla ya shilingi milioni 220 katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya ununuzi wa gari la wagonjwa ili kuharakisha huduma za rufaa na kupunguza vifo vya akina mama na watoto.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali, naomba tu niipe taarifa Serikali kwamba hiyo fedha imetengwa shmilioni 220 siyo sahihi ni

fedha ambayo ipo kwenye maombi maalum, kwa sababu binafsi nilipitia bajeti ya Halmashauri yote, *CDG* tulipewa shilingi bilioni 1.24; *allocation* ya gari la wagonjwa haikuwepo kutokana na fedha kuwa ndogo na mahitaji ya Jimbo la Nsimbo kwa upande wa elimu, afya, na maeneo mengine kuwa na uhitaji zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo gari moja lililopo ni msaada ambao Jimbo la Nsimbo lilipata kutoka Shirika la Kuhudumia Wakimbizi (*UNHCR*), tunashukuru kwa mgao huo, kutokana na Jimbo kuwa na makazi ya wakimbizi kwenye Kata ya Katumba.

Je, Serikali haioni ule mpango tuliouleta wa maombi maalum wakachukua kile kipengele tu cha gari la wagonjwa, watuidhinishie ile Halmashauri yetu tuweze kupata gari hilo au laa, hatuna wasiwasi na utekelezaji wa ahadi mbalimbali za Serikali kuhusiana na kujali afya za wananchi wake kwa kutoa magari ya wagonjwa, kama hivi juzi Mheshimiwa Rais ametoa magari matatu je, Serikali haioni tena kuna umuhimu wa Jimbo la Nsimbo na lenyewe likaangaliwa kupata gari la wagonjwa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nimesema kwamba kwanza tumewashukuru wenzetu wa Nsimbo na Mheshimiwa Mbunge naomba nikushukuru sana kwa kuonesha *commitment* yenu kwamba kulikuwa na hili hitaji ya gari. Ndiyo maana naomba niseme kwamba, kwa kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Tano, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, Mheshimiwa Rais na Serikali yake amejipanga sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri umesuhudia hapa kwamba, juzi Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Ally Kessy Mohamed na wenzie Mheshimiwa Rais alitoa magari matatu *personally* pale, lakini kuna magari mengine 50 yaliweza kupelekwa katika maeneo mbalimbali. Hii yote ni jukumu la Serikali kuwahudumia wananchi. Hivyo, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Richard Mbogo kwamba

tutaangalia kile kinachowezekana ili kulisaidia Jimbo lako ambalo liko mpakani kabisa ili suala hili la gari la wagonjwa na yale mambo mengine ya msingi likiwemo suala zima la ujenzi wa kituo cha afya, kufanya ukarabati katika eneo lako tualifanya. Serikali ya Awamu ya Tano lengo kubwa ni kuwapunguzia adha akina mama na watoto. (*Makofi*)

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mazingira yaliyopo Nsimbo yanafanana kabisa na mazingira yaliyopo katika Jimbo la Kavuu na kupitia *initiative* ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja kwenye ziara katika Jimbo la Kavuu alitomba tuanzishe Hospitali ya Halmashauri ya Mpimbwe kufuatia kuwepo na kadi za CHF kwa sababu za NHIF hazitumiki kule.

Je, Serikali sasa haioni kuna umuhimu, kutokana na juhudi za wananchi wa Jimbo la Kavuu kuwapatia gari la wagonjwa ambao wamekuwa wakitumia umbali mrefu kutoka Mpimbwe kwenda Mpanda na sasa tutumie katika Jimbo la Kavuu? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi sana huwa nazungumza hapa Bungeni kwamba, *issue* ya gari la wagonjwa ni vema kwanza tukai-*allocate* katika bajeti zetu za kila mwaka, hilo ni jambo la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu sana Mheshimiwa Dkt. Kikwembe anavyohangaika kwa Jimbo lake, ndiyo maana hapa juzi alikuwa anahangaika tupeleke huduma za afya pale na ndiyo maana tulimhakikishia pamoja na Waziri wa Afya, na Mheshimiwa Waziri Mkuu alienda pale na akatoa ahadi, tutaenda kufanya ukarabati mkubwa wa kituo chake cha afya kwa kuingiza fedha nyingi ili akina mama na watoto sasa waweze kupata huduma nzuri, hasa huduma ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Kikwembe mahitaji yako ambayo umeongea mbele ya Waziri Mkuu, Serikali imeyachukua kwa ujumla wake, hata hivyo, naomba nipendekeze, kwa Wabunge mbalimbali katika suala la *ambulance* lazima tuliainishe katika bajeti zetu, likishakuwepo katika bajeti tunapata msingi mzuri wa kulifanya jambo hilo katika utekelezaji wake.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Daniel Mtuka.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la gari la wagonjwa Jimbo la Nsimbo ni sawasawa kabisa na tatizo hili linalotukabili Wilaya ya Manyoni. Tunayo Hospitali kubwa ya Wilaya pamoja na vituo viwili vya afya vya Nkonko pamoja na Kintinku. Magari tuliyonayo ni chakavu sana na kumekuwa na matukio mengi ya kubeba wagonjwa na magari yanaharibika njiani mpaka kulala njiani, inabidi utoe gari sasa kutoka Manyoni Mjini kwenda kufaulisha wale wagonjwa.

Je, ni lini Serikali sasa itatupatia nasi angalau gari la wagonjwa kwa Wilaya ya Manyoni ukizingatia hali halisi ya Manyoni pale, kuna ajali nyingi zinatokea kwenye ule mlima wa Saranda Sukamahela?

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa lugha ya kwetu sisi, ndiyo maana mwanzo nilianza na kile kitu kinaitwa *kingilambago*. Nilieleza pale awali kwamba, lazima hili jambo tuliainishe katika suala zima la mpango wetu wa bajeti. Mheshimiwa Mtuka naomba nikuhakikishie kwa sababu nami nilifika pale Manyoni, kwanza nilitoa maelekezo katika hospitali yako kwa sababu, hata hili suala la *referral* ni lazima maeneo yetu watu wafanye kazi vizuri, niligundua baadhi ya uzembe pale katika watalaamu wetu, nikatoa

maelekezo. Jambo hili naomba nikuhakikishie katika mpango wako wa bajeti 2018/2019 naomba liainishwe wazi na likifika kwetu katika Ofisi ya TAMISEMI tatalipa nguvu ili kwamba eneo la Manyoni pale tupate gari la wagonjwa.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mimi swali langu dogo tu, nilikuwa naomba, maana uzoefu inaonekana kama Waziri Mkuu ama Waziri wa TAMISEMI anafika katika eneo kuangalia hali halisi ya matatizo ndiyo pale inapomuuma katika moyo na kutoa kipaumbele katika haya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba ni lini sasa Waziri wa TAMISEMI ama Waziri Mkuu atafika kwenye Jimbo la Mlimba ili aangalie matatizo alie na machozi halafu aone *sympathy* ya kuwasaidia wananchi wa Mlimba katika masuala ya magari, afya na mambo mengine? Ni hapa tu. (*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kiwanga kwamba tulifanya ziara ofisi yetu, tumetembelea Halmashauri zote kati ya Halmashauri 185 tumebakisha chini ya Halmashauri kumi hivi sasa na moja ikiwa yako ya Mlimba. Ndiyo maana tumekubaliana hapa na nimezungumza katika kipindi mbalimbali kwamba baada ya Bunge nitakuwa na *session* maalum katika Mkoa wa Morogoro kumaliza Halmashauri zilizobaki na Mkoa wa Songwe, vilevile nitaenda kule Ukerewe pamoja na Mara ambako kuna Rorya, Tarime na Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo tunaenda kuyafanya lengo kubwa ni kufikia maeneo mbalimbali tubadilishane mawazo tikiwa *site* kule tukubaliane, tubaini changamoto halafu tujadiliane, nini tutafanya ili kuwahudumia wananchi. Kwa hiyo, naomba nikutoe hofu katika hilo tutaenda kulifanya katika kipindi cha sasa. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa

Vedasto Edgar Ngombale, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 188

Kupeleka Huduma ya Mawasiliano ya Simu – Jimbo la Kilwa Kaskazini

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE aliuliza:-

Maeneo mengi ya Jimbo la Kilwa Kaskazini bado hayajapata huduma ya mawasiliano ya simu kama vile kata za Kibata, Kinyumbi, Kandawale na vijiji vya Nandete na Mkarango.

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma hii katika maeneo hayo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vya kata za Kibata, Kinyumbi, pamoja na vijiji vya Nandete na Mkarango kutoka katika kata ya Kipatimu, Jimbo la Kilwa Kaskazini vitafikishiwa huduma ya mawasiliano ya Kampuni ya Simu ya Viettel kupitia utekelezaji wa awamu ya tatu ya mradi unaotegemewa kukamilika ifikapo Novemba, 2017. Aidha, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, itaainisha vijiji vya kata ya Mandawale na kuviingiza katika orodha ya miradi kwa ajili ya zabuni za siku za usoni kulingana na upatikanaji wa fedha.

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri katika jibu lake la msingi amesema kwamba vijiji vya Mkarango na Nandete katika kata ya Kipatimu na vijiji vya Kata ya Kinjumbi na Kibata vitapata mawasiliano katika mradi utakaokamilika ifikapo Novemba, 2017; sasa tunazungumza ni mwezi Mei. Nataka nijue tu, je, programu ya utekelezaji wa miradi hiyo umeshaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kumekuwa na utaratibu kwa kampuni moja kujenga minara ya simu, baadae makampuni mengine kuja kufunga mitambo yao ya mawasiliano. Nataka nijue katika kata ya Chumo pana kampuni imejenga mnara wa simu na kuna kampuni moja tu ya Vodacom ndiyo imefunga mitambo yake ya mawasiliano.

Je, ni lini makampuni ya Airtel na Tigo yatakuja kufunga mitambo yao ya mawasiliano, ili kutanua wigo wa mawasiliano kwa wananchi wa kata ya Chumo? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kutokana na jibu la msingi kwamba ifikapo Novemba mwaka 2017, mwaka huu tulionao kwamba, miradi ambayo inaendelea itakuwa imekamilika. Kwa msingi wa jibu hilo ni kwamba, programu hii inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la pili, amesema kwamba, kuna Kampuni ya Viettel imetajwa, lakini kuna Kampuni ya Vodacom, kuna Kampuni za Tigo, umeona kampuni moja ipo pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala moja dogo Mheshimiwa Mbunge, ni suala la fizikia nyepesi tu kwamba hii minara inafanya kazi kwa kutegemea mawimbi na mawimbi ya Vodacom, mawimbi ya Airtel, minara ya Airtel, mawimbi ya Viettel ni mawimbi yanayotegemeana, kwa hiyo, kukishakuwa na Mnara mmoja wa Vodacom unarahisisha pia Mnara wa Viettel kuja kujengwa pale. Kwa

hiyo, ukishatangulia mnara mmoja, basi tarajia kabisa kwamba, na minara mingine na makampuni mengine yatakuja kuwekeza kwa sababu kumeshakuwa na urahisi wa kuwepo mawimbi katika lile eneo. *(Makofi)*

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Matatizo ya Mawasiliano ambayo yanalikabili Jimbo la Kilwa Kaskazini yanafanana na yale ya Jimbo la Nanyamba kwa sababu kuna kata za Njengwa, Nyundo, Nitekela na Kiyanga ambayo hayana mawasilinao. Na nilishawahi kuuliza swali hili hapa Bungeni nikaambiwa kwamba Mfuko wa Mawasiliano utapeleka mawasiliano huku na mradi huo bado mpaka sasa hivi haujatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nipate majibu ya Serikali kuhusu miradi hii? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO): Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Mawasiliano upo na huu unatekelezwa moja kwa moja na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini pia kuna programu nyingine ambayo ni ya watu binafsi ambao wamependa kuja kuwekeza katika nchi yetu. Kwa hiyo, kama hukupata kwenye mradi wa mawasiliano, basi tarajia pia unaweza ukapata kwenye hawa wawekezaji ambao wamekuja kufanya biashara kwenye eneo letu la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika hoja yako tayari umesema tayari ulishaahidiwa kupitia kwenye huu Mfuko wa Mawasiliano, Mheshimiwa Mbunge, niseme tu kwamba hebu tuvute subira kidogo, kama umeshaahidiwa hili lazima litatekelezwa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tupunguze kelele kidogo ili tuweze kuelewana humu ndani.

Tutaendelea, Wizara ya Nishati na Madini. Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 189

Usambazaji wa Umeme wa REA – Vijiji vya Same Magharibi

MHE. DKT. DAVID M. DAVID aliuliza:-

Vijiji 48 vya Jimbo la Same Magharibi vyenye zaidi ya kaya 2,943 havijapatiwa umeme wa REA japokuwa vina mahitaji makubwa ya umeme.

Je, ni ipi ratiba ya kuwasambazia umeme wananchi hawa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi kabambe wa usambazaji umeme vijijini awamu ya tatu umeanza nchi nzima tangu Machi, 2017. Mradi huu unajumuisha vipengele vya miradi vitatu vya *Densification, Grid Extension* pamoja na *Off Grid Renewable*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zitakazofanyika ni kuongeza wigo wa usambazaji umeme katika vijiji, vitongoji vyote, taasisi za umma na maeneo ya pembezoni ambayo hayajafikiwa na miundombinu ya umeme, ikiwa ni pamoja na visiwa.

Mradi wa REA Awamu ya Tatu utakamilika mwaka 2020/2021. Vijiji vya Jimbo la Same Magharibi vitapatiwa umeme kupitia mradi huu wa REA Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kupeleka umeme katika vijiji hivyo itahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 67.81. Ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 261, ufungaji wa transfoma 43 pamoja na kuwaunganishia umeme wateja 2,457.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii itagharimu shilingi bilioni 10.8.

MHE. DKT. DAVID M. DAVID: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana, lakini naipongeza Wizara hii kwa kuwa makini katika kufanya kazi katika sekta hii ya nishati na madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijauliza maswali mawili ya nyongeza ningependa kuwapa pole wananchi wa Jimbo la Same Magharibi, hususan kata ya Hedaru ambao wamepoteza nyumba nyingi pamoja na mifugo na mazao kutokana na mvua kubwa iliyonyesha usiku wa kuamkia juzi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu *Subhuhana Wataallah*, aweze kutupa mvua za kiasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza, katika Mradi wa *REA* Awamu ya Pili, mkandarasi ambaye anaitwa *SPENCON* alishindwa kufanyakazi na kwa hiyo, vijiji vingi pamoja na vitongoji vingi vya Jimbo la Same Magharibi hususan vijiji 48, umeme haujakamilika kutokana na kwamba, mkandarasi huyo alishindwa kazi.

Je, *REA* Awamu ya Tatu, vijiji hivi ambavyo vilikosa umeme pamoja na vitongoji vyake, Serikali ina mkakati gani katika kuhakikisha kwamba, vitongoji vyote vinapata umeme na vijiji vyangu vyote vya Jimbo la Same Magharibi katika Awamu hii ya Tatu ya *REA*?

Swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari baada ya Bunge hili la Bajeti kuongozana na mimi kwenda katika Jimbo la Same Magharibi, ili akajionee mwenyewe vijiji na vitongoji ambavyo havina umeme katika Jimbo langu? Ahsante sana. (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, awali ya yote niungane na Mheshimiwa David kuwapa pole wananchi wake kwa tatizo walilopata.

Mheshimiwa Nibu Spika, kulingana na maswali yake mawili ni kweli kabisa katika utekelezaji wa *REA* Awamu ya Pili, Mikoa miwili ya Kilimanjaro na Singida haikukamilika ipasavyo na ni kweli kabisa mkandarasi *SPENCON* hakufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kutoa taarifa pia ya hatua za Serikali ambazo zilichukuliwa kutokana na kutofanya kazi vizuri kwa mkandarasi huyo. Hatua ya kwanza tulichukua asilimia 10 ya mkataba wake ambayo ni *retention* kimkataba kabisa. Hatua ya pili, kazi hiyo sasa atapewa mkandarasi mwingine ili aikamilishe vizuri na wananchi wa Same waendeleo kupata umeme. Lakini hatua ya tatu, tunaendelea sasa kuchukua hatua za kisheria, ili Wakandarasi wa namna hiyo sasa wapate fundisho waache kuwakosesha miundombinu wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David kwamba wananchi wa Same, vijiji vyako vyote 48 vitapata umeme. Naelewa viko vijiji vya milimani kwa Mheshimiwa Dkt. David kijiji cha Muhezi, Malaloni kule Malalo pamoja na kwa Hinka, vitapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika naelewa vile vijiji 48 anavyosema Mheshimiwa, yapo maeneo kama kule Hedaru, yako maeneo kule ambako Mheshimiwa tumesema Chekereni, Mabilioni pamoja na Jificheni Mabilioni, pamoja na kijiji cha Njiro vyote vitapata umeme. Hivyo, ninakuhakikishia kwamba vijiji ambavyo havijapata umeme

kwenye REA II, sasa vyote vitapata umeme. Siyo vijiji tu hata vitongoji vyake na taasisi za umma pamoja na maeneo mengine muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala lake la pili la kuongozana naye, kwanza kabisa niko tayari, ninaweza nikasema utakaponikaribisha utakuwa umechelewa, ukichelewa sana utanikuta kwenye Jimbo lako, kwa hiyo, niko tayari kutembelea kwenye Jimbo lako. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekimbia sana kwa hivyo, maswali tutaishia hapo, lakini niwatoe wasiwasi, chati iko hapa mbele kwa maswali ya nyongeza. Kwa hiyo, mtu anayeitwa kuna mawili, ama amewahi sana ama hana swali hata moja ama ana moja. Kwa hiyo, ambaye ana maswali mengi zaidi, labda kuwe hakuna Mbunge mwingine anayetaka kuuliza swali la nyongeza kwenye swali hilo.

Kwa hiyo, niwaondoe wasiwasi, ile karatasi iko hapa mbele, hamna mtu anayeonewa au anayepewa nafasi chache kuliko wengine.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na tangazo la Wageni walioko hapa Bungeni leo. Tunao wageni 75 wa Spika wa Bunge Mheshimiwa Job Ndugai ambao ni wanafunzi 70 na walimu watano kutoka shule ya Sekondari ya Kongwa iliyopo Mkoani Dodoma wakiongoza na Mwalimu Joachim Mpagama. Karibuni sana walimu na wanafunzi kutoka Kongwa. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 12 na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni (KUB) Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, ambao ni viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kutoka Jimboni kwake Hai, Mkoani Kilimanjaro, wakiongozwa na Mheshimiwa Joel Nkya ambaye ni Diwani wa Bomang'ombe kutoka Wilaya ya Hai, karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Mbowe. *(Makofi)*

Tunao pia wageni saba wa Mheshimiwa Balozi Adadi

Rajab ambao ni Wawekezaji kutoka nchini China, wakiongozwa na Ndugu Yu Xiumei. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wanafunzi waliokuja kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine kutoka kwa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambaye ni Mratibu wa Mfuko wa Faraja kwa Wabunge, anawatangizia Waheshimiwa Wabunge ambao ni wanachama wa Faraja kwamba leo kutakuwa na Mkutano Mkuu wa mwaka utakaofanyika saa saba mchana, mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge na Mkutano huo utafanyika eneo la Bunge upande wa chini ya ukumbi huu, ambao ukitoka upande wa kushoto utaziona ngazi zikielekea huko hili eneo linaitwa *Basement*. Kwa hiyo, mnakaribishwa huko ili muweze kufanya kikao hicho mnasizitizwa wote kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tutaendelea.

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Tusikilizane Wabunge, kwa sababu kama nilivyosema kwamba sitachoka kuzungumza ukisimama kuhusu mwongozo, ukazungumza jambo ambalo halijatokea hapa ndani na wala swali lako siyo kwamba linaruhusiwa ama haliruhusiwi nitakukatisha kabla hujamaliza.

Mheshimiwa Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Jana na leo kuna vuguvugu ambalo linaendelea la uchaguzi tuliomaliza wa Afrika Mashariki. Nilikuwa naomba Mwongozo wako, kwa kuwa niliwahi kushutumiwa kutokana na uchaguzi huo kutokana na ushauri nilioutoa ukaitwa matusi, ukafanyiwa kazi kwa muda wa

wiki mbili na uongozi wa CHADEMA matokeo yake wakaufuata, wakaleta wagombea wanawake na matokeo yake mmeyaona yamezaa matunda chanya, wanawake wamechaguliwa kwa kishindo, lakini nilipohoji niliambiwa nimetukana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mmwongozo wako, kwa kuwa kwanza nia yao ilikuwa kunigombanisha kati yangu na kiti chako kwa kusema kuwa unanibeba, pili kunigomanisha na Watanzania wote kuonekana Mlinga anafanya kazi ya kutukana Bungeni.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mwongozo wako nataka uongozi wa CHADEMA uniombe radhi kwa kuwa wameufanyia kazi ushauri wangu ambao niliutoa. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mlinga hilo vuguvugu mimi silifahamu kwa hivyo hakuna mwongozo juu ya jambo hilo. Mheshimiwa Haonga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7), juu ya jambo lililotoa hapa Bungeni leo mapema.

Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI alipokuwa anajibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbowe, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Swali Namba 186, Mheshimiwa Simbachawene alijibu kwa kiongozi huyu kwamba wakati mnaomba barabara huko kwenye majimbo yenu akae vizuri na Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba labda Mheshimiwa Simbachawene aweze kulithibitishia Bunge hili kama Mheshimiwa Mbowe, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kama ana mahusiano mabaya na Rais; wakati huo huo atuambie je, huo siyo uchochezi kati ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na wananchi pia kati ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchochezi huu naomba Mwongozo wako kama kitendo cha namna hii unavumiliwa katika Bunge hili ambalo tunaamini kwamba sisi wote tunaishi kama ndugu na tunaamini kabisa kwamba haitakiwi kwa kiongozi kama huyu kutoa majibu kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kama haya maneno ya Waziri yanaruhusiwa kumfanyia hivi Mheshimiwa Mbowe. Ahsante sana.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuomba mwongozo.

Na mimi nimesimama kwa Kanuni ya 68(7), pamoja na kwamba umesema jambo litokee sasa hivi lakini kwa kuwa jambo ninalozungumza linahusu haki za Bunge naomba Mwongozo wako na naomba kwa ridhaa yako uniruhusu nilizungumze jambo hili.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kubenea kama wewe umeshasema unataka kwenda kwenye jambo lingine suala kama linahusu haki za Bunge tumia Kanuni nyingine siyo inahusu Mwongozo. Kama unataka kuzungumzia mwongozo jambo live limetokea hapa ndani kwa mujibu wa hiyo Kanuni ambayo unaitumia. Sasa nakupa nafasi ama uzungumzie jambo lililotoa hapa kama unataka kuzunmguzia lingine tumia Kanuni inahusika.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Naibu Spika, natumia kanuni ya 47 pamoja na Kanuni ya 68(7). Ibara ya 89 Sura ya Tatu inayozungumzia Utaratibu, Madaraka, Haki za Bunge. Sura ya Tatu inazungumzia kuwepo Kanuni za Bunge na zimetambuliwa kwenye Katiba hii. Katika Kanuni zetu Kanuni ya 16(1) na 16(3) inazungumzia kuwepo Wanadhimu wa pande mbili wa Serikali na wa Upinzani katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, umekuwa ni utaratibu wa kawaida kabisa wa Bunge hili, kwamba Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni anaposimama kutaka

kuzungumza na Mnadhimu wa Kambi kwa mujibu wa Kanuni zetu ni kiungo muhimu kati Wabunge wa Upinzani na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, hapewi nafasi anachukuliwa kama Mbunge wa kawaida kabisa. Mheshimiwa Jenista Mhagama kila anaposimama na anapotaka kuingilia anapewa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kabisa naomba Mwongozo wako kwamba utaratibu huu unaruhusiwa katika Bunge hili na katika Mabunge ya Jumuiya ya Madola au huku ni kukiuka Kanuni za Bunge?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Gulamali Mwongozo wa mwisho.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuomba Mwongozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wangu kwa kutumia Kanuni hiyo ya 68(7) jambo lililotokea hivi karibuni, nataka kupata Mwongozo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI juu ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga kutokutoa ma-*file* (majalada) ya Kamati ya Fedha kwa Wabunge, kwa maana yangu Gulamali pamoja na Mheshimiwa Dalaly Kafumu na kusema kwamba haturuhusiwi kama Wabunge kuwa na mafaili ya Kamati ya Fedha kutoka katika Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri sasa atusaidie, je, huu ni utaratibu ambao umetolewa ama umeekezwa kwa Wakurugenzi kutokutoa mafaili ya Kamati za Fedha kwa Waheshimiwa Wabunge. Mwongozo wangu ni huo tu. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nadhani tunakoelekea itabidi tumwombe Mheshimiwa Spika atusaidie tufanye semina tena. Kwa sababu tunapokuwa kwenye Bunge kama hivi siyo muda wa semina.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Haonga kuhusu swali la Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzania Bungeni Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, maelezo yake yanasema wakati Waziri wa TAMISEMI Ofisi ya Rais, akijibu swali ameleza kwamba Mheshimiwa Mbowe kwa maelezo ya Mheshimiwa Haonga akae vizuri na Rais, Waheshimiwa Wabunge wote tulikuwepo hapa.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Simbachawene hajasema akae vizuri na Rais, amesema tuwe na mahusiano mazuri na Rais, amesema 'tuwe' hajasema 'awe'.

Pili, Mheshimiwa Spika alishatoa Mwongozo juu ya kuomba mwongozo kwenye swali lililoulizwa na Mbunge mwingine. Mheshimiwa Spika alisema hivi, "Yule ambaye hakuridhika ndiye anayepaswa kuuliza." Kwa hivyo, swali hili halikuulizwa na Mheshimiwa Haonga, Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni maana yake ameridhika. Kwa hiyo, mwongozo wangu ni huo Mheshimiwa Spika alishatoa mwongozo wa mwenye swali tena Mheshimiwa Haonga ndiye uliyepewa Mwongozo huo siku hiyo. Maana uliuliza mwongozo wakati swali liliulizwa na mtu mwingine, kwa hiyo ndiyo Mwongozo wangu aliyejibiwa ndiye aliyepaswa kufanya hilo jambo.

Mwongozo wa pili, nimeombwa na Mheshimiwa Kubenea ambaye ametoa maelezo kwamba anatomia Kanuni ya 47 na Kanuni ya 68(7) akatoa maelezo kuhusu Katiba kutambua Kanuni zetu, pia kwamba Kanuni ya 16 inatambua Wanadhimu wawili Bungeni kwa maana kwamba Mnadhimu wa upande wa Serikali na Mnadhimu wa Upinzani. Kwa maelezo yake anasema wakati Mnadhimu wa Upinzani akisimama kuwa hapewi nafasi ya kuzungumza lakini Mnadhimu wa upande wa Serikali anapewa nafasi ya kuzungumza.

Mheshimiwa Wabunge, hapa leo hatujaanza kuchangia, hakuna Mnadhimu aliyesimama kwa ajili ya jambo lolote akanyimwa nafasi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Kubenea Mwongozo wangu ni huo kwamba leo hii hakuna Mnadhimu aliyesimama akanyimwa nafasi. (*Makofi*)

Mwongozo mwingine nimeombwa na Mheshimiwa Seif Gulamali wakati akitoa maelezo yake anasema anaomba Mwongozo kutoka kwa Waziri akazungumzia kuhusu kunyimwa kwao ma-*file* yeye na Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, kwamba wamenyimwa ma-*file* ya fedha na Mkurugenzi wa Halmashauri.

Waheshimiwa Wabunge, nilisema jana narudia tena leo. Jambo hilo halijatokea hapa Bungeni. Hakuna yeyote aliyeomba *file* linalomhusu akanyimwa hapa Bungeni. Hiyo taarifa ya kunyimwa ma-*file* na Mkurugenzi, Mheshimiwa Waziri yuko hapo afuatwe akaulizwe. Hivyo, siyo suala tu la kupata nafasi ya kuzungumza, nimesema nilizungumza jana na narudia leo muda wa miongozo siyo muda wa kupotezeana muda Waheshimiwa Wabunge, tusipoteze muda wa Bunge, Mawaziri wako hapa, Waziri Mkuu yupo, ukiwa na swali ambalo halihusiani na Mwongozo mfuata yeye, kwa sababu siyo kazi ya Kiti kutoa maelekezo ambayo hayahusiki. Kwa hiyo kwenye jambo hili hakuna mwongozo wowote wa Kiti kwa sababu jambo hilo halijatokea Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo nimeletewa tangazo hapa kutoka kwa Kaimu Mkurugenzi Uhusiano wa Kimataifa na Itifaki, anasema Wenyeviti, Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliopewa taarifa kuhusu ile semina iliyoandaliwa na Bunge la Ulaya kwamba itafanyika leo tarehe 11 Mei, 2017 *New Dodoma Hotel*/kuanzia saa saba mchana. Usafiri wa kuwapeleka Waheshimiwa Wabunge *New Dodoma Hotel*/utakuwepo mbele ya lango kuu la kuingia Ukumbi wa Bunge mara baada ya kusitishwa kikao hiki cha Bunge. Waheshimiwa Wabunge tangazo hili linawahusu Wenyeviti, Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge na baadhi ya Waheshimiwa waliotaarifiwa. Kama haupo kwenye hiyo orodha basi usafiri hata hivyo utakuwa hautoshelezi watu wote.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo sasa tutaendelea. Katibu.

NDG. CHARLES MLOKA- KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Wizari ya Maji na Umwagiliaji

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na majadiliano ya Hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji. Nimeshaletewa orodha ya wachangiaji kutoka vyama vyote na tutaanza na Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo yeye alikuwa ametajwa tangu jana, atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah na Mheshimiwa Ester Bulaya ajiandae.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunikumbuka na kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kutokana na ufinyu wa muda nianze kwa kusema kwanza kabisa naunga mkono hoja. Pili, nitoe mapendekezo yangu juu ya masuala ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti yetu ya maji imepungua sana, licha ya kupungua na hata ile bajeti ambayo imekwenda ni asilimia 19 tu, na mimi naungana na wale wote wanaosema tuongeze kwenye tozo ya mafuta ili tuweze kupata fedha zaidi ili tupate maji zaidi kwa ajili ya vijiji vyetu huko Majimboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba sana Serikali tutakapokubaliana kwamba tunaongeza tozo kwenye mafuta angalau kwa shilingi 50/= kwa lita basi mgawanyo wa fedha hizi uende sawa, isionekane tu kwamba upande fulani wa nchi ama upande fulani wa Majimbo ndio unapata fedha nyingi zaidi kuliko mwingine, kwa sababu tutakaolipia fedha kwenye mafuta ni Watanzania wote. Kwa hiyo, tupate

kwa usawa, miradi yote ya maji igawiwe fedha kwa usawa.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais katika masuala ya maji anataka kumtua ndoo Mama wa Kitanzania na kasi ya Mheshimiwa Rais wako ambao hawajui na wasiojua kasi Mheshimiwa Rais juu ya kumtua mama ndoo ni Wahandisi wa Maji walioko kwenye Halmashauri zetu, vilevile watu wa Idara ya Manunuzi wakiongozwa na Idara ya Manunuzi ya Halmashauri ya Mji wa Njombe pamoja na Mhandisi wa Idara ya Maji Njombe, hawana habari kabisa kwamba Mheshimiwa Rais anataka kumtua ndoo mama wa Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maji ya Njombe haiendi, haiendi kwa sababu hawa watu wawili yaani Idara ya Manunuzi na Idara ya Maji hawana habari kabisa kama kuna kumtua mama wa Kitanzania ndoo ya maji kichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana kwa kuwa, Idara hizi mbili Idara Manunuzi na Idara ya Uhandisi zipo chini ya TAMISEMI, TAMISEMI waziangalie Idara hizi ili kusudi waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji kaka yangu Mheshimiwa Lwenge ni Injini na kaka yangu Mheshimiwa Kamwelwe pia ni Injini. Kadri tunavyofahamu teknolojia ya maji ilivyo rahisi haikupaswa sisi tukose maji, tunakosa maji kwa sababu ya uzembe wa wahandisi walioko kwenye Idara ya Maji huko kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji Njombe pamoja na Idara ya Manunuzi wanafanya manunuzi mwaka nzima, wanahangaika kufanya manunuzi, sielewi wananunua kitu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo miradi ya maji ya Igongwe imeshindikana kutekelezwa ndani ya Halmashauri ya Mji Njombe kwa sababu tu kwamba Idara ile ya Manunuzi imesimamia utaratibu wa manunuzi mwaka mzima, mpaka

leo naongea hivi bado mkandarasi hajakabidhiwa mradi, bado anahangaika na taratibu za manunuzi. Mara sijui tusaini hiki, mara tusaini hiki.

Ninaomba sana kwa kuwa ndugu yangu Mheshimiwa Simbachawene wanaokufahamu sasa wanakujua wewe ni Mwanasheria, lakini mimi ninayekufahamu zaidi najua wewe ni fundi, tulisoma chuo kimoja. Walioko kule wanahitajika *Technician* ili wafanya ile kazi, *Engineer* ni mtu ambaye kwa kweli hana uwezo kabisa wa kushughulika na maji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana tuweke vijana ambao wana moyo wa kushughulikia matatizo ya wananchi na wana uwezo mkubwa. Injiniya kwanza anajisikia, kwenda kwenye mabonde yale ya maji na uinjiniya wake anaweza kuona ni matatizo.

Kwa hiyo, ninaomba sana kwamba tuweke *technician*, vijana wadogo ambao wako tayari kuhakikisha kwamba maji yanapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi ya maji kule Njombe tuna shida sana ya miradi miwili ya maji, Mradi wa Lugenge na Mradi wa Ngalanga. Miradi hii imeathirika vibaya sana. Serikali imetoa fedha ndiyo, hata kama imetoa kwa kuchelewa lakini jinsi miradi inavyotekelezwa inatia huruma, mradi wa Lugenge ulikuwa ni mradi wa mwaka 2012 na ulikuwa ni mradi wa miezi tisa, leo hii ni miaka mitano mradi haujakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiutembelea mradi unatia huruma, wananchi wale wanasikitika sana, mabomba yameachwa porini, mitaro imechimbwa na maji zaidi ya pale walipochimba. *Intake* zimejengwa hazijakamilika, Mhandisi yupo Mhandisi Mwelekezi yupo, Mhandisi wa Mkoa yupo, watu wote hao lakini mradi hauendi. (*Makofi*)

Ukiuliza Wizarani Mheshimiwa Waziri anasema fedha ipo walete *certificate*. Mkandarasi anatengeneza *certificate* anampelekea Mhandisi, Mhandisi anatoa *copy certificate* analeta ile *copy* wizarani, nani atalipa kwa malipo ya *copy*? Kwa hiyo, huu ni uzembe wa dhahiri kabisa na uzembe wa makusudi, wanasababisha wananchi wakose huduma bila sababu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe Wizara ya Maji mtusaidie hasa huu mradi wa Lugenge, naomba mje muukague na mtusaidie kwa sababu huu mradi umeshapitisha miaka mitano. Leo hii mkisema bei ya mradi huu utekelezwe kwa gharama zilezile haiwezekani, hata kama utaratibu hauruhusu, lakini vifaa vilivyokuwa vinanunuliwa miaka mitano iliyopita vikinunuliwa leo bei zimebadilika. Niwaombe sana Wizara ya Maji mtusaidie, mje muangalie mradi wa Lugenge ili kusudi tuweze kuurekebisha, kwasababu wananchi wale wanashindwa kuielewa Serikali, na tumekuwa tukiwashawishi mara zote kwamba maji yenu mtapata. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, walishatengenezewa mabomba mitaani, mabomba hayana hata maji lakini intake hazijajengwa na mabomba hayajalazwa ya kukamilika. Kwa hiyo niombe sana Wizara sasa itusaidie, ituletee mtaalam aje afanye ukaguzi na atoe ushauri tufanye nini na mradi huu kwa sababu sasa hivi tunaona hata mkandarasi naye anasua sua.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mradi wa Ngalanga nao unaonekana kama umekosewa kufanyiwa *designing* kwa sababu wenyeji wanasema chanzo hakina maji kabisa na wanashangaa mabomba yanalazwa watapeleka nini? Kwa hiyo niombe sana miradi hii miwili ya Njombe ikaguliwe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya LAAC, katika Kamati yetu tulitembelea baadhi ya miradi ya umwagiliaji, kwa kweli inasikitisha. Unakwenda pale Halmashauri ya Lindi kuna mradi unaitwa Ngongo mpaka

CAGamesema mradi unakosa umeme. Tumetembelea mradi hakuna dalili ya mradi kuanza leo wala kesho, ni pori. Sasa unajuliza mpaka CAG anasema bado umeme halafu kuna pori hakuna maji, hawajalima wala nini lakini unaambiwa bado tu umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mradi wa maji tulitembelea pale Tabora nao ni hivyo hivyo, bwawa limekauka, fedha nyingi imetumika. Kwa hiyo, niombe sana kama kuna uwezekano kwenye miradi ya umwagiliaji nchi hii, kama tunaamini itatuokoa basi hiyo idara ya umwagiliaji huko wizarani ifanyiwe maboresho kwa sababu *designing* zao zimeonyesha kwamba miradi ile haina tija kabisa wala haifanyi kazi na wala haielekei kwamba inaweza kufanya kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, gharama za maji. Yuko mjumbe hapa jana ameongea kwamba hivi haya maji ni huduma au ni biashara? Ni kweli watumia maji wanapaswa kulipia gharama za maji lakini gharama zenyewe angalau ziwe zinaendana. Mji wa Njombe gharama ya maji ni juu sana, *unit* moja ya maji Njombe ni shilingi 855, na katika hiyo bei unalipa tena na *service charge* ya shilingi 2,000. Lakini maji tunayopata katika Mji wa Njombe ni maji ya mtiririko, mitaro ile tulichimba sisi wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu Njombe maji yetu yale pamoja na kwamba ni ya mtiririko hayana mtambo wa kuyasafisha wala nini, yanavyotiririka huko toka Mungu alivyoyaumba basi mpaka ndani ya nyumba zetu. Sasa gharama hii inavyokuwa kubwa namna hii wananchi wa Njombe wanalalamika na kusema kwamba hii inakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyofika aliambiwa jambo hili lakini akatoa maelekezo. Kwa hiyo, naomba tena idara ya maji, lifuatilie jambo hili. Ni kweli EWURA walikuja lakini je, unampambanisha EWURA na mwananchi wa kawaida? EWURA wale ni wataalam, mwananchi wa kawaida anaelewa nini? Haiwezekani kabisa kama anataka kulinda haki za wananchi wetu

tuwapambanisha eti *EWURA* kwa sababu *EWURA* wanakaa wanaongea na mlaji. Mlaji anamsikiliza mtaalam wa idara ya maji anachosema, mtaalam wa Idara ya Maji ameshapiga hesabu zake pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo haiwezekani upandishe bei ya maji kutoka *unit* moja kutoka shilingi 395 mpaka shilingi 855 kwa mara moja? Una sababu gani na unakimbilia wapi? Umebanwa na nini cha pekee mpaka uamue kupandisha maji kwa gharama kubwa namna hii? Haiwezekani kwa sababu kama ninavyosema maji ya Mji wa Njombe ni maji ya mtiririko na gharama yake sehemu kubwa tulifanya wenyewe wananchi kwa kuchimba mitaro na wenyewe Idara ya Maji wamekuja wamekuta ule mradi upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana na kama haiwezekani kupunguza maji basi Mamlaka ya Maji ya Mji wa Njombe iondolewe, Idara ya Maji irudishwe Halmashauri kusudi ishughulikiwe na Halmashauri kusudi ishughulikiwe na isimamiwe na Halmashauri. Tunaamini kwamba gharama za maji zitapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoiendea miradi hii ya maji niendeleo kusisitiza kwamba tuombe sana mhandisi, idara ya maji ya Halmashauri ya Mji wa Njombe ije iangaliwe upya kwa maana ya wataalam wake na ikiwezekana...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagongwa.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, asante sana. *(Makofi)*

MHE. MUNDE A. TAMBWE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia Wizara hii nyeti, Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa mimi binafsi nianze kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, niwashukuru Mawaziri wote, lakini hususan Waziri wa Maji. Sisi kwa Mkoa wa Tabora kwa kweli tunawashukuru sana. Mheshimiwa Rais alivyokuja Tabora kwenye kampeni alituhidi atatuwekea maji ya Ziwa Victoria. Lakini mpaka ninavyosema hivi tumeshazindua na mkataba umeshafanyika wa maji Ziwa Victoria na maji haya yataenda karibia eneo kubwa sana la Mkoa wa Tabora. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali, tunaishukuru Wizara na nimeongea na Mheshimiwa Waziri amesema muda mfupi watakuja kufanya uzinduzi Tabora tayari kwa kuanza kujengwa kwa mradi huu mkubwa ambao utamtua mwanamke ndoo ya maji kwa asilimia 90. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile niishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kutuletea mradi mkubwa wa *JICA* wa bilioni 29. Mradi huu umetusaidia Mkoa mzima, niweke tu sawa tu *Hansard* siwezi ku-*attack* Mbunge mwenzangu. Jana Mheshimiwa Sakaya alisema mradi huu umegusa Wilaya moja ya Uyui, si kweli; mradi huu umegusa Mkoa mzima wa Tabora. Mradi huu Wilaya ya Tabora Manispaa umeenda Kakolo kwa maana ya bomba, umeenda Mabama - Uyui, Kizengi - Uyui, Nzega kwa maana ya mabomba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mradi huu umechimba visima 101 Kaliua kwake Mheshimiwa Magdalena Sakaya visima vipo, Urambo, Sikonge na Mkoa mzima wa Tabora. Kwa hiyo, niweke *Hansard* sawa Mradi wa *JICA* umepita Mkoa mzima wa Tabora na si tu Wilaya moja kama ilivyosemwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hayo machache naendelea kuipongeza Serikali, lakini changamoto hazikosi. Tunaiomba Serikali sasa wakati ikituletea maji ndani ya Tabora Manispaa maji haya sasa yatoke Tabora Manispaa kwenda Sikonge awamu ya pili. Vilevile hatukuwa na mpango wa kuyatoa maji haya ya Ziwa *Victoria* Tabora kuyapeleka Urambo, mimi nadhani tuweke

mpango huu wa kupeleka Urambo. Najua Urambo kuna mkakati mkubwa wa Malagarasi kwa kupitia Kaliua na kwenda Urambo. Hata hivyo Mheshimiwa Waziri hili jambo ni kubwa, Malagarasi ipo mbali sana na Urambo na Kaliua, litachukua muda mrefu. Nikuombe Mheshimiwa Waziri kwenye mipango yako uweke maji ya Ziwa Victoria yaende Urambo, ni kilometa 90 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama mtayapeleka Igalula baadaye mkija kuyapeleka Urambo nadhani ni rahisi zaidi kuliko kupigana na Malagarasi kwa sasa. Ila mradi wa Malagarasi uendelee kama mlivyokuwa mmeupanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine kubwa ambayo tunayo watu wa Tabora Manispaa ni *water table* ambayo iko juu. Serikali imetuletea maji mengi sasa, kwa hiyo niwaombe Serikali itupatie pesa tulizomba shilingi bilioni 14 kwa ajili ya mabomba ya maji taka. Tumeomba shilingi bilioni 14 tupatie mabomba ya maji taka ili tuweze kupitisha maji taka, maji yasiwe mengi ili kuepuka magonjwa ya milipuko yatakatayokuja baada ya kupata hayo maji mengi ya Ziwa Victoria.

Sasa hivi tuna mtandao wa mabomba ya maji taka kwenye kata mbili tu Ngongoni na Bachu Kidogo, huko kote hakuna mtandao wa maji taka. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itupatie mtandao wa maji taka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni madeni, Idara ya Maji inadai madeni makubwa sana. juzi nikiwa Tabora tarehe 28 mpaka tarehe 3 tulikatiwa maji, nikaenda Mamlaka ya Maji kuuliza tatizo ni nini? Wakaniambia tumekatiwa umeme tunadaiwa shilingi milioni 500 za umeme na *TANESCO*. Lakini *TUWASA* Tabora inadai shilingi bilioni tatu; ambapo Jeshi linadaiwa shilingi bilioni mbili, Kitete Hospitali ya Mkoa na inadai Polisi na Magereza hawawalipi pesa zao. Sasa hii taasisi itaendeshwaje kama taasisi hii ya *TUWASA* tu Tabora inadai shilingi bilioni tatu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali ije na mpango mkakati mwingine. Mimi nimefanya kazi Halmashauri, tulikuwa tunakatwa *LAPF* na nini, lakini hela haziendi sehemu husika. Serikali ikaamua madeni yote yale yatoke Hazina moja kwa moja yapelekwe sehemu husika. Kwa hiyo, mimi naomba Serikali yangu iamue sasa madeni yote ya hizi Mamlaka za Maji, ya Jeshi na nini bajeti zao za maji zikatwe moja kwa moja na Hazina zipelekwe zikalipe maji ili na wananchi wengine waweze kufaidika na haya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumekatiwa maji Tabora nzima kwa sababu tu kuna taasisi za Serikali zinagaiwa. *TANESCO* wakakata umeme wao, kwa hiyo, sisi watu wa Tabora wote tukakosa maji kwa sababu watu wanadaiwa madeni makubwa ambao ni Taasisi za Serikali. Naomba Serikali ije na mpango mkakati *otherwise* watu watakosa maji wakati Serikali imeshayaleta maji mpaka sehemu husika. Nawaombeni sana Serikali mliangalie hili suala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naenda moja kwa moja kwenye bajeti. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuhusu suala suala la tozo na mimi naiomba Serikali yangu iongeze shilingi 50 kwenye Mfuko wa Maji ili kupata shilingi 100. Lakini napingana na watu wanaosema kwamba tukatae bajeti au tuibadilishe bajeti kwa sababu ukiangalia Kanuni ya 105 kwa kuokoa muda sitaisoma inasema kwamba sisi Wabunge kwa ushauri wetu Kamati hii inaweza ikarudi kwenye *Budget Committee*, ikakaa upya na ikaangalia taratibu je, hizi tozo tukiongeza kuna tatizo gani? Kama kuna tatizo basi labda tupunguze *REA* au tupunguze kwenye Mfuko wa Barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuwape muda Serikali wakakae kwenye *Budget Committee* wafanye hii kazi, lakini tukisema humu ndani tunaikataa bajeti hakuna tutakachokuwa tumekifanya ndugu zangu. Tusikubali kabisa kukataa bajeti, kanuni inatuelekeza kwamba tuna uwezo wa kuirudisha Serikali ikakaa tena upya na wakaja kwenye

Kamati ya Bajeti wakati wa hotuba ya bajeti wakatuletea wameonaje na wamefikiriaje. Nawaomba sana ndugu zangu bajeti hii isirudishwe, isipokuwa warudi kwenye *Budget Committee* wakakae upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu naomba niongelee kidogo, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *PAC*, nilipata bahati ya kwenda kukagua *DAWASCO* Dar es salaam. Nilikuta vitu vya ajabu kweli na vikashangaza na nikaona kweli Serikali yangu sasa iko kazini na inafanya kazi na inadhibiti hizi taasisi za Serikali. Wakati tumekwenda tumesomewa ile taarifa wakati huyu *CEO* aliyepo sasa hivi anaingia alikuta *DAWASCO* haina chochote hata senti tano, lakini alikuta deni la shilingi bilioni 28 la *PPF*, shilingi bilioni 16 la *TRA*, watumishi shilingi bilioni tano na alikuta upotevu wa maji asilimia 56 lakini alijitahidi kufanya kazi mpaka sasa hawadaiwi hata senti tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, fikiria hii ni mwaka 2017 ameingia mwaka 2015 mwishoni, hakuna deni hata moja; tunajuliza kipindi kile hizi hela zilikuwa zinakwenda wapi mpaka madeni yakawa makubwa kiasi hiki? Kwa hiyo, naamini kabisa Mheshimiwa Waziri wa Maji hii kazi unaifanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Waziri nilikuwa na ushauri mmoja; *DAWASCO* inakusanya shilingi bilioni tisa kwa mwezi lakini inatoa asilimia 23 sawa na bilioni mbili inapeleka *DUWASA*.

Sasa mimi najjuliza hizi bilioni mbili *DUWASA* za nini? Wakasema sijui kwa sababu maji yanalipiwa umeme na umeme unalipwa na *DAWASCO*, *service* ya mitambo inafanywa na *DAWASCO*, lakini *DUWASA* ina watumishi 68 na hawa watumishi 68 wanapelekewa shilingi bilioni mbili kila mwezi, kwanini *DUWASA* na *DAWASCO* visiunganishwe kama tulivyofanya *TRL* na *RAHCO*? *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Tambwe muda wako umekwisha.

MHE. MUNDE A. TAMBWE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nilikuwa nimemuita MMheshimiwa Esther Bulaya atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi na Mheshimiwa Andrew Chenge ajiandae.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa niwapongeze Wabunge wa Afrika Mashariki wanawake waliochaguliwa jana, na bila kujali itikadi zetu tukiungana katika mambo ya msingi, tutakuwa tunaitendea haki nchi yetu. Pili, nipongeze kabisa jitihada zinazofanywa na Jiji la Dar es Salaam kwa kudhibiti huo wizi ambao umesemwa na aliyenitangulia chini ya UKAWA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kama ambavyo tumeungana jana na kuweka historia ya kuwapeleka Wabunge wanawake wengi kwenye Bunge la Afrika Mashariki, ninaamini tutaungana tena kuibana Serikali kuhakikisha tunaitendea haki bajeti hii ya maji ambayo ukizungumzia watu ambao wanaumia katika suala zima la kutafuta maji ni mwanamke. Ninaamini tutaacha itikadi zetu pembeni ili tulitendee haki Taifa letu na tuwatendee haki wanawake wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina sababu kubwa za kusema hivi. Waheshimiwa Wabunge mwaka jana zilitengwa shilingi bilioni 937 fedha za maendeleo ni shilingi bilioni 915, zilizotoka ni asilimia 19 tu ya zaidi ya shilingi bilioni 900. Sasa tujjulize tupo kwenye kipindi hiki ambacho leo hii Waziri na Naibu wake shemeji yangu wanaomba tupitishie hapa bajeti. Hiyo asilimia 81 mtaleta lini kuwatendee haki watanania na wanawake wa Taifa hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaposema tunaikataa bajeti naunga mkono hoja ya Kambi Rasmi ya

Upinzani si kwamba tunawachukia, si kwamba hatutaki maji, no, tunaitaka Serikali na tunamtaka Waziri wa Fedha aende afanye anavyofanya mkae mjipange upya mjue sasa mtakapopata fedha mtuletee ili sasa sisi wanawake na wanaume wote na Waheshimiwa Wabunge wote ndio tuungane kuipitisha bajeti yenu. Haiwezekani tunasema tuna mkakati wa kuhakikisha tunamtua mwanamke ndoo ya maji kichwani mijini na vijijini, halafu mpaka leo zaidi ya asilimia 81 haijaenda kwenye Wizara ya Maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilishasema nitasema ukweli, fitina kwangu mwiko. Nakupenda shemeji yangu na nakupenda mzee wa *site*, katika hili kwa sababu ninawapenda ninahitaji asilimia 81 mpate Serikali iende ikakae, ikatafute pesa iwape. Kuunga mkono hapa siwezi nikawapaka mafuta kwa mgongo wa chupa, hiyo si desturi yangu mimi. Si desturi yangu na kama mama, kama mwanamke na kama Mbunge wa Jimbo ambaye Jimboni kwangu..., nimesoma kitabu chako umeweka, umetenga hela. Mwaka jana ulitenga na miaka kumi iliyopita huo mradi ulikuwepo yaani leo wana Bunda kama ni *birthday*ni *birthday* ya kuanzishwa mradi wa maji kwa miaka kumi bila kupata maji safi na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa biashara ya kutenga pesa ambazo hazifiki na kila siku nimekuwa nikisema mkandarasi huyo ni mwizi, amekataliwa Kigoma na Rorya. Mimi nilisema simtaki alienitangulia akawa ananibishia, wananchi wa Bunda wakasema *mwana Bulaya jaga*, nimekuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, wizi sitaki jimboni kwangu; wizi jimboni kwangu sitaki, silindi wezi, ninachotaka mimi ni maslahi ya wananchi wangu kwanza.

Mheshimiwa Waziri huyo mkandarasi ana madeni mengi, mkiweka hela kidogo badala ya kwenda kufanya shughuli za kukamilisha ule mradi wa maji ambao sasa hivi una miaka kumi haukamiliki, halafu mimi leo nije hapa hata kama nakupenda kiasi gani siwezi kukubali kuja kuunga

mkono wakati wananchi wangu wanaona tu mwaka wa kumi sasa hivi mradi wa maji haujakamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri yetu ni changa lakini Mamlaka ya Maji Bunda ni *class c*, inapaswa kupata ruzuku Serikalini na ndiyo maana wanashindwa kulipa bili ya maji kwa sababu hampeleki fedha kwa mujibu wa taratibu anahitaji kupata ruzuku. Kwa sababu kuna neno kata, wanakata! Nilimuomba kaka yangu nashukuru umenisaidia na baba yangu Muhongo. Neno kata linatumiwa vibaya. Mnashindwa kupeleka fedha wakisikia kata wanakata bila kujua wanaathiri mamia ya wanawake na maelfu ya watanzania kwa kukosa huduma ya maji hicho kidogo ambacho kinapatikana, *please!* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine nadhani kwenye Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani mmeambiwa kuna miradi hewa, nendeni mkaishughulikie kule, mkichelewa mimi nitawaumbua. Nilishasema kule kwa kaka yangu Mheshimiwa Bonny, mradi ule wa Mgeta – Nyangalanga amepewa mtoto wa mpigakura wangu *senior*, kala milioni 800 haujakamilika wakawa wanalazimisha apokelewe kinguvu, Makalla alikataa wakataka kumtumia *DC* nikamwambia wewe utaondoka wewe mradi hautapokelewa, haukupokelewa. Shughulikieni hawa wezi, msipowashughulikia nitawaumbua hapa, sicheki na mtu mimi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wizi Jimboni kwangu sitaki. Mradi wa Mgeta, shughulikieni. Wizi, *conflict of interest*, unatoa *tender* kwa mtoto wako, hana vigezo, kakataliwa maeneo kibao mpaka Mtwara kule, ondoeni wizi, nimesafisha mtu sitaki na mtoto wake, nataka mambo yangu yaende vizuri ili wananchi wangu wapate maendeleo kupitia binti yao, Ester ngw'ana Bulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, naomba sana Mheshimiwa Waziri, mzee wa *site* na shemeji yangu wa Kantalamba, sana, mbali ya kwamba kuna hii miradi mingine imeanzishwa kama kule Rwabu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa Ester Bulaya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilimtaja Mheshimiwa Rashid Shangazi na atafuatiwa na Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa John John Mnyika ajiandae.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Baada ya sauti hiyo kutoka Bunda sasa ni sauti ya mahaba kutoka Tanga, mubashara kabisa kule ambako mahaba yamezaliwa. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi napongeza kwanza Mawaziri wa Wizara hii, ni Mawaziri wasikivu sana. Kwa kweli nafarijika hata Mheshimiwa Ester Bulaya amemuita ni mzee wa *site*, kweli huyu ni mzee wa *site*. Mheshimiwa Naibu Waziri hata anapojibu maswali yetu hapa ndani anajibu kwa *data* na kwa uhakika. Kwa hiyo, tunawapongeza sana pamoja na changamoto hii ya upungufu wa bajeti katika Wizara yao, niwaombe Waheshimiwa Wabunge tulijadili jambo hili kwa umakini mkubwa, tutafute namna ya kupata vyanzo vya kuwawezesha hawa majembe wakahakikishe kwamba ile dhana ya kumtua mama ndoo kichwani inakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri amefika katika Jimbo la Mlalo lakini pia Jimbo la Lushoto katika Halmashauri ya Lushoto. Ninaomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri amepata wokovu na jiko lake linatoka Mkoa wa Tanga. Kwa hiyo, huyu ni shemeji yetu na ndiyo maana hii kazi unaona anaifanya ni kwa sababu ana mtunzaji mzuri kule nyumbani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale katika Kata ya Manolo ule mradi wa vijiji 10 ulitoa ahadi kwamba ukamilike kabla ya Juni 30, nataka nikuhakikishe kwamba matenki yameshajengwa lakini bado hatua ya usambazaji wa

mabomba inasuasua. Hii ni sambamba na kule Lushoto katika mradi ule wa Ngulu, kata ya Kwemashai, nao unasuasua, mkandarasi bado hajaanza hatua ya usambazaji wa mabomba. Kwa hiyo, nikuombe shemeji yangu ujitahidi kabisa kwamba ahadi uliyoiweka ya Juni 30 kwamba miradi hii iwe imekamilika, ahadi hiyo uitekeleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunayo miradi mingi, ile miradi ya maji ya mwaka 1972. Tunao mradi wa kata ya Mng'aro, kata ya Mbaramo, kata ya Rangwi, kata ya Lukozi na kata ya Malindi. Hii miradi ni ya mwaka 1972 imeshakuwa ni miradi chakavu na watu wameongezeka sana katika maeneo haya. Vyanzo vya maji vimezidi kupungua hasa kutokana na mabadiliko haya ya tabianchi, kwa hiyo nikuombe Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwamba miradi hii twende tukaiboreshe. Tutakapoiboresha katika hatua hizi za awali itatusaidia kwamba hatutakuwa na gharama kubwa ya kuandaa tena miradi mikubwa ya vijiji kumi kumi. Kwa hiyo, niombe sana kwa kuwa miradi hii haigharimu pesa nyingi sana ni vizuri tukaitekeleza wakati huu ambapo bado haijawa na mahitaji makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ni pamoja na mradi ule wa kata ya Mlola katika Jimbo la Lushoto, nao ule ni mradi wa siku nyingi, mkandarasi alikuwepo *site* muda mrefu, lakini haupigi hatua. Niwaombe tuchukue jitihada za makusudi ili dhana hii ya kumtua mama ndoo kichwani iweze kutimia kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala zima la umwagiliaji. Katika Hosea 4, aya ya sita, anazungumzia watu wangu wanateketea kwa kukosa maarifa na anasema wazi kwamba kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa nami nitakukataa.

Katika Halmashauri ya Lushoto na Wilaya ya Lushoto kwa ujumla na Milima ya Usambara tunatiririsha maji mengi sana ambayo yanapotea tu na kuelekea baharini. Hata sasa tunavyozungumza tuna wimbi kubwa la mafuriko katika Mji wa Korogwe eneo la Mkumbara, lakini maji haya yote

yanatoka katika Milima ya Usambara. Yapo makorongo mengi yanayoshusha maji na maji haya yanapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe Wizara, hatuwezi tukawa na kilimo endelevu bila kuwa na skimu za kilimo. Nimeona hapa katika ukurasa wa 87 mmetaja baadhi ya skimu za kilimo kwa ajili ya kilimo cha mpunga, lakini kule kwangu kuna skimu ile ya Mnazi ambayo tumezungumza sana Mheshimiwa Waziri, ambayo pia inakwenda kusaidia na kata jirani za majimbo ya Same Mashariki na Same Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nikuombe sana kwa pale Mnazi ambapo tulikusudia tujenge mabwawa kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji. Vilevile ukumbuke katika Wilaya ya Lushoto hili ndilo eneo pekee ambalo lina wafugaji, wenzetu hawa Wamasai. Kwa hiyo, tulikubaliana kabisa kwamba eneo hili tupate bwawa kwa ajili ya kutunza maji kwa ajili ya shughuli za kilimo, lakini pia maji haya yasaidie kunywesha mifugo, kwa sababu katika kata tatu za Jimbo la Lushoto ambazo ni tambarare ni pamoja na eneo hili ambalo ninalizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunakusudia kwamba yatakapopatikana mabwawa katika eneo hili yatasaidia kutatua pia tatizo la wafugaji kuingiza mifugo katika Hifadhi ya Mkomazi na ndiyo maana nasema watu wangu wanateketea kwa sababu ya kukosa maarifa. Kwa hiyo sasa sisi tutumie maarifa haya ili kutatua kero hizi za wafugaji kuingiza mifugo katika hifadhi, lakini tutatue kero hizi za kuacha maji yakiwa yanapotea bila kuwa na matumizi yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba nipendekeze eneo ambalo Wizara hii inaweza ikapata fedha, wenzangu wengi wamezungumzia kuongeza tozo katika tozo ile ya mafuta, mimi naunga mkono sina tatizo na hilo, lakini hivyo bado kuna eneo la simu. Mitandao ya simu hii wakati mwingine inatumika vibaya nadhani kwa sababu labda hatujasimamia hili eneo vizuri. Ni eneo ambalo na lenyewe

tunaweza tukaja na wazo zuri tukapata tozo kiasi kutoka kwenye mitandao ya simu ili likaweze kutunisha mfuko wetu huu wa maji vijijini. Kwa hiyo niombe sana Wizara ya Fedha ijaribu kuliangalia hili tuone namna gani tunaweza tukapata chochote katika mifuko hii ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Udhhibiti wa Maji na Nishati (*EWURA*) huwa wanachukua asilimia katika Mamlaka za Maji lakini pia wanachukua asilimia tatu nadhani katika bili za *TANESCO*. Pesa hizi zingewekewa ukomo kwamba labda asilimia 40 ya pesa hizo wanazozikusanya kutoka mamlaka za maji na kwenye madini pamoja na *TANESCO* angalau asilimia 40 iingie katika mfuko huu wa maji ili kwenda kutunisha mfuko wa maji na kumtua mama ndoo kichwani kama ambavyo ilani inatuelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la maji ni suala ambalo kwa kweli ni jambo kubwa sana ambalo ni ahadi ya ilani na wote hapa hakuna Mbunge ambaye hajaahidi. Kwa hiyo ninaiomba sana Wizara izingatie hilo. Ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia 100. Ahsante sana, nashukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kabla Mheshimiwa Andrew Chenge hajasimama wapo wageni ambao nimeletewa ujumbe sasa na hawa ni wageni wa Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI na hawa ni Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji vya Wilaya ya Tarime. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Simbachawene. (*Makofi*)

Mheshimiwa Andrew Chenge, atafuatiwa na Mheshimiwa John John Mnyika, Mheshimiwa Dunstan Kitandula ajiandae.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii nami niweze kuchangia kwenye hoja hii. Nitamke naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Naibu wake na timu yake kwa kuandaa hotuba nzuri, ina taarifa nyingi za manufaa kwa maendeleo ya nchi yetu. Mnyonge mnyongeni lakini haki tuwape. Hii Wizara inajitahidi sana Waheshimiwa, kwa nchi nzima tunaona sura hiyo lakini ni kwa saabu ya rasilimali fedha ambalo ndilo linalotusumbua wengi hapa, lakini tunawapongeza wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mkoa wa Simiyu, naendelea kuishukuru Serikali kupitia hotuba hii kwa mradi mkubwa ambao ni wa kihistoria kwa Mkoa wa Simiyu kutoka Ziwa Victoria ambao utahusisha Wilaya zote tano za mkoa huo. Lakini nitakuwa mchoyo sana wa fadhila nisipotambua kazi kubwa iliyofanywa na Rais mstaafu Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete, maana yeye tangu mwaka 2005 alipoingia madarakani ndio amehangaika sana na mradi huu kwa kutambua hali halisi ya ukame katika Mkoa wa Simiyu. Mimi naamini mbele ya safari mradi huu utakapokamilika hata katika awamu ya kwanza wamkumbuke angalau awepo katika uzinduzi wa mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nirudie tena kumshukuru sana Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli, juzi alipokuwa Bariadi aliusemea mradi huu kwa nguvu na akamaliza kabisa akakata mzizi wa fitna kuhusiana na mradi huu ambao ulikuwa umeanza kuoneshwa kuhusu wapi matenki ya maji yakae na alisema bila kumung'unya maneno mradi huu utatekelezwa na matenki ya maji yatakaa palepale kwenye Mlima wa Ngasamo, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji, mimi ningependa tu Waziri labda kesho anapohitimisha anithibitishie, kwa sababu mradi huu umesanifiwa kwa kutambua hali halisi ya mkoa huo, kwamba yatakuwepo mabomba makubwa mawili, bomba moja la maji ambayo hayakutiwa dawa (*raw water*) na bomba lingine ndiyo la maji safi ambayo ndiyo yatatumika kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lile la maji ambayo hayakusafishwa, hayakutiwa dawa ni kusaidia kurejesha hali ya uoto wa asili katika maeneo hayo lakini pia kwa mifugo; na ndiyo maana hoja kubwa ya mradi huu ilikuwa ni kuangalia hali nzima ya mkoa huo ili mifugo hii isiende maeneo mengine kwenda kuharibu mazingira. Kwa hiyo ningependa hiyo *confirmation* tui pate, kwamba bado dhana ni ile ile katika usanifu wa mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali, nimeona pesa ambazo zimetengwa kwa Mji wa Bariadi ambao ni makao makuu ya Mkoa wa Simiyu. Mahitaji ya maji ni makubwa, idadi ya watu inazidi kuongezeka Bariadi na viunga vyake, tunahitaji hizo pampu tano kwa sababu visima vile vitano vimechimbwa mwaka juzi na viko pale. Sasa tungependa tupate umeme, ziunganishwe, tuongeze uzalishaji wa maji na tusambaze kwa matumizi ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye Jedwali Namba 5A, pesa ambayo imetengwa kwa kutekeleza miradi ya maji vijijini. Nina vijiji vitatu ambavyo tumepata maji tangu mwaka 2012; vijiji hivyo ni Igegu, Masewa na Sengerema katika kata ya Dutwa, kata ya Sapiwi na kata ya Masewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wananchi hawa wanajua kuna maji, wanafahamu, waliyaona wakati wanachimba visima hivi, ningependa sasa zile pesa ambazo nimeziona angalau zikatumika katika kusambaza mabomba ili maji yatoke chini yawafikie wananchi hawa kwa matumizi ya maendeleo yao. Naendelea kushukuru Serikali, nimepata maji ya msaada wa Serikali ya Misri, kisima kirefu pale Kololo lakini nazidi kuomba tena kwa Ngulyati, Mhango na Kasoli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu skimu ya umwagiliaji, nimeona ya Mwasubuya, lakini tuna eneo kubwa ambalo tunaamini Kasoli tukiweza kujenga bwawa kubwa tukafanya shughuli ya umwagiliaji sehemu kubwa ya eneo la Simiyu tutaweza kujitosheleza kabisa kwa mahitaji yetu ya chakula, kwa hiyo, naiomba Serikali ione hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije sasa mwisho, kwamba niliposema mnyonge mnyongeni. Waheshimiwa Wabunge na mimi nakubaliana na walionitangulia kwa kusema kwamba tutafute njia nzuri ya kuishauri Serikali ituongeze pesa katika Wizara hii na njia nzuri ni hii ambayo kesho Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja hii, tujaribu kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona nia njema ya Serikali, lakini tukifuata Kanuni zetu suala hili likarejeshwa kwenye Kamati ya Bajeti tuweze kufanya uchambuzi wa kina, njia ambayo naiona ya haraka ambayo hata kwenye ukurasa wa 13 wa hotuba hii mnaona, iliyonyanyua bajeti hii ni tozo ya shilingi 50. Asilimia 52.7 ya pesa ambazo zimefika zimetokana na tozo hii. Sasa hivi kwa wastani tunaingiza lita bilioni 1.8 za dizeli na lita bilioni 1.2 za petroli. Tukiangalia kwa suara hiyo uwezekano wa kupata fedha tukaongeza kwa asilimia 100 tena yaani shilingi 50 na tukipiga mahesabu tunaweza tukaongeza shilingi 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unafahamu maendeleo lazima tuyatolee jasho na ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge safari hii hii lugha ya kusema kwamba tutaongeza mfumuko wa bei, tulikatae kwa sababu sio hoja ya msingi. Hii inawezekana tukayafanya haya, mahitaji ya maji kwa watu wetu ni makubwa na tunaona, sasa tukiendelea namna hii hatutafika kokote, mimi ndiyo ushauri wangu na inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. *(Makofi)*

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze na hili suala la nyongeza ya fedha kwenye Bajeti ya Wizara ya Maji. Tunaweza tukakimbilia kufanya maamuzi, maamuzi ambayo yakawa na athari ya ongezeko la gharama za maisha kwa wananchi, kwa hiyo, badala ya kupunguza tatizo tukaongeza tatizo. Tatizo letu la msingi ambalo naliona katika

Serikali hii inayoongozwa na Chama Cha Mapinduzi ni vipaumbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kama Serikali inaamua kununua ndege (*Dreamliner*) kwa *quotation* ya watu wa *Boeing* wanasema dola milioni 224 ambayo ni takribani shilingi bilioni 400 Serikali haitaki kusema walichokubaliana hasa ni kiasi gani wanasema ni pungufu ya shilingi bilioni 400. Kama tunaweza tukatoa pesa kununua ndege shilingi bilioni 400 hivi ni nini kinatushinda kutoa shilingi bilioni 400 kuongeza kwenye bajeti ya Wizara ya Maji? Kwa hiyo, ndiyo maana nimeanza kwa kusema kwamba, tatizo letu kubwa ni kipaumbele. Serikali ya CCM kwa awamu zote pamoja na kuwa inatamka kuwa maji ni kupaumbele *number one* katika nchi hii, lakini kwenye bajeti kwa nyakati mbalimbali maji hayajawahi kufanywa kipaumbele *number one* katika nchi hii.

Katika mazingira ya namna hii ya Serikali ya CCM kupuuzwa kero ya msingi ya wananchi, mimi kwa maoni yangu kwa muda ambao nimekaa Bungeni nianze na hili la kwanza, ufumbuzi hauwezi kupatikana katika huu mjadala tulioanza jana unaohitimishwa kesho. Ufumbuzi kwa maoni yangu unapatikana kwa Watanzania kutambua kwamba kwa miaka mingi wamedanganywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ufumbuzi ni kuindoa Serikali ya CCM madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeyasema haya bila kusubiri Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha hotuba kesho. Kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu amekwishazungumza leo na Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiyo Kiongozi wa Serikali. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipojibu maswali, swali mojawapo liliulizwa asubuhi leo kuhusu maji, nilitarajia Mheshimiwa Waziri Mkuu kuelezwa namna ambavyo hii bajeti ya maji imepungua, yaani mwaka jana bajeti ya maendeleo ilikuwa bilioni 915, leo bajeti ya maendeleo ni shilingi bilioni 623 yaani tumepunguza bajeti kwa shilingi bilioni 292; nilitarajia Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Kiongozi wa shughuli za Serikali aliposimama hapa kujibu swali Bungeni angesema; kwa kweli nimesikia kilio cha Wabunge kuanzia jana na

nimesikia vilevile swali nililoulizwa leo na naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tutakaa tena katika Serikali, tutaongeza bajeti ya Wizara ya maji badala yake Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshatoa kauli hapa Bungeni leo kwamba Wabunge tuiptishe bajeti kama ilivyo. Kwa maneno mengine mheshimiwa Waziri huyu wa Maji hatarajiwi kuja na jipya lolote kama Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshatoa mwelekeo wa Serikali tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira ya namna hii Serikali hii ni vyema ikakiri tu kwamba imekwishashindwa kwenye suala la maji. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 aya ya 67 iliahidi kwamba ikifika mwaka 2010 asilimia 65 ya wananchi vijijini watakuwa na maji na asilimia 90 ya wananchi watakuwa na maji mijini.

Mheshimiwa Nasibu Spika, kwa maneno mengine, wale wananchi wenzangu walionituma Bungeni wa Kata ya Kibamba, iwe ni Kiluvya na maeneo mengine ya pembezoni Kibwegere na kadhalika kule Kwembe kule iwe ni Kisopwa, iwe ni Kwembe Kati katiza mpaka Kata ya Msigani, Malambamawili, nenda Mbezi kule maeneo ya pembeni, Mpiji Magohe, Goba sijui Kinzudi, Matosa maeneo yote haya ya Saranga, King'ong'o, Mavurunza yaani kwa ahadi hii ya Serikali; Serikali ya CCM iliahidi mwaka 2010 asilimia 90 wangepata maji, mwaka 2010 ikafika hawakupata maji, Serikali ikaahidi tena kwenye ilani nyingine ya CCM ya mwaka 2010/2015 kwamba ikifika mwaka 2015 asilimia 90 watapata maji, asilimia 65 watapata maji, ahadi nyingine ya uongo miaka 10 ikapita ikafika 2015, Serikali ikarudia tena ahadi ile ile ya kuahidi tena mwaka 2020 ndiyo matatizo haya yatatauliwa na Mheshimiwa Waziri ulijibu uongo Bungeni naomba tu utakapohitimisha ujibu ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipouliza swali Bunge hili, ukasema kwamba kwa sasa na hata katika kitabu chako umeonyesha tena kwamba kiwango cha maji kimeongezeka kutoka mita 300 mpaka 504 milioni na kwamba sasa kero kwa maneno yako mwenyewe umetumia maneno; "huduma ya maji imeimarika." Wakati unanijibu swali Bungeni ulisema

kuanzia sasa kilomita 12 huku, kilomita 12 huku kwenye barabara ya Morogoro, maeneo yote haya sasa yenye mabomba ya Mchina maji yatakuwa yanatoka. Ukaniahidi hapa Bungeni Mkutano huu huu ukasema maji yameshasukumwa tatizo ilikuwa ni umeme tu, maji yamesukumwa mpaka tanki pale Kibamba na sasa maji yatatoka, lakini Mheshimiwa Waziri ulisema maelezo ya uongo Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nasema, kwa haya majibu ya Serikali ambayo kimsingi Waheshimiwa Wabunge na hapa nitaomba nafasi kwa mujibu wa Kanuni ya 69(1) kabla ya kuingia kwenye hatua ya Kamati, kama Mheshimiwa Waziri hatatumia Kanuni ya 58(5) kuindoa hii hoja ili Serikali ilete *commitment* ya kurudisha zile shilingi bilioni 300 zilizoondolewa, kama Mheshimiwa Waziri hatatoa *commitment* hapa, Wizara ya Fedha haitasema ni kwa nini mpaka sasa imetoa asilimia 19.8 na wakati mpaka sasa ilipaswa pesa zitoke asilimia 75, kama hakutakuwa na *commitment* ni afadhali mjadala huu tuuhirishe kimsingi ili Serikali ikajipange upya ili bajeti hii ya maji iweze kuletwa ikiwa ina marekebisho ya msingi pesa za maji ziweze kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kuwa Serikali hii ni muendelezo tu wa kusema uongo Bungeni, ni muendelezo wa kutotekeleza ahadi, kama hamtayafanya haya ni wakati wa Watanzania kote nchini wenye kero kubwa ya maji, kero *number one* kujipanga kuindoa CCM madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatambua kwamba mnaogopa haya yasiende kusemwa kwenye majimbo yenu ndiyo maana mnazuia mikutano ya vyama vya siasa. Lakini nawaambia mtatuzuia humu Bungeni, mtatuzuia majimboni, mtatuzuia maeneo mbalimbali lakini Watanzania wanauelewa ukweli wa kudanganywa na Ilani za CCM za toka miaka niliyoitaja. Bila kero ya msingi ya maji kuondolewa watachukua hatua mwaka 2019/2020.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge nilimtaja Mheshimiwa Dunstan Kitandula, kabla hajasimama kuchangia nimepewa tena ujumbe, inavyoonekana wageni leo wanakuja kwa makundi.

Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii na hawa wanatoka *Goodall foundation* ni Ndugu Andrew Goodall na Sylvia Goodall na wameambatana na watu wengine ambao wao ni Watanzania, karibuni sana.

Mheshimiwa Dunstan Kitandula atafuatiwa na Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, Mheshimiwa Moshi Kakoso ajiandae.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba iliyoko mbele yatu. Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kusimama mbele ya Bunge letu Tukufu na kuweza kuwasilisha mawazo ya watu wa Mkinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii vilevile kuwapa pole ndugu zangu wa Mkinga kwa maafa makubwa waliyoyapata kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika Jimbo letu la Mkinga na kwa Mkoa wa Tanga kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za Kituo cha Utafiti cha Mlingano zinasema mvua zinazoendelea kunyesha sasa zimefikia milimita 316 katika *span* ya siku tatu. Kiwango hiki ni kikubwa sana, mvua hizi hazijawahi kuoneka kunyesha kwa miaka 40 iliyopita. Kwa hiyo, tunapozungumzia madhara yaliyotokana na mvua hii tunaiomba Seriakli ilichukulie jambo hili kwa umakini mkubwa. Hivi ninavyozungumza mabwawa yangu saba katika Wilaya ya Mkinga ambayo yanatusaidia kupata maji yamepasuka. Miradi ya maji ambayo mabwawa

yamepasuka ni Bwagamacho, *Horohoro border*, Doda, pamoja na Machimboni na mradi wa maji Maramba mabomba yamesombwa na maji, kwa hiyo, mpaka kwenye hospitali yetu ambayo sasa tunaitumia kama Hospitali ya Wilaya imekosa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bwawa la maji Mwanyumba ambapo sambamba na hilo kuna daraja kubwa limepsuka na daraja limekatika, kwa hiyo, mawasiliano kati ya Tarafa ya Maramba na Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga yamekatika. *Scheme* yetu ya umwagiliaji Mwakijembe imesombwa na maji, mitaro imejaa mchanga, hekta karibu 98 za mazao zimesombwa. Athari yake; takribani watu zaidi ya 10,000 hawana maji.

Naiomba Serikali ilichukulie jambo hili kwa uzito mkubwa na kwa uharaka ili huduma ya maji iweze kurejeshwa. Ninawaomba ndugu zangu wa Mkinga waendeleo kuwa wavumilivu Serikali ninaamini itaifanyia kazi jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi naomba nianze mchango wangu kwa kunukuu taarifa ya wataalam katika jarida la *World Water and Sanitation*. Katika mchango wao pale wanasema na ninanukuu:-

“The world does not stand a chance without water, it spread disease, compromise safety, makes education elusive and economic opportunity further out of reach. The lack of access to safe and clean water is deadly, dangerous and major obstacle to people of developing world becoming economically empowered and it is what it is standing between billions of people and their health, safety, opportunity to unlock their potential.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali yangu isikubali ukosefu wa maji ukazuia fursa za maendeleo kwa watu wetu. Naiomba sana Serikali yangu isikubali ukosefu wa maji ukawa chanzo cha vifo vya watu wetu.

Wale tuliokuwemo kwenye Bunge lililopita wanakumbuka, tulijadili mambo kwa kina hapa katika Bunge hili wakati tunazungumzia kuweka tozo kwenye mafuta ya taa ili kupata fedha za kupeleka umeme vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia watakumbuka *sentiments* zilizokuwepo, hofu ya kuleta mfumuko wa bei na kadhalika, lakini tuliishauri Serikali na hatimae ikakubali, tukaweka tozo kwenye mafuta ya taa na leo kila mtu anashangilia upatikanaji wa umeme vijijini. Wananchi walikubali maumivu yale na leo wanashangilia umeme vijijini. Tusiwe wazito kukubali ushauri wa Bunge hili kuongeza tozo ya mafuta ili tupate fedha za kupeleka maji vijijini, *let us unlock the potential of our people*, tuwape maji safi na salama. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Makao Makuu ya Mkinga hayana maji. Nimelisema hili kwa muda mrefu, nafurahi leo katika hotuba hii nimeona Wizara imetenga fedha kwa ajili ya kutengeneza mradi wa maji pale, lakini fedha zile nimeona zinagusa maeneo mengi, nimeona shilingi bilioni mbili pale; lakini fedha zile zinaigusa Handeni na maeneo kadhaa. Hofu yangu ni kwamba inawezekana fedha zile zisiweze kutosha kukamilisha jambo lile. Shida ya maji kwenye mji wa Kasera ni kubwa mno, naomba twendeni tukatekeleze mradi ule wa kutoa maji Kinyatu ambao utagusa kata za Mkinga, Parungu-Kasera, Boma pamoja na Manza. Tusaidieni tupate maji kwenye Makao yetu makuu ili tuweze kuujenga mji wetu, tuweze kuwahakikishia watu wetu afya bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine nilisema hapa kwenye bajeti iliyopita kwamba mji wa mpakani wa Horohoro ambako tumejenga Kituo cha Biashara ya Pamoja (*One Stop Border Post*) hauna maji. Tunapata aibu, watu wanakwenda kuchota maji Kenya. Tulikuwa na bwawa dogo pale ambalo lilikuwa linasaidia watu, leo hii ni miongoni mwa maeneo niliyosema hata bwawa hilo limepasuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mradi, tumeshafanya usanifu unaotoa maji Mwakikonge, mradi ule unahitaji shilingi

bilioni sita, tutakuwa tumemaliza tatizo lote la maji kwenye eneo lile. Naomba Serikali tusaidieni watu wale wapate maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni yamekuwepo malalamiko ya maji ya mji wa Tanga kuchafuka. Chanzo cha maji yale yanatoka Boshha na Mhinduro...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kitandula muda wako umemalizika.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wale hawana maji, tunaomba muwapatie maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante.
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere atafuatiwa na Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Dokta Prudeciana Kikwembe ajiandae.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kabla sijatoa hoja yangu ya kuunga mkono niwape pole wakazi wa Jimbo langu la Bunda kwa taabu kubwa waliyonayo ya upungufu mkubwa wa chakula na niwahakikishie kwamba Serikali kwa maelekezo yake hivi karibuni inaweza kuwasaidia kupunguza tatizo walilionalo.

Suala la pili, niwape pole wanavijiji wa barabara ya Bukama, Salamakati, Mihingo na Mgeta ambayo imevunjika daraja zake kwasababu ya mvua na mkandarasi wiki ijayo au wiki mbili zijazo atakuwa kwenye site, kwa hiyo wategemee watapata huduma, kwamba Serikali inawasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme tu kwamba humu ndani pamoja na kwamba tupo Wabunge wengine

wa miaka mingi lakini pia kuna wazee humu ndani, hili suala la bajeti ya maji tumelisema sana, watu wameonyesha njia, lakini iko hoja ya msingi kwamba sasa litakwenda kwenye Kamati ya Bajeti ambayo itakaa na kulitazama upya. Sasa kama hiyo ndiyo hoja basi hakuna haja ya kulipinga ni kuliunga mkono tu kwamba pengine katika ongezeko litakalokuja litatusaidia kufanya mambo.

Kwa hiyo, mimi nitaiunga mkono hii bajeti mkono kwa sababu itakwenda na itarudisha majibu ambayo yataleta neema. Mambo mengine haya ya kuota kwamba CCM itakufa lini, unaweza ukakaa miaka mingi tu hujapata jambo hilo kwa sababu CCM pia ni nembo ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwenye hoja ya msingi ya Jimbo langu la Bunda. Haihitaji kusoma sana kujua kwama asilimia 72.6 ya huduma ya maji inayopatikana vijijini haihitaji kwenda darasa la saba wala la ngapi. Hivi kwa mfano, kama asilimia 72.6 ndiyo huduma ya maji vijijini, kwa lugha nyingine ni kwamba kama una watu milioni moja maana yake watu 726,000 wanapata maji vijijini. Yaani kama tuna vijiji 1,000 ina maana vijiji 726 tu vinapata maji sasa jamani hivi ni kweli? Maana yake ni kwamba vijiji 274 ndivyo havipati huduma ya maji. Hivi Waziri, wazee wangu hawa mmetoka sijui engineer sijui nini inahitaji hilo kutuuliza? Hivi takwimu hizi tunazipata wapi? Waheshimiwa Wabunge sisi wote tuko humu ndani, kwanini usituambie kila Mbunge atuletee vijiji vyenye huduma ya maji na wewe ukaviona kwenye asilimia? Msikariri bajeti hizi kwa mambo ya kukariri kwenye vitabu jamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazee wangu nyie ndiyo mnamalizia hivi, mkishatoka hapa na uwaziri unaacha. Kwa hiyo naomba mjikite kutusaidia sisi. Mbona Waziri wa Nishati na Madini ametuambia leteni vijiji ambavyo havina umeme, tumempa na ameviona vijiji vinaonekana, ninyi kwa nini hamfanyi hivyo? Mnakariri bajeti sio wataalam? Mimi ninawaambia kumekucha hali si nzuri sana. Kwenye Jimbo la Bunda amezungumza mwenzangu hapo, lakini niseme tu nimeandika barua tarehe 26/10/2016, utata wa miradi ya

Jimbo la Bunda nikataja mradi wa maji Mgeta-Nyangaranga. Nashukuru kwa sasa hivi mkandarasi yupo lakini bado anasuasua tu, anaweka leo bomba moja kesho haweki, hakuna kinachoendelea pale, mradi una miaka sita unahangaika tu, haiendi vizuri. Barua hii haikujibiwa; hata sikujibiwa mimi kama Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupewa nilichoandika jamani ni sawa? Mheshimiwa Waziri nimekuja kwako, Mheshimiwa Naibu Waziri nimekuja kwako, kwa Katibu nimeenda, sasa mnataka tuende wapi? Wazee wangu mnataka tuende wapi tuseme? Mradi wa Maji Mgeta matatizo, Mradi wa Nyamswa Salama Kati mmetenga shilingi 367,291,127, wanasema mradi umetengenezwa kwa asilimia 55 umekufa una miaka mitatu; mnataka twende wapi? Nimezungumza mkasema mtarekebisha miradi ya zamani iendelee, lakini hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mradi wa Kilolei shilingi milioni 400, vijiji vya Nyabuzume, Kiloleni na Kambugu shilingi milioni 400, ile mnasema visima kumi. Nimewaambia ofisini hakuna kinachoendelea, mnasema tuseme nini sasa kwenye hili? Ameandika Mhandisi wa Wilaya ya Bunda tarehe 1 Juni, 2016 miradi ya viporo vya madeni ya wakandarasi wa mradi wa maji Wilaya ya Bunda; mmeleta shilingi bilioni tano. Miradi karibu asilimia sabini na kitu asilimia haifanyi kazi, ninyi mkija kwenye asilimia hapa mnaandika maji yanapatikana Bunda, hayapo, hayapo Bunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ndugu zangu wamekuja watu wa *JICA* tumewapa taabu kubwa sana, tumewaambia watusaidie kwa sababu kwenye Jimbo langu la Bunda lina ukame mkubwa, wametuambia tufanye bajeti tumewapelekea bajeti ya dola 63,879 ya ukarabati ya marambo yaliyoingiliwa na magugu maji.

Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri mliwahi kujibu hapa Bungeni kwamba mwaka huu mtafanya ukarabati wa malambo sita, iko wapi mzee wangu? Sasa mnafikiria sisi Wabunge tufanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *JICA* hawa hawa wamesema tutengeneze malambo, tumewapa bajeti ya dola 255,237.17 tusaidieni basi, tusaidieni kwenye *JICA* hawa ambao wametuona kwenye tatizo mtusaidie kutusemea watusaidie. Jimbo la Bunda lina ukame wa kutisha, Jimbo hilo hilo ndio lina tembo wanaokula mazao ya watu kila siku, lina watu wana taabu zao kule; tunaomba mtusaidie kwenye jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona mradi wa umwagiliaji Bunda. Mradi wa umwagiliaji maji wa Nyatwali hauko Jimbo la Bunda, haupo Wilaya ya Bunda uko Bunda Mjini. *Bunda DC* kuna mradi wa umwagiliaji wa Maji unaoitwa Mariwanda pamoja na mradi wa Kasugutwa wa Buramba, haiku kwenye bajeti yanu; na kwenye takwimu zenu mnaonesha kwamba Mradi upo *Bunda DC* lakini upo Bunda Mjini. Kwa hiyo, naomba mlirekebishe hili na mradi wetu wa Mariwanda muufanyike kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu hebu tusaidieni, kama mmepeva hiyo Wizara na hali ndio hii inaenda miaka miwili sasa inaenda miaka mitatu na ninyi wazee ma-*engineer* mpo hapo, watu wazima ambao tunawategemea mtusaidie na hamna *plan* mpya ya kukomboa mambo ya maji, tunakaa na ninyi humu kufanya biashara gani? Maana sasa lazima tuwaambie kwamba miaka mitatu ijayo mtuambie mmeingia humu ndani mmekomboa nini au ndiyo zile asilimia mnazoimba tu asilimia 72 wakati hazipo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri naomba nimeandika kwenu, nimewaleta, kwenye Jimbo langu mnasema kwamba miradi ya zamani iendeleo kuwepo; na kwangu miradi ya zamani ipo, endeleeni kunisadia au mnampango wa kuniondoa huko ndani? Mniambie sasa mapema nijue.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda wako umekwisha ahsante sana. Mheshimiwa Savelina Mwijage atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Moshi Kakoso ajiandae.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nami ninaomba kuchangia Wizara hii ya Maji ambayo watu wengi wamechangia na mimi niweze kuchangia. Nilikuwa naomba sana, ningekuwa na uwezo hii Wizara ningeweka Mwanamke mmoja. Matatizo ya maji yanawasibu wanawake ndiyo maana tunapata matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha nne Serikali haikutenga pesa katika mradi wa maji Mkoa wa Kagera. Tuna shilingi bilioni nne za wahisani na Mkoa wa Kagera Mwenyezi Mungu alitujaaia vyanzo vya maji na kila siku naongelea hapa. Kuna Mto Kagera, tuna Ziwa Victoria na Itimba, tuna Buhigi; ukizunguka Mkoa wa Kagera mzima tuna vyanzo vingi ambavyo ni vya kuweza kuwasaidia Wana Kagera, lakini ndio wa kwanza wanabeba ndoo baada ya kutua ndoo wanabeba ndoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimeingia hapa mwaka 2005, kila mwaka nimelia na maji mpaka nimemaliza; na kila mwaka na kila bajeti tunalia na maji na ndio maana nasema hivi ukingalia Wizara ambazo wakina mama wameshika, wanajitahidi kutafuta vyanzo vya maji kuwasaidia akina mama wenzao ambao wanateseka na maji. Angalia Mheshimiwa Umyy, sipendekezi kwa sababu ni Kamati yetu, hapana, anajitahidi sana kuhangaika kutafuta vyanzo. Tunawawekezaji, mwekezaji akiingia kuwekeza ndani ya Mkoa au Wilaya kitu cha kwanza ukimwekea awe anachimba mabwawa kuwasaidia akina mama inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa ukiangalia hata kwenye hospitali hakuna maji, Hospitali ya Bukoba Vijijini akina mama wananunua ndoo shilingi 1,000. Ameenda kujifungua ataondoka na uchafu! Akina baba mmependeza kwa

sababu ya maji. Mama atafulia nini kukufulia suti yako? Tukikosa hata maji ya kufua suti akina baba labda mtakuwa na uchungu wa kuwatetea akina mama wasibebe ndoo kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wanatembea kilometa 20 au 15 kutafuta maji. Anaondoka asubuhi hajatafuta chakula, hajajua anapika nini, hajajua atalima wapi, hajajua atafanya nini lakini anakwenda kutafuta maji na maji yenyewe hayatoki; kama mnavyosema kwamba ni mabadiliko ya tabia ya nchi, mito mingi imekauka. Tuna mradi nimeuongetea hata hata mwaka jana, Mradi wa Kahama na Shinyanga, mnashindwa nini kuwasogezea watu wa Bukoba? Watu wa Muleba wamezungukwa Kanda ya ziwa yote imezunguka maji. Ukienda Ngara wana Mto Ruvu na Mto Kagera umezunguka una maji, watu wa Misenyi wanakunywa maji ambayo ukiyaangalie hata wewe kwenye glasi utafikiri ni maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtanzania wa karne hii mpaka huyu wa sasa hivi bado wanakunywa maji machafu kiasi hicho. Tuna Kienyabahsa kuna mto mkubwa ambao unaweza kusambaza hata Bukoba Vijijini. Tuna Ikimba ambayo inaweza ikasambaza hata Bukoba Vijijini na Wilaya zingine jirani; lakini ni kukosa kuwa na ma-*engineer* na Waheshimiwa Mawaziri muwe wabunifu wa kuweza kuleta hata wataalam kuchimba mabwawa ili watu wapate maji salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Karagwe kwa ndugu yangu Bilakwate, ni mjomba wangu, lakini pale ukienda utasikitika hawana maji kabisa na sasa hivi mvua inanyesha kwa nini usiwe na watalaam wa kuweza kutengeneza mabwawa angalau tukawa tunavuna maji ya mvua ya sasa hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalia na mafuriko hapa kila Mbunge anayesimama hapa analia na mafuriko. Yale maji tukiyavuna tukatengenezewa mabwawa kitaalamu tunaweza kupata maji miaka hadi miaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye kilimo cha umwagiliaji na ninalia kila siku, hapa huwa nauliza kwamba maswali ni kwa nini tusipate wataalam wa kuwafundisha wananchi wetu kulima kilimo cha umwagiliaji ili tukaweza kupata chakula cha kutosha na akina mama wakapata ajira ya biashara ya kuweza kuuza mboga na chakula? Kila siku tutakuwa tunasimama hapa tunalia na jambo moja la maji, maji/kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri nawaomba sana na ninyi mna wanawake mna mama zenu na ndugu zenu, muwasaidie hawa akina mama. Au tuwabebeshe ndoo, wakati mmoja na sisi wanawake tusimame tuseme wanaume mtuletee maji, mtaweza? Hamuwezi! Kwanza hata kusogeza chakula kwenyewe kukitoa hapa kukiweka pale unasema mwanamke kaniroga ananiambia nibebe chakula, sasa ukiambiwa ubebe maji! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, na wewe ni mama, tunaoma sana muwaokoe akina mama hata akienda kujifungua hospitali, akiwa nyumbani ama akitoka kulima apate maji. Hata mtoto anatoka shule anafika nyumbani anakuta mama hana chakula, hajapika ni kwa sababu ya ukosefu wa maji. Naomba sana tena sana kwa sababu kila mwanamke anaesimama hapa au mwanaume anaongelea hivo hivo kuhusu maji. Mheshimiwa Naibu Waziri sehemu ya Bukoba Mkoa mzima wa Kagera nimekutajia Mito ambayo inaweza ika-*supply* Mkoa mzima watu wote wakapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunakaa kusubiri bajeti ya Serikali na bajeti ya Serikali kwenye kitabu hamna, tunasubiri wahisani. Mtu akija kwako kukutembelea au kuja kwenye harusi yako akakuta wewe huimbi na yeye hawezi kuimba, sasa hao wahisani watakuwa wanatoa pesa mpaka lini? Wanakuta sisi hatukutenga pesa yeye mwenye anakuja kujitolea pesa, watachoka kutusaidia kama sasa hivi wanavyoendelea kuchoka katika kutuwezesha kwa angalau watuwekee bajeti kidogo ya kutusaidia sisi ili tuweze kupata hata mabwawa. Kila siku tukisimama hapa mnasema

wahisani, kila tukifanya hivi mna sema wafadhili, kwa nini Serikali yetu isiwe inaona kitu cha muhimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mnaanza kupanga miradi mipya, nimeona kwenye kitabu mna miradi mipya, kwa nini msimalize miradi ya zamani? Angalau mkasema Mkoa wa Kagera tunafanya hapa na Mkoa huu tunafanya hapa. Maliza miradi ya zamani ili msiwe na viporo kwa kuzidi kuongeza miradi mipya, itatusababisha kila siku tusimame hapa. Amesema Mheshimiwa Mnyika hata na mzee akizeeka anakaa chini mtoto anakimbia. Kwa hiyo, tunaomba CCM tuwasaidie huu mzigo umewachosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana tena sana, kilimo ni uti wa mgongo na kilimo tusitegemee msimu wa mvua. Hata mvua kama ya sasa hivi si inanyesha sana, kipindi kilichopita umetokea ukame mkubwa sana na mahindi yamekauka na maharage yamekauka, lakini sasa hivi maji ni mengi unayaona yamejaa tu, yatakauka tuendeleo kulia tena na maji. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, tafuta wafadhili waweze kutusaidia kuvuna maji ya kilimo tupate kilimo cha umwagiliaji ili tupate chakula cha kutosha, mboga za kutosha na akina mama waweze kupata biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tupo karibu na Uganda, akina mama wakiwa wamelima kilimo cha umwagiliaji tunaweza kuuza mboga sehemu mbalimbali. Kwa sababu ukiangalia ndizi zetu wanatoa Bukoba, Karagwe na Ngara wanapeleka Uganda. Ndizi hizo hizo za Mkoa wa Kagera zinasafirishwa kwenda nje lakini sisi wenyewe hatuna mahali hata pa kuuza. Kama tukiwa na mboga kama hizo watu wanakuja wananunua na akina mama hawawezi wakallilia, hata ukimwambia mama changia mradi wa maji hatakataa kuchangia kwa sababu najua matatizo anayoyapata. Akina mama wanachangia harusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii nasikia wanasema tuongeze tozo kwenye mafuta, sasa tutakuwa tunaongeza kila siku kama bajeti inakwenda kuongezwa kwenye vinjwaji.

Kila bajeti inayokuja wanaongeza kwenye vinywaji, vinywaji itakuwa kama hii hii ya kuongeza mafuta unaongeza kiasi fulani kwenye mafuta, tusiongeze hapo. Tutafute vitu vingine vya kubuni ili tuweze kupata na sisi watu wa kutusaidia au mradi wa maji uweze kupata na vyanzo vya maji... *(Makofi)*

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwijage muda wako umekwisha.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwijage hoja iliyopo mezani ni moja tu. Lakini hata hivo mzigo wa CCM nadhani ni mzito sana, CUF mnauweza kweli. *(Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, tunauweza!!

NAIBU SPIKA: Sawa, Mheshimiwa Dkt. Pudensiana Kikwembe atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Kangi Lugola ajiandae.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika hotuba ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji ambayo ni muhimu sana katika maendeleo ya binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba niwaaminishe ndugu zangu wa Kambi ya Upinzani kwamba CCM hajachoka kubeba mzigo, CCM ni kama tembo, tembo hachoki kubeba mkonga wake na wale wanaofikiri itatoka madarakani ni ndoto za mchana. Sasa niwaombe tu kwamba tuwe wavumilivu na Serikali hii makini inayotekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili naomba niendele kuwaomba ndugu zangu wa Kata ya Kasansa na Mamba wawe wavumilivu kwa mvua zinazoendelea na pili waweze kuchukua tahadhari kwa ajili ya kujinusuru na maafa yanayoweza kutokana na mafuriko; na mafuriko yale niliwahidi nayashughulikia na niko mbioni kukamilisha ili nikawatembelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishukuru Serikali yangu na niishukuru Wizara hii ya Maji, katika bajeti ya mwaka uliopita imeweza kunisaidia angalau nusu ya jimbo langu kupata maji. Vijiji vya Kashishi, Chamalendi, Mwamapulu, Ukigwamizi, Msadya, Maimba, Ikulwe, Kaunyala, Minyoso, Ntompola, Mkwajuni, Lichima, Kibaoni, Nyambwe, Lunguya, Ilalangulu, Mawiti karibu kote huko nimepata visima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo nililonalo gari la kuchimbia liko moja, kwa hiyo, naomba mniongezee magari angalau mawili ili tuweze kumaliza tatizo hili mara moja. Nirudi pale pale kwenye kata yangu ya Kibaoni, tuna mradi mkubwa na kisima kikubwa pale cha maji. Niliomba mnitafutie wataalam kuja kuangalia kisima pale tatizo ni nini sijapata taarifa, naomba nipate taarifa na nijue *status* ya pale kwa sababu kile kisima ndicho kinachosambaza maji katika kata ya Kibaoni nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na wenzangu wote waliotanguliza kusema sasa tuongeze tozo kutoka ile shilingi 50 tupate shilingi 100 na ikiwezekana 150 ili wananchi vijijini wapate maji safi na salama, maji ya kutosha na yawe endelevu isiwe kwamba yakifika kipindi cha kiangazi maji yanakuwa yanakauka hapana, tunaomba namna ambavyo tutafanya miradi yetu hii iwe endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudi tena kwenye mradi wangu wa umwagiliaji wa kata ya Mwamapuli, humu sijaona umetengewa fedha yoyote. Skimu ya Mwamapuli naomba nipate *status* yake. Katika bajeti iliyopita mliniambia mmenitengea karibu shilingi bilioni moja kwa ajili ya upembuzi yakinifu.

Kwa hiyo, ninaomba sasa kama upembuzi yakinifu mmeshafanya mniambie, kama ni pesa mtanipa kutoka kwenye hiyo asilimia tutakayoongeza ndiyo yenye uhakika zaidi naomba mnifikirie katika mradi huu, ni mradi wa Kitaifa kwa hiyo naomba muutafutie pesa ili tuweze kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale tumeshakufungua maghala manne na tuna mashine ya kisasa ya kuchambulia Mpunga. Sasa ile mashine inakaa bure pamoja na yale maghala yanakaa pale bure. Sasa naomba mradi huu uanze mara moja ili wananchi wanufaike na kazi walizojitolea za asilimia 20 za kuchangia maendeleo katika kujenga miradi ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niseme neno moja. Wapo wenzangu waliotangulia kuzungumza kwa kusema kwamba tupunguze tutoe hela kwenye *REA*, hapana. Si vijiji vyote vimekwishapata umeme, naomba ile tozo ya kwenye *REA* ibaki vilevile, tuhakikishe vijiji vinapata umeme. Nimekuwa nikilia kila siku na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kata zote zilizoko Jimbo la Kavuu pamoja na kata zote zilizoko Jimbo la Kwela kwa Mheshimiwa Malocha hakuna umeme hata kijiji kimoja. Jimbo la Kavuu lina umeme kata ya Kibaoni na *Usevya centertu*, Usevya ni nyumba kumi.

Kwa hiyo, ninaomba sana kwa sisi tunaotoka majimbo ya vijijini hii hela tusikubali ipunguzwe. Lazima tuhakikishe inapatikana tena kwa wingi na wananchi kule vijijini wana *enjoy* haya matunda ndugu zangu. Tusiwe wachoyo watu wa mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijijini ndio kwenye nguvu kazi kubwa, ndiko tunakotoa chakula na nimewaomba hata ndugu zangu wa Jimbo la Kavuu, tukivuna mazao yetu hakuna kupunguza bei, tulinunua kwa shilingi 25,000 kwa debe na wao wauze shilingi 25,000 na kuendelea ili mjini yapande zaidi na wakulima waone sasa wanapata chochote kidogo na kukuza maisha yao kwa sababu pembejeo walijinunulia wenyewe. Leo tunataka tuanze ooh, chakula kule kimefanya hivi, hapana, tuwaache wauze kwa

bei zile zile walizonunua ili na wao waweze kubadilisha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niongelee mradi wangu wa umwagiliaji wa Kilida. Mradi huu ulikula hela nyingi sana na ni mkubwa, umeharibika kutokana na mvua na mafuriko yaliyopita pale. Sasa sababu mvua bado zinaendelea niombe sasa Wizara na nimekwishaleta maombi yangu maalum, mabanio na mifereji na magati pale yavunjika. Kwa hiyo, zile mvua zinavyoendelea maji yale sasa yanahama kwenye ile kata yanaenda kujaa kwenye Mto Msadya ambao umefurika sasa kwenye kata ya Usevya. Kwa hiyo, niwaombe mshughulikia lile banio, Naibu Katibu Mkuu yupo hapa ananifahamu na hilo banio analifahamu, *Mr. Kalobelo* unalifahamu vizuri. Naomba mlisimamie sasa ili ile *scheme* irudi kwenye miundo yake ili tuokoe kata zingine zisipate mafuriko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naishukuru sana Serikali yangu, nawashukuru sana Wizara ninaomba magari mawili ya nyongeza yaje kunisaidia kuchimba vile visima, tena nashukuru ni visima virefu vitakaa muda wa mwaka mzima ili wananchi wangu wapate maji safi na salama, na shule zangu zote za msingi na sekondari zipate maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na ninaunga mkono hoja ninaomba ile tozo iongezewe asante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Moshi Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Kangi Lugola; Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa ajiandae.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru sana kwa kunipa nafasi hii, kuchangia bajeti ya maji. Awali ya yote niishukuru sana Serikali kwa kuweza kukamilisha baadhi ya miradi ambayo ilianzishwa kwenye Halmashauri yangu ya Wilaya ya Mpanda, naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja nashukrani za dhati ambazo Serikali imezifanya na kuonesha jitihada za maksudi za kutatua kero ya maji lakini bado Mkoa wa Katavi kwa ujumla tunatatizo kubwa sana la maji. Suluhisho la Mkoa huu katika kutatua tatizo la maji ili tuwe na uhakika wa kupata maji safi na salama ni vyema sasa Serikali ikajielekeza kupanga mipango mikakati ya kuleta maji kutoka ziwa Tanganyika mpaka Manispaa ya Mpanda sambamba na Halmashauri ya Nsimbo ili iweze kutekeleza mradi ambao kimsingi utatatua tatizo kubwa sana la maji. Mradi huu ukianza kwa kiwango kikubwa kwenye eneo la jimbo langu utasaidia sana kutatua tatizo la kero ya maji katika kijiji cha Itetemya, Kapalamsenga, Kaseganyama, Kasekese, Nkungwi, Sibwesa, Ikaka, Kabungu mpaka Mpanda Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba sana Serikali ielekeze nguvu kutatua tatizo la maji kwa kuyatoa maji Ziwa Tanganyika. Kama maji yanatoka Ziwa Victoria kuja Mkoa wa Tabora, zaidi ya kilometa mia 300 itashindwaje kuyaleta maji kutoka Ziwa Tanganyika mpaka Manispaa ya Mpanda Mjini ambapo ni kilometa 120 tu? Nilikuwa naomba sana hilo tulipe nguvu ili tutatue tatizo la maji ndani ya Mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya maji vijijini; maeneo haya vijijini kunashida kubwa sana ya maji. Nilikuwa naomba sana kwenye jimbo langu, kata ya Muhesi ni eneo ambalo kuna tatizo kubwa sana la maji, na kuna chanzo kizuri cha kutega maji tu ambacho kingetatua sana vijiji vyote vilivyopo kwenye kata ya Muhesi vikawa havina tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuna maeneo kwenye kata za Mishamo ambako kimsingi Serikali haikuwekeza, ni eneo ambalo kuna Watanzania wanya, eneo hili bado tunatatizo kubwa sana la miundombinu ya maji. Nilikuwa naiomba Serikali ipeleke huduma kwenye vijiji vya kata ya Mishamo, kata ya llangu, kata ya Bulamata ili kuweza kutatua tatizo la maji kwenye maeneo ambayo kimsingi yalikuwa yakihudumiwa na *UN* sasa hivi yako

mikononi mwa Serikali. Tunaomba sana Serikali iongeze huduma ya maji kwenye vijiji hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya umwagiliaji; tuna miradi ya umwagiliaji ambayo ilianzishwa na Serikali. Eneo langu tunamradi wa *scheme* ya Karema, Mwamkuru na Kabage. Hii miradi imechukua muda mrefu sana na imetumia fedha nyingi ambazo kimsingi zimechezewa tu na watu ambao walipewa dhamana ya kuisimamia. Miradi hii inaonekana ni mashamba ya fedha ambayo yanaliwa, lakini hayaleti tija ambayo imekusudiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii miradi imepewa fedha nyingi, lakini haisimamiwi vizuri, bahati mbaya sana hata Wizara yenyewe ambayo inatoa hizo fedha haina usimamizi, ni fedha ambazo zinachukuliwa tu kiana aina na zinaliwa bila kuwa na usimamizi wowote. Naomba Serikali iangalie kwenye maeneo haya na ninaomba Serikali ituhakikishie itakapokuwa inaleta majibu hii miradi itaikamilisha vipi ili iweze kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni usimamizi wa miradi. Serikali itakuwa inatoa fedha nyingi na kutoa ndani ya Bunge na Waheshimiwa Wabunge wakashangilia kwamba wamepata miradi, kama hakuna usimamizi mzuri hakuna kitu chochote kitakachokuwa kinafanyika. Kwa sababu fedha inatoka Serikalini inaenda kwenye Halmashauri ambapo hakuna usimamizi, halafu zile fedha ukizifuatilia zinarudi makao makuu. Tunaomba hili likomeshwe, tusidanganywe tuwe tunapewa changa la macho kwamba tumeletewa fedha baadae zinarudi kule ambako zilitoka. Tunaomba hii tabia ikomeshwe na tuhakikishe kwamba imefanyiwa kazi ili iweze kutekelezwa kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ambayo tungependa kuchangia ni uwiano wa miradi ambayo tunagawiwa. Sehemu hii ni vyema sasa Serikali na Wizara kwa ujumla ikaangalia, kwa sababu fedha nyingi zinazotolewa ukiangalia mgawanyo ambao unagawanywa

kwenda kwenye maeneo husika tunatofauti kubwa sana. Sasa tunaomba tupewe vigezo ni vigezo vipi ambavyo vinafanya maeneo mengine yanapata fedha nyingi na maeneo mengine yanapata fedha kidogo. Ukiangalia pengine maeneo ambayo yana fedha kidogo yana idadi ya watu wengi kuliko maeneo ambako yanapelekwa fedha zingine. Tunaomba Serikali iangalie ili tuweze kwenda sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la bajeti; bajeti ya Wizara ya Maji mwaka huu imepungua lakini bado Watanzania walio wengi wanahitaji huduma ya maji. Mimi niombe Serikali, ni vyema sasa tukajipanga kuhakikisha bajeti hii inaboreshwa na tusitoe fedha kwenye zile mradi wa REA hapana, naomba tukate kwenye simu, tunaweza tukapata fedha nyingi sana ili ziweze kuwasaidia wananchi kupata maji ambayo yatawasaida walio wengi. Vijijini kuna matatizo makubwa sana ya maji, hasa kwa akina mama, ni vyema Serikali sasa ikaangalia mfumo wa kupeleka huduma ya maji vijijini ambako ndiko Watanzania waliowengi wanaishi. Inavyoonekana ukiangalia vitabu hivi, karibu asilimia kubwa ya huduma ya maji inapelekwa maeneo ya mijini, lakini tunadanganyika, asilimia kubwa ya Watanzania wanaishi vijijini na hawa ndio ambao wanahitaji huduma ili waweze kuzalisha na kuweza kulisha wananchi wanaoishi mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naunga mkono, lakini nitahitaji majibu ya Serikali ili tuweze kuangalia ile miradi ambayo imeletwa na Serikali. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajiandae.

MHE. KANGI A. N. LUGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Mnyika nataka nikuhakikishie kwamba ni vyepesi sana ngamia kupenya tundu la sindano kuliko upinzani kuiondoa CCM madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kumpongeza Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa jitihada kubwa anazozifanya kwa kuwatetea wanyonge wa Tanzania na kutetea maslahi ya nchi hii. Ninampongeza kwa sababu amejitoa mhanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukawa Rais lakini usijitoe mahanga kwa ajili ya kupigania maslahi ya watanzania na kuziacha rasilimali zikiporwa na kutumiwa na watu wachache; ninampongeza sana Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli na ndiyo maana zile pushapu alizopiga, na yale majina ya tingatinga tuliyompa na zile nyimbo tulizokuwa tunaimba za Kisukuma *ling'ombe lyamapembe, lyekumakinda mumbazu* ndiyo maana sasa matunda tunaanza kuyaona, ndiyo maana amewanyima pumzi mafisadi, wakwepa kodi amewanyima pumzi hawapumui, wenye vyeti *fake* hao nao na wenyewe sasa ndio wanakandamizwa, ninakuomba Mheshimiwa Rais uendelee kukandamiza hapo hapo na wala usibadilishe gear. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge nianze kwa kuwapa nukuu zifuatazo, nianze na ukurasa wa 30 wa kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, anasema; "Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli amekuwa ndiye msemaji mkuu (*champion*) wa masuala yanayohusu maji Barani Afrika." Na kwamba Waziri mwenyewe ni Rais wa Baraza la Mawaziri wa maji Afrika kwa kipindi cha miaka miwili. Waheshimiwa Wabunge, u-*champion* huu naomba niwakushe, u-*champion* wa maji wa Mheshimiwa Rais wetu aliuanza wakati ule alipopiga *push up* kwenye kampeni, na aliponyanyuka kutoka chini kwenye *push up* aliwaambia Watanzania kwamba najua Watanzania akina mama mna tatizo la maji, ninakwenda kutatua tatizo la maji na ole wake Waziri wa Maji nitakayemteua asipowaleteeni maji nitamgeuza kuwa maji na Watanzania waweze kumnywa. Mheshimiwa Waziri, bajeti hii jiandae sasa unaenda kugeuzwa maji endapo tozo ya shilingi 50 haitakubalika na kuongeza pesa kwenye bajeti hii, kwa ajili ya kutatua kero ya maji kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini *champion* mkuu wa maji Waheshimiwa Wabunge ni Yesu Kristu Mwana wa Mungu. Ukisoma Yohana 19:26-28 Yesu alipopata maumivu msalabani anateswa wakati mama yake yuko pembeni, alimwambia; "mama tazama mwanao" na baadaye alipoona kwamba lazima haya yakamilike akasema; "naona kiu." Hakuna kitu kingine ambacho Yesu alikiona ni isipokuwa kiu, kiu ni maji na ndiye *champion* mkuu wa maji kwa ajili ya akina mama katika Taifa letu. Tatizo la maji kwa akina mama, huu ni mwaka wa saba nilipoingia Bungeni humu nilingia na nyoka ya shaba, nikawaambia akina mama msichague Wabunge ambao watapitisha bajeti isiyotatua kero ya maji. Leo ni mwaka wa saba maji bado ni kero kwa wananchi hasa Watanzania akina mama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie Wabunge wenzangu atakaye kwenda kupitisha bajeti hii kwa ndiyo! Ndiyo! Ndiyo! Ndiyo! Wakati Bajeti hii, haijaongezwa pesa ya tozo ya shilingi 50, niko tayali na mimi kuanzisha mwenge, mwenge wa sauti nitachukua kwenye *Hansard* sauti za Wabunge za ndiyo nitazikimbiza nchi zima kuwaambia akina mama sikilizeni Wabunge wanavyowasaliti na nyinyi hampati maji katika nchi yenu. Lazima tuwe na huruma kwa akina mama. Waheshimiwa Wabunge ni nani ambaye hakunyonya mtindi kwenye ziwa la mama yake katika nchi hii? Waheshimiwa Wabunge ni nani ambaye hakuishi miezi tisa kwenye tumbo la mama yake halafu leo inakuja bajeti ambayo haitatui tatizo la maji tunaendelea kufanya ushabiki katika suala la msingi la bajeti ya maji, hatutakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule vijijini kule Mwibara kule, miradi ya Buramba, miradi ya Kibara, Bunda Mjini amesema Mheshimiwa Ester Bulaya hapa, zaidi ya miaka kumi akina mama hawapati maji, kwa nini, ni kwa sababu ya Bunge hili lenye uwezo wa kutatua kero ya maji kwa akina mama tunafanya ushabiki na kupitisha bajeti ambazo hazitekelezeki. Naomba Waheshimiwa Wabunge tukatae. Nitashangaa kwa kweli Mbunge atakayepitisha bajeti hii ambayo haijaongezwa pesa za maji. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ngoja ni waambie, kule vijijini wako wanaume ambao sasa hivi ni vilema ambao akina mama wanawaacha vitandani saa kumi usiku na kurudi saa tano ilhali wanadhani wana wivu kwamba akina mama wanakwenda kufanya mambo mengine wanapanda juu ya miti, matokeo yake wanadondoka wanakuwa ni vilema, leo tunakuja kufanya mzaa hapa. Waheshimiwa Wabunge, kule vijijini wanaoga kwa zamu maji hayatoshi. Aoge baba, aoge mwanafunzi aende shule, lakini hata wale wanaopata maji ya kuoga na wao wanachagua sehemu nyeti tu za kuoga kwa sababu maji hayawatoshi, halafu tunakuja tunafanya mzaa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye umwagiliaji. Nilishasema hapa Bungeni. Kule Mwibara kuna bonde zuri kwenye Ziwa Victoria kuanzia Musoma Vijijini kule Bugwema linakuja linapita kwenye kata ya Butimba maeneo ya Kabainja linaenda Karukekele, Namhula, Bulendabufwe, Igulu matokeo yake linaingia mpaka Genge, Kisolya mpaka Nansimo lakini hatuna umwagiliaji. Tumechoka kuletewa mahindi ya msaada ya kilo nne kwa familia ilhali tuna maji ya Ziwa Victoria. Tunaomba miundombinu ya umwagiliaji. Nimeangalia kwenye kitabu hiki hakuna kabisa, lazima tutende haki kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye mgawanyo wa fedha za maji. Nilikuwa nasoma humu unakuta kuna Halmashauri nyingine zina kata sita wana shilingi bilioni nne za maji. Kuna Halmashauri nyingine wanakata 20 mpaka 30; kuna Halmashauri nyingine zina majimbo mawili lakini wanapata shilingi milioni 800 tutakwenda wapi sisi, tutawambia nini wananchi wetu kwenye mgawanyo kamba huu? Tunasema tunagawana sungura mdogo, haiwezekani Halmashauri nyingine; niliona ya Mheshimiwa Kitwanga hapa ana shilingi bilioni nne wengine tuna shilingi 500,000,000 au kwa sababu anatahisha kung'oa mitambo ya maji ndiyo sababu mnapatia maji? Haiwezekani, huyu sungura mdogo lazima tugawane hapa pasu kwa pasu; haiwezekani kabisa Halmashauri ipate shilingi milioni 500 wengine wana shilingi bilioni nne; haiwezekani tukamla kuku wengine wakachukua

mapaja, wengine wakachukua mnaita chenye mafuta mafuta kile, halafu wengine mafuta mafuta yale, kakiuno kana mafuta na haka kakiuno kenye mafuta ndiko ambako wewe Waziri umechukua, ndiko wewe Naibu Waziri umechukua na sisi tunakataka hako, na sisi tunataka mafuta haiwezekani... *(Makofi/Kicheko)*

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kangi Lugola, muda wako umemalizika.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mheshimiwa Vedasto Ngombale ajiandae.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, niruhusu na mimi niungane na wale waliompongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri, lakini nimewasikiliza Wabunge wenzangu kwa umakini sana tangu jana na leo, tatizo hapa ni rasilimali fedha. Hakuna zaidi ya hapo kwa sababu hata tukipiga kelele namna gani, tukiimba namna gani kama hakuna pesa hata hii miradi tunayoiombea saa hizi haiwezi kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitoe ombi kama alivyotoa Mheshimiwa Kangi Lugola pale, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu, wa vyama vyote tukubaliane kimsingi, yale mapendekezo ya mwaka jana ya tozo ya shilingi 50 yaongezeke sasa yaende shilingi 100. Yakiwa shilingi 100 yatatupa shilingi bilioni 316. Hizi ukizijumlisha na fedha za ndani ambazo ni shilingi bilioni 408 ukajumlisha na fedha za nje ambazo ni shilingi bilioni 214 unapata jumla ya shilingi bilioni 940 na zaidi. Fedha hizi shilingi bilioni 940 inazidi hata ile bajeti ya mwaka jana. Sasa ili tufike huko, tukubaliane tu kimsingi tutoke kwenye 50 ya tozo twende shilingi 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunataka kweli miradi yetu hii ambayo tunaizungumzia humu ndani iende ikatekelezwe, tukubaliane kwamba shilingi bilioni 316 kila mwaka ziende kwenye miradi ya maji. Tukijipa miaka mitatu, tutakuwa na karibu shilingi trilioni moja, zote hizi zinakwenda kwenye maji. Najua matatizo ya maji kuanzia 2018, 2019 na 2020, kama tutakuwa na pesa hizo shilingi trilioni moja na zaidi, nina uhakika matatizo ya maji yanaweza kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili matatizo ya maji yapungue, ni lazima tuamue kwamba sh.50 itoke huku iende sh.100. Lazima tuamue! Bila kuamua kwa sababu hakuna sehemu nyingine, tukitegemea bajeti ya Serikali ya shilingi milioni 408 na pesa za nje shilingi milioni 214, fedha za nje zinaweza zikaja kidogo au zisije. Sasa ili tuondoke huko, ni lazima Bunge lako liamue, kwamba shilingi 50 tuachane nayo, twende kwenye shilingi 100 itakayotuzalishia shilingi bilioni 316 kila mwaka na hizi zinakwenda kwenye maji. Bila kufanya hivyo, tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuamue sisi Wabunge wote. Naomba Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Mama Hawa Ghasia, naomba mwende mlisimamie hili. Mwaka 2016 tulikubaliana humu ndani, lakini halikutekelezwa, tunaomba mwaka huu, mlibebe kama lenu, lakini ni la Bunge zima. Yale maneno kwamba itashusha *inflation*, *inflation* hii itashuka lakini *in multiple effect* itakuwa ni kubwa zaidi, kwa sababu matokeo ya kuongeza sh.100/= *multiple effect* yake itakuwa ni kubwa zaidi tofauti na tunavyofikiria. Naomba sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mama Hawa Ghasia hili walibebe ili kusudi waende kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali angalau kwa kuanza mradi wa maji wa *Ziwa Victoria*. Naomba *process* zilizoanza ziharakishwe. Mwaka 2016 tulitenga shilingi bilioni moja, hakuna kilichofanyika; mwaka huu imetengwa

shilingi bilioni mbili, najua yupo hapa Mheshimiwa Lwenge, hili suala nafikiri ni la kusukuma haraka haraka ili kusudi mradi huu ukamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Kwimba, tayari nimeshamwandikia Mheshimiwa Waziri kwamba kuna visima vya maji 188 Wilaya nzima, havifanyi kazi, vimezeeka, maji hayatoki na pampu zimeibiwa. Visima 188 kwa Wilaya nzima ya Kwimba, Majimbo mawili Sumve na Kwimba, maana yake mimi ndio Mbunge ninayejumuisha Majimbo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hii dhana ya kuwatua ndoo akinamama ili ikamilike na iwe na uhalisia visima hivi 188 tuangalie namna ya kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna miradi mingine minne ya maji ya *World Bank* imekuwa ya muda mrefu sana, leo ni zaidi ya miaka 10 na kila siku nimekuwa nikiuliza swali humu ndani. Mheshimiwa Lwenge, matatizo yaliyoko kule hayasemek! Watu wana urasimu wa kumwaga. Ukiuliza hiki, unaambiwa Mkandarasi; ukiuliza hivi, utaambiwa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kuondoa kero iliyopo kwenye maeneo hayo. Kadashi na Isunga tatizo ni kubwa, nimemwandikia, mengine yako chini ya asilimia 45 mengine 50, tatizo wanasema hela mnazo ninyi, wengine wanasema hela ziko huku. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri hili alisimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kuomba tena, hata ukitaka maji kule Tukuyu, najua kuna mvua nyingi tu huko, kwa Mheshimiwa Spika pia anataka maji; bila kukubaliana hapa ongezeko la shilingi 50 kutoka kwenye shilingi 50 kwenda kwenye shilingi 100 tutakuwa tunasema hapa, tutaimba umwagiliaji sijui vitu gani; tutazame *REA!* Tulivyoanza *REA*, tulikubaliana humu ndani; leo tazama vijiji karibu vyote vinakwenda kupata umeme kwa sababu ya makubaliano

ya humu ndani. Pesa za Mfuko wa Barabara sabini kwa thelathini, tazama barabara zetu leo ni sababu ya kukubaliana. Naomba na hili sasa na lenyewe tukubaliane tutoke kwenye shilingi 50 twende kwenye shilingi 100 ili tupate shilingi bilioni 316 kila mwaka ili tuweze kujenga visima na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Na mimi naamini hilo ulilochangia hapo mwisho Mheshimiwa Waziri amelisikia.

Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Vedasto Ngombale na Mheshimiwa Felista Bura ajiandae. *(Makofi)*

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwa mara ya kwanza. Niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kutoa pole kwa wananchi wa Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwaangalia rafiki yangu Mheshimiwa Kangi Lugola, ameondoka; naanza kwa kuunga mkono hoja, nami ndiye nitakayeongoza ile sauti ya ndiyo ambayo atazunguka nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya kwenye Idara ya Maji. Sisi wengine ni waathirika wa miaka mingi na tunaona mabadiliko yanavyokwenda kwa *speed*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niko tofauti kidogo na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanaosema tusipitishhe, hela ni ndogo. Binafsi yangu naona hii hela ni nyingi sana, tatizo itoke yote. Kwenye bajeti ya mwaka 2016 ukisoma ukurasa wa 13 utaona tulipitisha shilingi bilioni 915 lakini mpaka leo ni shilingi bilioni 181 tu. Kwa hiyo, Wizara ya

Fedha wakitoa pesa yote, hii pesa ni nyingi wala hata hizi kelele hatutazisikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha pili, kwenye Ilani ya CCM tumeahidi kumaliza matatizo ya maji, lakini hatukuahidi kumaliza mwaka huu peke yake, bado tuna miaka mitano. Kwa hiyo, kazi zilizoahidiwa kwenye Ilani ni nyingi, wala siyo moja na kila mahali tunataka pesa. Sisi tunataka barabara, tumepiga kelele tunataka afya, tunataka watoto wasome bure; kwa hiyo, hizi hela ni nyingi, tuziunge mkono, wala tusiwasumbue, tuwape nafasi waende wakafanye kazi. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: *Yes!*

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, mimi nashangaa wana-CCM wenzangu, jana nimesikiliza mchango wa Mheshimiwa Kitwanga analalamika anasema yeye ataenda ku-*mobilize* wananchi 10,000 wakazime mashine. Nilisikitika sana! Nataka niwaulize ninyi Mawaziri wa Mheshimiwa Dkt. Magufuli, hivi vile viapo mnavyovila mnavifahamu maana yake? Kama hamvijui sina hakika kama mko sawasawa na kama hamko sawasawa Mheshimiwa Ndalichako hebu apitishe *operation* ya vyeti, pengine na kwenyewe kuna feki za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana vipi mtu aliyekuwa Waziri anasimama anasema kwa kuwa nilikuwa Waziri, nilikuwa nimebanwa kuzungumza. Kwa hiyo, sisi ambao hatuzungumzi kwa kuwasaidia ninyi, tumebanwa na nani? Anasimama anasema nilikuwa nimebanwa, sasa nazungumza, naenda kuunganisha wananchi 10,000 wakazime mashine ya lhelele. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwakumbushe kidogo, mwaka 2014 Mheshimiwa Kitwanga nilitegemea atakuwa pale. Akiwa Waziri wa Nishati na Madini, aliyekuwa anashughulika na mambo ya madini, alikuja Geita, mimi kama Mwenyekiti wa Mkoa niliwalazimisha wananchi wasitoke mpaka walipwe na Mzungu. Yeye akaja,

akamwambia Mkuu wa Mkoa, hata kama kuna Mwenyekiti wa Mkoa, piga mabomu. Kweli kesho yake tulipigwa mabomu!

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie Waziri wa Mambo ya Ndani, siku anaenda kuunganisha wale wananchi, apeleke mabomu Misungwi pale, aonje joto la jiwe. Haiwezekani Waziri aliyeapa kiapo, akitimuliwa anakuja humu anatuchanganya sisi wengine ambao hatujui mambo mnayoongea kwenye *Cabinet*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ndugu yangu Mheshimiwa Nape yuko hapa, jana alichangia...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Hakuna kuogopana humu, anayeguna nani? Mimi ndio nachangia. Ndugu yangu Mheshimiwa Nape aliyekuwa Mwenezi wangu wa Taifa, jana alizungumza mambo mazuri, lakini kuna moja alisema tusipowatekelezea suala la maji wananchi, hawataturudisha, haiwezekani! Wananchi wa Tanzania wanatutegemea kwa mambo mengi wala siyo maji peke yake na tumewafanyia vizuri. Hata hizi Ilani hazijaanza kuzaliwa kwenye Awamu ya Tano, tumepitisha awamu nne, zote zilikuwa zinaandaa hayakamiliki. Kwa hiyo, suala hapa siyo kulazimisha Ilani yote ikamilike. Rais gani aliyewahi kutekeleza asilimia mia moja ya Ilani? Tusibebeshane mzigo!

(Hapa kuna Mbunge alikuwa akiongea na mchangiaji bila kufuata utaratibu)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Wewe ulikuwa unaongea nilisikiliza, sikiliza! Kwa hiyo, tupeane nafasi, Rais wetu anafanya kazi nzuri, tusianze kumchambachamba humu ndani. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri aliyoifanya pale Geita. Tulikuwa na malalamiko ya awamu mbili. Leo ukifika Geita,

hatujawa na asilimia mia moja lakini tuna nafuu. Tuna mradi wa shilingi bilioni sita; uko asilimia karibia 85, halafu tusimame hapa kuiponda Serikali ya Awamu ya Tano, kwa miaka miwili! Haiwezekani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Wabunge wamo humu akina Mheshimiwa Mnyika, unataka tumalize tatizo la maji leo, kwa nini haisemi *population* ya Dar es Salaam? Wakati anaomba maji Awamu ya Kwanza alivyokuwa Bungeni, Jimbo lake lilikuwa na watu wangapi? Kila siku binadamu wanaongezeka, hatuwezi kumaliza tatizo hili kwa awamu moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuiptishe bajeti hii kwa *speed*, tushauri tu kwamba Wizara ya Fedha iachie fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongee kidogo kwamba tumeona mfano kwa *CEO* wa *DAWASCO*; hivi Mheshimiwa Waziri watu kama hawa, wamesifiwa mpaka na Kamati, tunawezaje kutafuta watu kama akina Ruhemeja kwenye Tanzania hii? Mtu amekuta kuna deni la shilingi bilioni 40 na kitu, leo hakuna deni! Kwa nini watu kama hao msiwachukue na kuwapa vyeo vingine vikubwa ili wakawafundishe na Wakurugenzi wa kwenye Halmashauri nyingine na Majiji mengine? Tusikae hapa kuiponda bajeti, *issue* kubwa hapa hela zitoke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzengu wa CCM, Kanuni ya 105 imeelekeza jinsi ya kufanya, hatuhitaji kuiponda bajeti hapa, tunahitaji kuwapa zile siku sita wakajadili, waje watuambie, lakini bajeti ipite tena kwa ndiyo. Kama Mheshimiwa Kangi Lugola anataka kuzunguka na ndiyo za Waheshimiwa Wabunge, *term* hii sasa aandae *record*, ataenda na za *bass* ambayo hajawahi kuiona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Vedasto Ngombale, atafuatiwa na Mheshimiwa Felista Bura na Mheshimiwa Abdallah Ulega ajiandae.

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niseme yangu katika Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji. Awali ya yote, nachukua nafasi hii kutoa pole zangu kwa wenzetu wa Arusha kutokana na msiba wa wanafunzi. Namwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuunga mkono wale wote wanaosema kwamba bajeti ya Wizara hii iongezwe. Kwa ukweli kabisa kama tuna kusudio la kutaka kuwatendea haki wananchi wa Tanzania, basi tuna kila sababu ya kuongeza bajeti ya Wizara hii ili wananchi wakapate maji ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, falsafa ya kumtua mama ndoo kichwani, ililenga zaidi kwa wananchi wanaoishi vijijini. Kwa mazingira yetu, sehemu nyingi za mijini zina maji na ikiwezekana miundombinu yake, maji haya yanaenda kabisa mpaka majumbani. Sehemu ambazo bado akinamama wanabeba ndoo kichwani ni sehemu za vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifuatilia bajeti, bado imekuwa na upendeleo zaidi kwa maeneo ya mijini kuliko maeneo ya vijijini. Jimbo langu ni la kijijini na hakuna mradi wowote wa maji uliotengwa katika bajeti hii. Nimesoma kwenye kitabu hiki hakuna chochote kilichowekwa kule. Sasa ina maana kwamba mwaka huu wa fedha unanipita hivi hivi. Namwomba Mheshimiwa Waziri, wananchi wa Jimbo la Kilwa Kaskazini awaangalie, hakuna chochote alichotenga kwa ajili yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimeangalia pale, Mkoa wa Lindi umetengewa pesa kama *1.1 billion* fedha za wafadhili. Basi naomba zile pesa ziwaangalie pia wananchi wa Jimbo la Kilwa Kaskazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nachukua nafasi hii kupendekeza kuanzishwa kwa Wakala wa Maji Vijijini, kwa sababu vinginevyo basi mgawanyo wa keki hii, wenzetu wa mijini au wenzetu wa baadhi ya Majimbo watakuwa wanapata zaidi kuliko sehemu nyingine. Kwa hiyo, basi uanzishwe Wakala wa Maji Vijijini ili vile vijiji ambako ndiko Watanzania wengi wanaishi waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, nijielekeze katika matatizo ya maji katika Jimbo langu. Jimbo langu ambalo lina Kata 13, kuna Kata kama sita hivi, bado hazijawa na mradi wowote wa maji. Kuna Kata ya Somanga ambayo iko pale barabarani haina mradi wa maji, Kata ya Kinjumbi, Kata ya Kibata, Kata ya Chumo, Kata ya Namayuni na baadhi ya vijiji katika Kata ya Kipatimu; kuna Vijiji vya Nandete, Intikimwaga, Nandemo, Mkarango na Kijiji cha Nasaya; vyote hivi havina mradi wowote wa maji. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri ayaangalie maeneo hayo nao waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza utekelezaji wa Wizara kwa Mradi wa Maji wa Mingumbi Mitete. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, tumekuwa tukishirikiana na ule mradi umeelekea kukamilika. Ule mradi unapitia katika Kijiji cha Njia Nne. Namwomba Mheshimiwa Waziri wananchi wa Kijiji cha Njia Nne wapate maji katika mradi ule kwa sababu haiwezekani likapita bomba tu pale halafu wao waliangalie. Ule mradi unaopeleka maji katika Vijiji vya Mingumbi, Poroti, Nangambi na Ipuli, Tingi, Mtandango na Miteja, lakini wale wa Njia Nne wamesahaulika. Kwa hiyo, naomba pia na wale wa Njia Nne waweze kupata maji katika ule mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, nijielekeze katika matumizi ya chanzo cha Mto Rufiji. Tumekuwa tukiona hapa, vyanzo vyote vikubwa vya maji tayari vinatumika kwa ajili ya matumizi ya maji kwa wananchi wa maeneo hayo. Kuna chanzo cha Ziwa Victoria, Mto Malagarasi na sehemu nyingine; lakini mpaka sasa na nimekuwa nikishauri mara

kadhaa, Serikali haijakiangalia chanzo cha Mto Rufiji kwa ajili ya wananchi wa Rufiji na Kilwa. Mpaka sasa yale maji yanapotea tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji wanaita *RUBADA*. Wapo pale, lakini sioni kama kuna jitihada zozote zinazofanyika, maana hakuna mipango yoyote ya umwagiliaji inafanyika pale; yale maji yanatupita tu hivi hivi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie ana mpango gani wa kuhakikisha kile chanzo cha Mto Rufiji kinatumika kwa manufaa ya watu wa Rufiji, Kibiti, Kilwa, Kilwa Kusini na maeneo ya jirani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nijielekeze katika ripoti ya Mkaguzi na Mdhhibiti wa Hesabu za Serikali. Mkaguzi na Mdhhibiti wa Hesabu za Serikali anaeleza kuwa kuna zaidi ya pesa shilingi bilioni nne zinapotea kutokana na miradi kukamilika, lakini kutotumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*) na tumefanya ziara za ukaguzi wa miradi maendeleo katika sehemu mbalimbali za nchi hii. Tulichojiifunza huko, kuna miradi mingi inakamilika, lakini haitumiki na moja ya miradi hiyo ni miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna mradi kule Nachingwea, kuna mradi kule Tabora, miradi ile imekamilika lakini haitumiki. Tatizo kubwa, kuna shida kubwa kwa *Ma-planner* wetu wa Halmashauri. Wasanifu wetu, wanasanifu miradi ambayo baada ya kuja kukamilika wananchi wanashindwa kuitumia. Kwa mfano, kuna mradi pale Nachingwea, ili wananchi waweze kutumia ule mradi, basi inahitaji ndoo moja ya maji inunuliwe kwa sh.300/= kitu ambacho wananchi hawawezi kumudu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna shida kubwa kwa wataalam wetu wa Halmashauri kusanifu hii miradi. Naomba wataalam wanapokaa na kusanifu hii miradi wawe

makini sana na wawashirikishe wananchi kuona namna gani wao wanaweza wakaimudu hiyo miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Felista Bura, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Ulega.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, lakini pia namshukuru Mungu wangu kwa uzima na afya njema aliyonijalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wote wanaosema kwamba bajeti ya Wizara ya Maji iongezwe, kwa sababu maji ni uhai. Nami kama mwanamke ambaye wenzangu wanahangaika usiku na mchana kutafuta maji, napata shida sana ninapowaona wenzangu hasa wa maeneo ya vijijini ninapofanya ziara; siku moja nililetewa maji ambayo sikujua kama ni majivu au ni maji, lakini yalikuwa maji ambayo wananchi wangu walikuwa wanayatumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kwamba katika Mikoa ya Kanda ya Kati, Mikoa ya Singida na Dodoma Serikali itutazame kwa jicho la huruma sana kwa sababu hatuna mvua. Nimemsikia Mbunge wa Mkinga akisema kwamba kwake mvua inanyesha na imepitiliza, lakini hata kwa Mkoa wa Dar es Salaam mvua zinanyesha sana, Mikoa ya Kanda ya Kusini mvua zinanyesha, lakini sisi tulishasahau mvua; na mvua zinazonyesha sasa hivi haziwezi hata kujaza dimbwi. Kwa hiyo, wanawake wa Mkoa wa Dodoma wanateseka mno kwa kutafuta maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nahisi maeneo ya vijijini watu wameacha mambo ya dini wakaoa wanawake wengi hasa Wakristo, kwa sababu ukioa wanawake wengi mmoja akiwahi kwenda kisimani mwingine atabaki kulinda mji. Kwa hiyo, wanapata shida. Asubuhi saa kumi ndiyo wanatoka kwenda kutafuta maji na wanarudi saa tano

mwanamke akiwa na ndoo moja na asubuhi wanaondoka na majembe na ndoo kichwani na jioni anarudi na ndoo na jembe begani. Naomba ufike wakati sasa Serikali ione namna ya kuisaidia hasa Mikoa hii ya Kanda ya Kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Dodoma na viunga vyake, unakua kwa kasi kubwa sana, lakini miundombinu ya maji ni ile ile. *DUWASA* bajeti yake ni ile ile, vijiji vinavyozunguka Mji wa Dodoma wanategemea *DUWASA* kupata maji, *DUWASA* haina uwezo wa kusambaza maji kwa vijiji ambavyo viko eneo la mji huu. Mji huu wameshakuja wafanyakazi 2,800 kwa taarifa nilizopata hivi karibuni, lakini miundombinu ya maji iko pale pale. Maji yanatoka Mzakwe Kijiji cha Veyula hakina maji; *UDOM* hapa Ng'ong'ona hawana maji, Mkonze karibu tu na Kilimani hapa, hawana maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Serikali iangalie kwa jicho la huruma Mji wa Dodoma kwa sababu unakua kwa kasi kubwa sana na miundombinu ya maji taka ndio hatuwezi kusema kwa sababu miundombinu ya majitaka *DUWASA* hawawezi peke yao bila mkono wa Serikali. Serikali iwasaidie *DUWASA* kuweka miundombinu ya maji taka lakini na maji ya kunywa kwa wananchi wa Dodoma Mjini pamoja na viunga vyake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali sasa, tumesema kuna maji, kuna mvua katika maeneo mengi, lakini shule zetu za sekondari na shule zetu za msingi hawana maji. Kwa nini Serikali isitafute namna ya kuvuna maji kwa shule zetu, Vituo vya Afya na Zahanati ili suala la maji katika Vituo vya Afya, Hospitali, Shule za Sekondari na Shule za Msingi sasa iwe ni hadithi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizingatia kwamba sasa hivi wazazi hawatakiwi kuchangia; hawachangii ada, lakini ukiwaambia wachangie kulipa bili ya maji hawakubali, lakini tukivuna maji hatutahangaika kuwaambia kwamba wachangie bili ya maji. Kwa hiyo, Serikali ione namna sasa

ya Vituo vyetu vya Afya na Shule za Sekondari na ikiwezekana Shule za Msingi pia wapate maji kwa kuvuna maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa vijiji kumi haujafanikiwa katika Mkoa wetu, maeneo mengi mradi wa vijiji kumi kupata maji haujafanikiwa sana na haujafanikiwa sana kwa sababu waliokuwa wana-*monitor* ni Wizara. Kwa hiyo, Halmashauri zetu hazikuwa na nafasi ya kusimamia ipasavyo. Wakandarasi ambao wamefanya kazi zao vizuri, walipwe ili wakamilishe kazi zao.

Pia tuna suala la Tanzania kuwa nchi ya viwanda, lakini viwanda, malighafi watapata wapi? Kwa sababu malighafi kwa sehemu kubwa ni mazao na mazao tunategemea mvua. Suala la umwagiliaji litiliwe mkazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna bwawa la Kongogo lina miaka minane halijakamilika. Miaka minane hata skimu yenyewe haijaandaliwa. Wananchi wameshasubiri mpaka wamechoka, ile skimu ya Kongogo haijafanya kazi. *Contractor* aliyekuwepo, mpaka ameondoka skimu haijafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji ya Maporomoko ya Ntomoko, tuliwahi kumpeleka Mheshimiwa Waziri Mkuu Mstaafu aliyepita, Mheshimiwa Pinda mwaka 2013/2014 na akatuahidi fedha na akapeleka, lakini hazikutosheleza na mradi ule una uwezo wa kusambaza maji vijiji kumi na nane. Sasa hivi nimeona vijiji vinane tu ambavyo vimewekwa kwenye bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana na suala la Farkwa. Farkwa litasaidia sana maji ya Mzakwe, Bahi, Chemba na Chamwino, lakini mradi ule tume....

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umemalizika.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, lakini suala la Farkwa Ntomoko na Dodoma Mjini...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Ulega, halafu tutamalizia na Mheshimiwa George Lubeleje kwa dakika zitakazokuwa zimesalia.

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia mjadala wa hotuba hii ya maji. Nami naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na niwapongeze sana kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajielekeza katika kuwaomba maji wananchi wangu wa Mkuranga, uniruhusu nitumie nafasi hii ya dakika moja, mbili kuwaonesha Watanzania kwamba Chama cha Mapinduzi bado ndiyo Chama imara chenye haki ya kuendelea kuwaongoza Watanzania. Tulipokuwa katika uchaguzi wa *East Africa* kwenye Bunge hili, hatua ya kwanza Chama cha Mapinduzi kiliwakataa Mheshimiwa Wenje na Mheshimiwa Masha. Wenzetu wakaondoka wakaenda kuwaambia Watanzania kwamba sisi tunataka kuwachagua watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jana unafiki wa Vyama vya Upinzani umedhiri katika Bunge hili. Wale waliowaleta sisi tukawakataa, wametusaidia jana kuwakataa kwa vitendo. Makamu Mwenyekiti wao Profesa Safari wamempa namba ya viatu, namba 35, Wenje wamempa namba 34, Masha wamempa namba 44. Tunaendelea kuwaambia Watanzania kwamba Chama cha Mapinduzi ndicho chama cha kweli na ndicho chama cha kukiamini na Wapinzani hawa ni wanafiki wakubwa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo na ujumbe umefika, naomba nisema yafuatayo sasa.

MHE. MWITA C. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu utaratibu! Kuhusu utaratibu!

MBUNGE FULANI: Kaa kaa wewe!

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Waitara, tulia mwanangu, uchome sindano hizo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ulega ngoja tusikilize kuhusu utaratibu.

Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Mheshimiwa Waitara.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. MWITA C. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ninasimama kwa Kanuni ya 68(1) ikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 67(a) – (g).

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja iliyoko mezani ni kuchangia Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Vilevile kanuni ya 64 inazuia kutoa maneno ya kuudhi na ambayo hayana ukweli.

Sasa mchangiaji anaposema kwamba sisi Wapinzani ni wanafiki, naomba kwa viwango vyovyote athibitisha kauli hiyo ni kweli ama siyo kweli? Pia unisaidie kama maneno hayo yanaruhusiwa humu ndani wakati wa mchango kama huu? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waitara amesimama kueleza kwamba kuna Mbunge hafuati utaratibu kwa mujibu wa Kanuni ya 68(1), akataja 67 ambayo haina hivyo vifungu alivyovitaja; akaenda Kanuni ya 64 akasema mchangiaji anatoa lugha ya kuudhi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwanza tuwe na utulivu Bungeni; moja. Pili, tuwe tunafuatilia michango ya pande zote mbili. Mchangiaji aliyezungumza huko nyuma siyo sasa,

amezungumza namna ambavyo Chama cha Mapinduzi kimechoka na kinatakiwa kukataliwa. Mchangiaji mwingine akasimama akasema CCM mzigo huu kwao ni mzito sana, wasaidiwe. Sasa huyu anayejibu hoja hizo kwamba mzigo huu siyo mzito, unabebeka, mbona yeye mnaona ana shida?

Hebu tuwe watulivu Bungeni, tufuate utaratibu, tafadhali! *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Ulega endelea!

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka tuwaambie sisi bado ni Walimu katika Taifa hili, wao wakijua hivi, sisi tunajua hivi, hiyo ndiyo habari. Nataka nimwambie Mheshimiwa Waitara, rafiki yangu kwamba hiki ndiyo Chama cha Mapinduzi ambacho hata yeye kilimlea pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana tumeendelea kuuthibitishia Umma wa Watanzania kwamba hiki ndiyo Chama cha Mapinduzi. Tutaendelea kuwafunzeni siasa, kwa sababu hiyo ndiyo kazi yetu. Kesho tutakwenda kupitisha bajeti ya Wizara ya Maji. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi letu ni kutaka kuona kwamba katika bajeti hii ya Wizara ya Maji tozo ya shilingi 50 inaongezeka. Mheshimiwa ukikaa hapo katika kiti tuelekeze, Kamati yetu ya Bajeti ikakae na Serikali iongeze bajeti ile ya tozo ya shilingi 50 tukawahudumie Watanzania. Watanzania wa Mkuranga Mjini wanayo maji pale katika Mlima Kurungu, kisima cha mita 600, kuna maji ya *litres* nyingi yanapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu mmoja pale anaitwa Manyanyau, anawauzia Watanzania wa Mkuranga maji. Mtu mmoja amechimba yeye binafsi. Katika bajeti ya 2014/2015 zilitengwa hela hazikwenda, mwaka huu wa fedha wa 2015/2016 uliokwisha zilitengwa pesa hazikwenda. Sasa katika bajeti hii tunachotaka pesa ziende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali. Katika miradi ya visima kumi, mimi nimechimba visima kumi Mwanambaya, Mlamleni, Mkenezange, Kimanzichana, Mdimni, Ng'ole, Mbulani, Yavayava, nimechimba huko kote. Ninachosubiri sasa ni kuona miundombinu ya maji inaenea kwa wananchi wa Jimbo langu la Mkuranga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina wasiwasi kwa sababu nikimtazama jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, naamini kabisa kwamba maji yanakwenda kutatuka na Watanzania ile nia yetu tuliyowaambia ya kumshusha mama ndoo kichwani, tutaifanya hiyo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri mimi ni Mbunge mpambanaji. Mimi ni ...

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ulega naomba ukae. Taarifa.

T A A R I F A

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba katika bajeti ya 2016/2017, Bunge hili ilitengea Wizara ya Maji bajeti ya Shilingi bilioni mia tisa na kitu. Fedha pekee ambayo imetoka mpaka sasa ni shilingi bilioni 181 sawa na asilimia 19.8. Nisikilize, sawa na asilimia 19.8.

NAIBU SPIKA: Zungumza na kiti, usipoteze wakati kujibizana na Mbunge. Wewe zungumza, mimi ndiye ninayekusikiliza.

MHE. MARWA R. CHACHA: Kwa hiyo, nataka kumpa taarifa kwamba kama tulitenga shilingi bilioni mia tisa na kitu, imetoka shilingi bilioni 181, ni muujiza gani utatumia kutua wanawake ndoo ya maji? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Sasa mbona unamwuliza swali badala ya kumpa taarifa? Mheshimiwa Marwa, unampa taarifa, unamwuliza swali ili akujibu? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Abdallah Ulega, malizia muda wako.

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Naibu Spika, unilindie muda wangu. Nimesema hapa ya kwamba na sisi hicho alichokisema ndicho tunachokitaka. Hizi pesa zilizotengwa tuhakikishe zinakwenda kwa wananchi. Hizi pesa zikienda, tuna hakika azma yetu ya kumshusha mama ndoo kichwani itakamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hapa ya kwamba tuongeze tozo hiyo shilingi milioni 181, *ninety something millions* zote zimetoka katika tozo ya mafuta. Tukiongeza tuta-*double*, tutawasaidia Watanzania wakiwemo wa kwa rafiki yangu Mwalimu Marwa kule Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa umuhimu kabisa, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri anisaidie kunipelekea pesa zile. Ukurasa wa 163 ziko peza zinapelekwa kwenye Mji 63. Mmoja katika huo Mji uwe ni Mji wa Mkuranga. Sisi hatutaki pesa nyingi, tunataka kama shilingi milioni 800. Nami kwa kuwa ni Mbunge mpambanaji, nimeshajiongeza, nimezungumza na Ubalozi wa Kuwait, wameniambia yatoe maji kutoka mlima Kurungu yapeleke katika tenki. Jenga tenki, sisi tutakusaidia katika pesa za kufanya *distribution*. Unataka nini tena? Mungu akupe nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa heshima kubwa na taadhima niseme kwamba Mawaziri wetu chapeni kazi, sisi tuko pamoja na ninyi, kazi yenu mnayoifanya tunaiona na tunataka tuwahakikishie mkienda mkakaa Serikali na Kamati yetu, mkatukubalia, tukaenda kubadilisha katika Sheria ya Fedha, tukaongeza tozo ya shilingi 50, basi mambo yatanoga sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Lubeleje, dakika nne.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza na mimi nianze kuunga mkono suala la kuongeza bajeti ya Wizara ya Maji. Tatizo, Hazina hawatoi fedha zote za Miradi ya Maendeleo. Hilo ndiyo tatizo! La pili, Mji wa Mpwapwa, Mheshimiwa Waziri anaufahamu, amekaa Mkoa wa Dodoma miaka mingi akiwa Wizara ya Ujenzi. Vyanzo vya Maji vya Mji wa Mpwapwa tangu Ukoloni ni vile vile. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atume watafiti wakafanye utafiti wa vyanzo vingine vya maji ili kuongeza huduma ya maji katika Mji wa Mpwapwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni uchimbaji wa mabwawa katika vijiji. Waliahidi kuchimba mabwawa Vijiji vya Chunyu na Msagali ili kusaidia bonde la Msagali ambapo kuna kilimo cha umwagiliaji. La tatu, kuna visima vitatu vya maji vimechimbwa katika Kijiji cha Iyoma, Bumila pamoja na Mima. Tayari maji yamepatikana, lakini visima vile havijawekwa pampu, mabomba, matenki ya maji ili kusambaza maji. Naomba Wizara ya Maji na TAMISEMI wasaidiane pampu ziwekwe, maji yasambazwe ili wananchi waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mbunge mzoefu, naona umetumia muda mfupi kwa kutaja matatizo yote ya Jimbo lako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitayasoma kwenu majina ya baadhi ya Wachangiaji wetu wa mchana ambao ni Mheshimiwa Lea Komanya, Mheshimiwa Zaynabu Vulu, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Alex Gashaza, Mheshimiwa Edwin Sannda, Mheshimiwa Norman Sigalla King, Mheshimiwa Yosepher

Komba, Mheshimiwa Qambalo Willy, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Kiswaga Bonaventura, Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa Saada Mkuya, Mheshimiwa Hadija Aboud, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Suzana Mgonokulima, Mheshimiwa Gibson Blasius Ole-Meiseyeki, Mheshimiwa Salma Mwassa, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka na wengine tutaendelea kuwataja tutakapoanza uchangiaji mchana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lllisitishwa Mpaka saa 11.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lllirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wa Hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji. Tutaanza na Mheshimiwa Leah Komanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Zaynabu Vulu na Mheshimiwa Khadija Aboud ajiandae.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii jioni ya leo na mimi niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa namna wanavyojituma. Muda mwingi nimekuwa nikifuatilia na kuwaona wako *field*. Kwa maana hiyo, wamekuwa wakifuatilia kuangalia namna miradi ya maji inavyotekelezwa na kuona changamoto zinavyojitokeza katika utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na Mheshimiwa Chenge Mbunge wa Bariadi kuhusu kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Bariadi, nami niongeze mambo mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Bariadi ni Makao Makuu ya Mkoa wa Simiyu. Hivyo, ongezeko la watu limekuwa likiongezeka kila siku. Mji umekuwa ukipanuka kila siku na mradi huu umekuwa ni wa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba basi wakati wanakamilisha utekelezaji, waweze kufanya tathmini tena, waweze kuona ongezeko la watu na ongezeko la makaazi ya watu lilivyoongezeka ili waweze kuendelea kuupanua mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, naomba niungane na Mheshimiwa Chenge kuhusu Serikali katika utekelezaji, iweze kukumbuka yale makubaliano kwamba wakati wa utekelezaji wa huo mradi maji yatatengwa kwa ajili ya mifugo na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini soko la Bariadi lina mahitaji makubwa, lina mahitaji ya mboga za majani, matunda na kadhalika. Angalau wanawake waweze kujipatia sehemu ya kuuza, kwa kulima mboga mboga na mazao mengine ambayo watapata soko lao katika Mji wa Bariadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichangie upande wa programu ndogo ya maji na usafi wa mazingira. Programu hii imekuwa mkombozi kwa wananchi waishio vijijini. Programu hii ilianza mwaka 2006 hadi 2016, sasa yapata miaka kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa Mtendaji nimeshuhudia kwa namna gani imeweza kusaidia upatikanaji wa maji vijijini. Nitoe masikitiko yangu; ukiangalia Kifungu 4001 - Maji Vijijini; Kifungu kidogo cha 3280 ambayo ni Maji na Usafi wa Mazingira, mwaka wa fedha wa 2016/2017 zilitengwa shilingi bilioni 310.7, lakini mwaka huu wa fedha wa 2017/2018 zimepungua hadi shilingi bilioni 158.5, zimepungua kwa zaidi ya asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba fungu hili liongezewe fedha. Kwa kuwa bajeti kuu imeongezeka basi na kifungu hiki kiongezewe fedha. Kwa sababu ukiangalia sehemu kubwa ya nchi ni vijijini. Kwa mfano, nikiongelea mradi wa maji wa kutoka Ziwa Victoria kwa Mkoa wa Simiyu, kutoka Busega na maeneo yake. Mradi huu tu uta-cover vijiji 253. Ukiangalia vijiji ambavyo havitafikiwa na mradi viko zaidi ya asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, nikiangalia Jimbo la Maswa Magharibi, Jimbo zima hakuna kijiji kitakachofikiwa na mradi huu. Kwa hiyo, bado ipo changamoto ya uhitaji wa mradi wa maji vijijini, uongezewe bajeti. Kwa mfano, kuna Vijiji vya Kinamgulu, Mwabayanda, Ilamata na Mwandu. Vijiji hivi vipatiwe hata visima virefu kwa sababu kule mradi hautapitia hata kijiji kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niungane na Wabunge wengine kwamba sasa shilingi 100 ziweze kukatwa katika bei ya petroli na *diesel*. Ziongezwe shilingi 50/= kwa sababu hii itaongeza bajeti ya maji vijijini. Nashauri asilimia 70 ielekee vijijini kwa sababu huko kuna changamoto ya upatikanaji wa vyanzo vya maji. Nashauri pia awepo Wakala wa kusimamia fedha hizi zitakapopatikana ili ziweze kuratibiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kuhusu Bwawa la Mwanjolo lililopo Wilaya ya Meatu, Jimbo la Meatu. Mwaka 2016 mwezi wa Tano Mheshimiwa Waziri mwenyewe aliniahidi kwamba litafanyiwa tathmini ili liweze kukamilishwa, lakini hakuna utekelezaji ulioendelea. Bwawa hili lilianzishwa 2009, wananchi walitoa eneo wenyewe lakini sasa hivi limeanza kuwa kero kwao, limesababisha mmomonyoko wa udongo, wananchi waliacha kufanya shughuli zao kwa ajili ya mradi huo, lakini utekelezaji hakuna. Naomba sasa utekelezaji wake ukamilike. *(Makofi)*

Pia nichangie kuhusu Mamlaka ya Maji Mjini Mwanhuzi. Tunategemea maji kutoka Ziwa Victoria, lakini Wilaya ya Meatu itakuwa awamu ya pili. Ukiangalia bwawa lile, limejaa

matope, nina wasiwasi kama maji yatafika hata mwezi wa Kumi. Mji mdogo wa Mwandoya, chanzo kilichopo cha Igobe kimezidiwa. Nashauri basi uwepo mpango wa dharura ili kuweza kuinusuru Wilaya ya Meatu, Mji mdogo wa Mwandoya pamoja na maji mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maji haya pia yanaweza yakapatikana kutoka Mto Sem ambayo itasaidia kupitiwa Kijiji cha Mwangila, Sem, Isengwa, Manyahina na Busia, Busia ambako tenki lipo pale lakini wananchi wa pale hawapati maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie pia kuhusu dhana ya mradi wa vijiji kumi. Katika *WSDP 1* dhana ya mradi wa vijiji kumi niliona kila kijiji kilikuwa kikitafuta chanzo cha maji. Nashauri katika *WSDP 2* kama ni vijiji viwili au vitatu kinaweza kikapatikana chanzo kimoja, mtindo huo utumike ili kuweza kuokoa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC*; wakati wa ufuatiliaji miradi *RWSSP* katika ile *component* ya *sanitation* utekelezaji wake haufanyiki vizuri, kwa sababu unapofanyika mradi wa maji lazima kijengwe choo. Ukiangalia mradi wa maji wenye mabilioni umekamilika, lakini kipengele cha usafi na mazingira kujenga choo, yaani hela kidogo tu miradi hiyo haijatekelezwa. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Leah Komanya, muda wako umemalizika.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zaynabu Vulu, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Aboud na Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla King ajiandae.

MHE. ZAYNABU M. VULU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami jioni hii ya leo niweze kutoa mchango wangu katika hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waswahili wana msembo wao, wanasema hivi, "ng'ombe hashindwi na nunduye." Nina hakika pamoja na uchache wa pesa ambazo zimetolewa, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli haitashindwa kutekeleza miradi ya maji ambayo tunaitarajia katika maeneo yetu. Nawatoa hofu wenzangu, hilo walijue kwamba hakuna nundu yoyote ambayo ng'ombe imemshinda akasema mimi leo, siwezi kutembea, nundu hii imezidi ukubwa, nakaa chini. Hata siku moja! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumzia suala la maji, lazima tutazungumzia suala la fedha; na tunapozungumzia suala la fedha, maana yake tunataka miradi hii ifike kwa walengwa na kwa wakati. Tumeona baadhi ya maeneo yamepata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kitabu cha hotuba, mimi natoka Mkoa wa Pwani; Mwenyezi Mungu ametupa neema, tuna Mto Rufiji, tuna Mto Ruvu, tuna Mto Wami, lakini pamoja na uzuri wa wananchi wale kulinda vyanzo vya maji katika mito ile, kwenye kitabu hiki yametajwa mabomba yaliyowekwa kutoka Ruvu, mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu chini kwenda Dar es Salaam na baadhi ya maeneo kwa Wilaya ya Kibaha, Bagamoyo na Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kumtua ndoo mwanamke kichwani. Wanawake wa Pwani ndoo wao kwao siyo shida, maji siyo shida, lakini wao wanachotaka miundombinu ya maji kutoka kwenye mito iweze kufika kwenye maeneo yao. Unakuwa na mti wa matunda unatarajia mti ule ukupe kivuli na ule yale matunda, lakini kule baadhi ya maeneo wanatunza maji, wanajitahidi, lakini maji yale yakiwekwa mabomba moja kwa moja

yanakwenda Dar es Salaam. Siwaonei wivu ila nasi tunahitaji hayo maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, imetenga fedha, lakini bado fedha zile hazitoshelezi. Kwa mfano, Shule za Sekondari za Rufiji, wako karibu na Mto Rufiji, lakini shule zile kama Utete, Ngorongo, Kibiti na maeneo mengine hawana maji. Kuna visima vimechimbwa lakini tunaomba yawekwe mabomba ambayo yatafika kwenye shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama imeshindikana, kuna DAWASA na DAWASCO waweke miundombinu ya kuvuna maji ya mvua ya kuweka matenki. Maji yale siyo kwa watoto wa kike tu na akinamama wanaoyahitaji, hata watoto wa kiume wanahitaji maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado katika vyanzo hivyo hivyo vya maji, kuna wakulima wadogo na wakubwa. Naomba Wizara husika na Taasisi husika ziangalie utaratibu gani utatumika kuzuia zile dawa ambazo zinatumiwa kwenye kilimo zisiende zikaharibu afya katika yale maji, kwa sababu baadhi ya watu hawana mabomba, wanakunywa maji yale yale ambayo kwa sasa hivi kwa mfano mvua zimekuwa nyingi, yametiririka maeneo mengi, dawa nyingine ni sumu. Matokeo yake watu wanakunywa maji, maradhi ya aina mbalimbali yanapatikana. Mwishowe tunajuliza, kunani? Mbona magonjwa yamekuwa mengi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba uwekwe utaratibu, wakulima wadogo wadogo wapate elimu, wapewe namna ya kuweza kuhifadhi vyanzo vyao vya maji ili zile dawa wanazomwagilia kwenye mazao zisiweze kuharibu yale maji wanayoyatumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, katika huo Mradi wa Ruvu Juu ambao umeanzia Mlandizi; mto umeanzia Morogoro umekwenda Dar es Salaam; watu wanaokaa maeneo ya Kisarawe, kuna eneo la Kimaramisale, Kigogo, Mzenga na Kurui. Hao wote hawana maji safi na salama

yanayotoka kwenye mabomba ambapo wao ndiyo wanatunza vile vyanzo vya maji vya Mto Ruvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, pamoja na kutenga hizo fedha, lakini bado kuna utaratibu wa kufuatwa, tunaomba tusaidiane, tushirikiane nao, inapobidi hata kutoa elimu wananchi wa Kisarawe tutakuwa tayari hata kujitolea katika uchimbaji wa mitaro, watuletee mabomba tu. Sisi shida yetu ni mabomba na dawa za kuhakikisha maji yale hayataharibu afya za watu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona mvua hizi jinsi gani maji mengi yamepotea yamekwenda baharini na jinsi gani maji yameharibu kilimo chetu, lakini bado kungeweza kukafanywa utaratibu wa kuvuna maji ya mvua, elimu ikatolewa majumbani. Siyo mara ya kwanza nasema neno hili. Elimu ikatolewa mashuleni, pesa zikatengwa na Halmashauri zetu na Serikali Kuu ili kuhakikisha maji ya mvua yanavunwa, wananchi wanatumia maji ya mvua kwa wakati fulani, yakiisha wanajua sasa maji yamekwisha. Tunaachia maji yanakwenda bila kuwa na utaratibu wa kuyavuna. Kwa kweli hilo ni tatizo kubwa sana! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo cha umwagiliaji, tuongeze *scheme* za umwagiliaji katika maeneo yetu. Nchi yetu haiwezi kuwa na shida ya njaa; iwe mchele au sukari lakini *scheme* za umwagiliaji zikiongezwa tutakuwa tumevuka hatua kubwa sana *especially* akinamama wanaolima mpunga. Wale akinamama wakiwezesha, wakajengewa *scheme* nzuri za umwagiliaji, watalima mpunga wa kutosha, watalima miwa ya kutosha, tutaondokana na njaa, watu watajiwezesha, wataendeleza maendeleo katika nchi yetu. Naomba sana, hilo pia liangaliwe na Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la adha ya mfumo wa majitaka. Mji wa Dar es Salaam umekua vibaya sana, kwa maana ya kwamba kwanza ongezeko la watu limekuwa kubwa, miundombinu ya nyumba zile za kwetu tulizozaliwa nazo za vyumba sita banda la uani, hazipo! Kumejengwa

nyumba za ghorofa, lakini miundombinu ya kuchukulia maji machafu bado haijakaa sawa. Naomba sana hilo nalo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naelekea Kisiwa cha Mafia. Sote tunaifahamu Mafia. Mafia ni kisiwa ambacho kina visiwa vingine zaidi ya vitatu, lakini kuna kisiwa kimoja kinaitwa Jibondo. Kisiwa hicho kina watu zaidi ya 3,000, lakini watu wale hawayajui maji matamu mpaka wavune maji ya mvua kwa sababu wako juu ya jabali. Juhudi zimeanza kuoneshwa za kutaka kupelekewa maji; ni kilometa tisa tu kutoka kisiwa kikuu kwenda kwenye Kisiwa cha Jibondo na usafiri wake ni boti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali iangalie utaratibu wa kuwajengea miundombinu ya kuvuna maji ya mvua au kuweka utaratibu wa mabomba kutoka kisiwa kikuu cha Mafia kupita chini ya bahari ili waweze kupatiwa maji. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Muda wako umekwisha Mheshimiwa Vulu.

MHE. ZAYNABU M. VULU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Khadija Aboud atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla King. Mheshimiwa Martha Umbulla ajiandae.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Naibu Spika. Awali ya yote, nachukua nafasi hii kuwapongeza kwa dhati sana Mawaziri wetu wawili hawa; Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Maji kwa ufuatiliaji wao wa karibu na kutenda kazi kwao kwa umakini katika kusaidia Taifa letu kuondokana na shida ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni moja kati ya nchi tano za Afrika zenye wingi wa maji na maji yanayofaa

kwa matumizi ya binadamu. Tatizo letu labda ni kwenye changamoto za utaalim na rasilimali fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nijielekeze kwenye hii taasisi ya Wakala wa Uchimbaji Visima na Mabwawa (*DDCA*). Hii ni taasisi ya Serikali, unapokuja ushindani mara nyingi wanashindwa kwa sababu wana bei zao ambazo zimewekwa kwa kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoshauri ni kwamba Halmashauri zetu zitumie hii Mamlaka ya *DDCA* katika uchimbaji wa visima na mabwawa, kwa sababu hawa wana utaalim wa kutosha na pindi wamechimba kwa bahati mbaya maji hayakutoka, huwa hawadai malipo. Taasisi binafsi wanatuchimbia visima na mabwawa na baadaye wanadai malipo na maji huwa hayatoki. Nashauri iongezewe nguvu na vifaa vya kisasa kabisa ili zile kanda ambazo wameweka ziweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kwenye mfuko wa maji. Nami nakubaliana na waliotangulia kwamba ile shilingi 50 sasa iongezwe kwenye bei ya mafuta, ya kukatwa kwenye mafuta, ile tozo ili ifikie shilingi 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishauri Serikali iangalie zaidi kwenye simu. Kwenye simu kuna fedha nyingi sana, tuangalie vyanzo vingine vya kuongeza huu mfuko na tuangalie haya Mashirika ya Simu. Mashirika ya Simu yanaingiza fedha nyingi, lakini wanavyowekeza kwenye maendeleo ya wananchi ni kidogo. Katika huu Mfuko wa Maji nashauri kwamba vijijini wapewe asilimia kubwa ili kuimarisha miundombinu ya maji huko Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninaloliona hapa kwenye *VAT* ni katika madawa ya kutibu maji. Kwenye madawa ya kutibu maji hii *VAT* inapelekea sasa maji yawe bei kubwa ambapo kuna baadhi ya mamlaka wanashindwa kujiendesha hata kulipa *bill* za umeme. Naomba liangaliwe suala hilo kwenye madawa ya kutibu maji ili kumshushia mwananchi mzigo wa kulipa *bill* kubwa ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kwenye mikoa yetu, mkoa wa chini zaidi unaolipa bei ndogo ni 640 Moshi, na DAWASCO wanalipa 1,663 kwa *unit*, lakini bei hizi bado kwa Tanzania ukilinganisha na nchi za nje, mfano Denmark kwa *unit* ile ile inayolipwa Moshi shilingi 650 wao wanalipa shilingi 7,658. Ukienda nchi ndogo ambayo inalipa bei ndogo na ina utaaalam wa kutosha, ni China; inalipa shilingi 902, lakini Moshi tunalipa shilingi 640. Hili nataka kutoa mchangano mdogo zipo nchi mbalimbali na bei zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuchangia Chuo cha Maji. Chuo hiki kiongezewe nguvu na vifaa vya kutosha ili tupate wataalam wa maji huko vijijini na kwenye Manispaa zetu. Kikiimarishwa Chuo hiki tutapata wataalam watakaosaidia kwenye Mikoa yetu na Wilaya zetu; mfano kwenye kitengo cha *drill* cha uchimbaji wa Visima, hiki kipewe msukumo mkubwa wa wataalam ili tuweze kuwatumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niongezee kuchangia kwenye uvunaji wa maji ya mvua ambapo suala hili liwe ndiyo kauli mbiu yetu. Tuanze na sisi Wabunge humu ndani kwenye majumba yetu na maeneo yetu tujiwekee akiba ya maji ya mvua. Nafahamu kuna nchi baadhi ya maeneo maisha yao yote wanaishi kwa maji ya mvua tu, hawana maji mengine yanayotumia, kwa sababu wapo juu ya milima, milima ni jiwe hawapati maji, maji yao ni ya mvua tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni afya. Kwa kuwa maji ni afya tukiwekeza zaidi kwenye maji, tutapunguza hata ununuaji wa madawa ya kutibu binadamu na hasa watoto wadogo ambao wanaathirika sana na maradhi mbalimbali ya maambukizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tukipata maji tutamsaidia mwanamama au mwanamke kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi, atapata muda wa kutosha wa kulea familia, atapata muda wa kutosha wa kujajiri na kuinua kipato chake, badala ya kutumia muda mrefu kuhangaika kutafuta maji. Kwa hiyo, nashauri tuwekeze zaidi kwenye

Mfuko huu wa Maji ili tuweze kumsaidia mwananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea, naamini kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ikiongozwa na Rais wake, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu na Mawaziri wote, wana nia na dhamira ya dhati kabisa katika kuhakikisha wananchi wa Tanzania wanaondokana na shida ya maji na shida mbalimbali zinazotukabili. Mambo huenda kwa awamu, awamu baada ya awamu, hatua baada ya hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Wizara imejipanga vizuri katika kutekeleza mpango kazi wao waliotuandikia katika bajeti yao. Naishauri Serikali zile pesa walizoomba zitoke na zitoke kwa wakati...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Prof. Norman Sigalla King, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Umbulla na Mheshimiwa Mendrad Kigola ajiandae.

MHE. PROF. NORMAN A. S. KING: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kabla sijaendelea na mchango wangu, ni vizuri nitambue kama Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu kazi kubwa inayofanywa na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ya kuimarisha miundombinu Tanzania. Wananchi wa Makete wamenituma niseme ahsante kwa sababu anashughulika na barabara yao ya kutoka Njombe, Makete kwenda Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, pia nitumie nafasi hii kupongeza uteuzi wa rafiki yangu na mdogo wangu Profesa Kitila Mkumbo kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Maji. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa nasoma kitabu hiki, nimerudia chote mara mbili, mara tatu nilishindwa kuamini. Nimeshindwa kuelewa kama Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Maji na Naibu na Wasaidizi wake wanaifahamu Wilaya ya Makete vizuri na mchango wake wa maji kwenye nchi hii. Labda nimkumbushe Mheshimiwa Waziri. Wilaya ya Makete ndiyo inayotoa mto unaoelekea au kumwaga maji Mbarali katika mashamba ya Kapunga yanayolima mpunga pamoja na bonde la Usangu. Ni mto ambao chanzo chake kiko Wilaya ya Makete, Tarafa ya Matamba na Ikuwo. Ni maji hayo hayo yanayokwenda kwenye Hifadhi ya Ruaha, yanatoka Makete.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maji hayo hayo yana kwenda kwenye bwawa la Mtera. Umeme wa Tanzania unategemea Makete. Ni maji hayo hayo yanabadilishwa jina lake yanaitwa Ruaha Mkuu ambapo eneo la Ruaha Mbuyuni wanalima vitunguu na nyanya, yanatoka Makete. Ni maji hayo hayo yanayotoka Makete yanayokwenda Kilombero na kuzalisha miwa, sukari wanayotumia Watanzania, yanatoka Makete.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ni maji hayo hayo yanayotoka Makete yanakwenda Rufiji na kubalishwa jina na kuitwa Mto Rufiji. Pamoja na kazi kubwa ya wananchi wa Makete kuachia eneo la kilometa za mraba 465.4 ili angalau Watanzania milioni 8.9 waweze kupata na kutumia maji kutoka Makete, lakini Makete yenyewe haina maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilihudhuria kikao cha Makamu wa Rais, pale Iringa ilikuwa bayana kwamba maji yanayotoka Makete yanNufaisha Watanzania milioni 8.9, lakini Tarafa ya Matamba na Ikuwo haina maji. Mheshimiwa Waziri ana ugomvi gani na wananchi wa Makete? Wanafanya kosa kuhama kilometa 465.4 ili waachie vyanzo vya maji ili

Watanzania wapone, lakini wao wasipewe maji. Je, ni kosa lao wananchi hawa kuwahurumia Watanzania wengine? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo unachokiona chote kwenye bonde hili ninalolisema mpaka Rufiji, maji yake yanatoka Makete. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hebu awe na jicho la huruma. Ni vizuri bajeti yake itambue ya kwamba wananchi wa Makete na hasa Tarafa ya Matamba na lkuwo wanahitaji maji na ndiyo zawadi pekee atakayowapa. Haiwezekani wao waachie eneo kwa ajili ya maji ya Watanzania wengine, lakini wao wenyewe wasipewe maji. Hivi ni dhambi gani wamefanya wananchi hawa wa Makete? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarafa ya Bulongwa, ukiongelea Kata ya Kipagalo, Luhumbu na Bulongwa yenyewe, nenda Kata ya Vijiji vya Tanala, Mang'oto, Mbarache, Kigala na Mfumbi maji hakuna, lakini wameachia eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, unafahamu kilometa hizi ninazozisema sehemu nyingine ni Jimbo zima. Kilometa za mraba 465 Makete halikaliwi na mtu wameacha ili Tanzania ipate kuneemeka, Tanzania iwe na maji mengi. Juzi wakati Waziri Mkuu alipofanya ziara pale Makete, aliambiwa kwamba tatizo, kuna mradi wa maji ambao Wizara ya Maji ilisimamia pale na ikaufanya vibaya mradi ule. Kwa hiyo, umepelekea Vijiji vya Kinyika, Matamba, Mlondwe na Itundu kukosa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni mradi uliosimamiwa na Wizara siyo wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete. Waziri Mkuu aliahidi wananchi wa Makete ya kwamba atamtuma Waziri mwenye dhamana aende autembelee mradi ule ili asahihishe makosa ambao Wizara yake ilifanya. Mpaka hivi ninavyoongea, rafiki yangu, kaka yangu Mheshimiwa *Engineer* Lwenge, Mheshimiwa Waziri hajafika Makete. Naamini ujasiri wake, natambua uwezo wake, najua ataitembelea Makete.

Naomba sana, awakumbuke wananchi wa Makete kwa sababu ya kazi yao nzuri ya kutunza vyanzo vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unafahamu, leo hii tunapoongelea vyanzo vya maji, ni vigumu sana kupata eneo ambalo linazalisha maji kwa wingi kama Makete, sijui kama lipo. Ndiyo maana marefu ya mto wote huu angalau leo Watanzania mnajua sasa kwamba kimsingi mto huo asili yake ni Makete.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja za wenzangu ambao wanasisitiza umuhimu wa bajeti hii kuongezwa na hasa shilingi 50 inayosemwa kwa lita ya mafuta, ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vitu vingine vyote siyo watu wote wanavitaka, lakini unapoongelea maji ni kila mtu. Ndiyo maana tukaja na sentensi inayosema, “maji ni uhai” kwa sababu bila maji, hakuna uhai. Huwezi kula bila maji, huwezi kufanya chochote bila maji, ndiyo maana ni muhimu sana bajeti ya maji ipate kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu Mheshimiwa Waziri atakaposimama atalijulisha Bunge Tukufu kwamba hitimisho lake kwenye bajeti yake anaonesha shilingi bilioni 672, lakini ni vizuri asome pia ukurasa wa 173 katika hotuba yake, unaoeleza fedha za kutoka India dola milioni 103 ambazo ni sawa na trilioni 1.1 kwamba: Je, zimo kwenye bajeti au la! Kama zimo, basi bajeti ya maji itakuwa ni shilingi trilioni 1.762 na siyo bilioni 672

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakaposimama ni vizuri kutoa ufafanuzi ili kulifanya Bunge lielewe kwa usahihi kwamba shilingi milioni 503.04 iliyopo ukurasa wa 173 kwenye hotuba yake, je, imejumuishwa kwenye bajeti au la.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

MHE. PROF. NORMAN ADAMSON SIGALLA KING: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Martha Umbulla, atafuatiwa na Mheshimiwa Mendrad Kigola na Mheshimiwa Alex Gashaza ajiandae.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa nami nitoe mchango wangu kwenye sekta hii ya maji. Nami nachukua nafasi hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, *Engineer* Lwenge na Naibu wake, kwa kweli wanafanya kazi kubwa kwa ajili ya Watanzania. Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni; wametembelea sana Mkoa wetu wa Manyara, wameona changamoto mbalimbali; pale palipowezekana, walitua na kule ambako hapawezekani tunaendelea kuwaomba watusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna asiyekubali kwamba changamoto kubwa katika nchi yetu ni uhaba wa maji. Kilio cha Waheshimiwa Wabunge hakijaanza leo, ni miaka mingi huko nyuma na hadi sasa tumewasikia Waheshimiwa Wabunge. Kama kungekuwa na mahali pana nafuu, tungeelezwa humu ndani. Bado changamoto inayokabili Taifa letu ni uhaba wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachosikitisha ni kuona kwamba kila mtu anaeleza kwa ufasaha, anajua changamoto ni uhaba wa maji. Penginepo wanaeleza pia ni namna gani tuondokane na tatizo hili, lakini bado hatuna majawabu. Tuna *program* nyingi za maji, tuna mikakati, tuna mipango kadhaa, lakini hakuna ambacho tunaweza kutamba nacho leo kusema kwamba mipango hii na *program* hizi na mikakati hii imeweza kuleta unafuu wa uhaba wa maji kwa kaya pengine hata laki mbili kwa mahali fulani. Hiyo hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tuendelee kuweka mikakati madhubuti ambayo ni halisia. Tufanye nini ili kuondokana na uhaba wa maji? Tuache kulia sana hapa, wapanga bajeti ni sisi wenyewe, mipango yote tunatengeneza wenyewe; kwa hiyo, tukiendelea kulia hapa kwa miaka mingi, nadhani hatuna majawabu. Ni muda muafaka sasa tuweze kupata majawabu, nini kifanyike ili tuweze kuondokana na tatizo hili la uhaba wa maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kuona sura ya umaskini, tembelea kijiji ambacho hakuna hata tone la maji, halafu ukitoka pale tembelea na kijiji ambacho kina maji. Ukitoka hapo utakubaliana nami kwamba kusema kweli maji ni uhai, maji huondoa umaskini, maji huondoa maradhi na maji ni kila kitu; maji ni viwanda na uchumi wa kati katika nchi yetu. Kama hivyo ndivyo kwamba maji ni kila kitu, iweje sasa bajeti ya maji ya mwaka 2016 ambayo ilipangwa shilingi bilioni 900 ikatolewa shilingi bilioni 180 tu kwa ajili ya Sekta ya Maji, hapo ndiyo unakuja mchanganyiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza nikawa nimesahau kidogo takwimu naomba radhi, lakini ukweli ni kwamba fedha zinayotolewa kwa ajili ya miradi ya maji ni kidogo sana kulingana na bajeti inayowekwa. Kwa ajili hiyo, naomba tupange bajeti yenye uhalisia, tusiwadanganye wananchi kusoma matrillioni ya pesa hapa, lakini fedha zinazotolewa kwa ajili ya miradi muhimu sana kama ya maji ni kidogo kama ambavyo tunaiona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza sana kuhusu mikakati ya kuondokana na uhaba wa maji, lakini tunajua kwamba nchi yetu ni tajiri sana, tumejaaliwa na Mwenyezi Mungu, tuna mito, tuna maziwa tuna wataalam waliobobea, nadhani tunakosa ubunifu. Tuanze kubuni ni namna gani tunaondokana na tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri ambao nilishautoa hata kwenye michango yangu ya huko nyuma, kwamba, tuangalie sekta ambazo tumeshafanya vizuri kiasi fulani kama Sekta ya Barabara, tu *pull resources* za sekta hiyo

pamoja na nyingine ili tuelekeze kwenye miradi ya maji. Tukimaliza kuondokana na tatizo hilo, tunaweza tukarudi kuendelea na sekta zetu za barabara na nyinginezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili ni jambo muhimu ambalo naona pengine litakuwa ni suluhisho pamoja na mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge wameweza kuzungumzia. Ni lazima tuwe wabunifu ili tuweze kufikia mahali tuseme sasa basi tumechoka na kulia kilio hiki cha uhaba wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukikosa chakula unaweza ukaagiza hata kwa jirani yako ukaomba msaada, ama ukaagiza hata nje ama nchi jirani, lakini kwa vyovyote vile huwezi kuomba msaada wa kupewa maji kutoka nje ama kwa nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni sisi wenyewe, majawabu tunayo wenyewe tuone ni namna gani tuweze sasa kukaa chini na kuona tunasaidiaje katika kuondoa changamoto hii ya maji inayotukabili. Kama hivyo ndivyo, iweje bajeti ya mwaka 2016 sasa iwe imeshuka mwaka huu wakati bado tunasema kwamba changamoto yetu kubwa ni uhaba wa maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na wenzangu wote kusema kwamba, tozo ambayo tunaweka kwenye *petrol* na *diesel* iweze kuongezwa hadi sh.100/= ili na yenyewe isukume. Siyo hiyo tu, nilikuwa nashauri kwamba tuangalie hata maeneo mengine kama *EWURA*, *TANESCO* na kwingineko tujaribu kuona ni namna gani tunajizatiti, tufanye maamuzi magumu kuweza kuondokana na tatizo la uhaba wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza sana kuhusu changamoto hii, hebu sasa Wizara iweze kukosa usingizi kuhakikisha kwamba inafanya ubunifu kuondokana na tatizo hili la uhaba wa maji. Tukiacha bajeti ya kushuka, Hazina inathubutuje kuchelewesha fedha zinazokwenda kwenye miradi ya maji? Kuchelewesha fedha za miradi ni tatizo sugu

la Hazina. Tunataka pia wakati Wizara inafanya majumuisho, ituambie kuna tatizo gani Hazina kuchelewesha fedha za miradi, ikiwepo na miradi ya maji kama ambavyo tunaiona? Tunaomba hili tatizo sugu nalo liweze kuondoka, tusiwachanganye wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mipango yetu na *programs* za maji, nashauri tuweke *benchmarks* ili tuweze kupima mipango yetu tunayotengeneza, tuweze kujua kwamba mwaka 2016 tulipanga mipango hii na sasa hii ndiyo *benchmark*, tumefikia hatua hii, lakini kusema kwamba tunajizatiti ama tunaendelea kupanga mipango ambayo haitekelezeki, ama inatekelezwa lakini haina majawabu, nadhani hatutafikia muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nioanishe uhaba wa maji na maisha ya wanawake wa Tanzania hasa wa vijijini. Kwa bahati mbaya teknolojia ya kisasa haijaweza kumsaidia mwanamke aondokane na tatizo la kubeba maji kichwani huko vijijini. Siyo hilo tu, usafiri wa mwanamke wa kijijini kwa bahati mbaya, teknolojia haijamsadia, bado anatembea kwa miguu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuweze kuwasaidia wanawake hawa wa vijijini hasa wanawake wa jamii ya kifugaji. Wanawake hawa wanaotafuta maji, siyo maji tu kwa ajili ya binadamu, ni pamoja na mifugo.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Umbulla, muda wako umekwisha.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mendrad Kigola, atafuatiwa na Mheshimiwa Alex Gashaza na Mheshimiwa Edwin Sannda ajiandae.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie kwenye Wizara hii muhimu ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Wizara ni ya muhimu sana kwa sababu inagusa uhai wa binadamu. Binadamu ili aweze kutembea, miili yetu lazima itumie maji. Kwa hiyo, tukitamka maji ni muhimu kwa kila mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitabu cha Mheshimiwa Waziri nimekisoma vizuri sana. Tunaposema maji, kuna wengine wanasema kwamba maji yanaenda kumkomboa mama. Maji tunaenda kukomboa binadamu wote pamoja na wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, akinamama wakiamba asubuhi saa 12.00 wanamwacha baba nyumbani na familia, wanatembea kilometa nne mpaka tano wanatafuta maji; na baba pale nyumbani anahangaika; kuna akinamama wengine wananyonyesha, anahangaika kuangalia watoto pale nyumbani. Ni shida kubwa! Kuna sehemu nyingine watu wanachota maji kilometa karibu nne kwa kufuata maji mbali na punda. Wakitoka saa 12.00 wanarudi saa 4.00 mpaka saa 5.00 asubuhi. Kwa hiyo, suala la maji ni suala la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusoma kitabu hiki, mimi kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini, kwa kweli wakati nasoma kitabu hiki nimesikitika sana. Mwaka 2016/2017, kwenye bajeti Wilaya yetu ya Mufindi tulipangiwa shilingi bilioni 2.5 na bajeti ile ya mwaka 2016 imerudi kama ilivyo. Mwaka 2016 hatukupata hela yoyote. Kwa hiyo, imerudi ile ile shilingi bilioni 2.5. Kwa Wilaya nzima shilingi bilioni 2.5 tukagawanya Majimbo mawili, ni sawasawa na sifuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini kuna miradi ambayo ina miaka mitano, mpaka leo tunavyoongea haijakwisha. Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri niliwaambia kwamba kwenye Jimbo langu tatizo kubwa, Serikali ilijitahidi sana kujenga matenki ya maji, miaka ya nyuma kama miaka kumi iliyopita. Yale

matenki ya maji, yanahitaji ukarabati. Bahati Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri waliniahidi, wakasema watatafuta fedha. Sasa leo nimesoma kwenye bajeti humu, bajeti hii hawajatenga kukarabati miundombinu ya maji katika Jimbo la Mufindi Kusini. Kwa kweli hii ni hatari sana. Kama tutakuwa tunakuja hapa tunatoa ahadi kwa wananchi kwamba miundombinu tutakarabati, lakini tusifanye hivyo, ni hatari.

Mheshimiwa Naibu spika, wanafunzi kwenye Shule za Sekondari na Msingi wanapata shida sana, hakuna maji. Watoto wanatoka na vidumu kutoka nyumbani wanapeleka maji shuleni. Badala ya kwenda kusoma, wanaanza kufuata masuala ya maji. Ukienda kwenye zahanati, kwenye hospitali hata Hospitali ya Mafinga pale mjini, maji ni shida kubwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri, matenki yale ambayo aliahidi kwamba atakarabati, wananchi waanze kupata maji, naomba hiyo kazi aifanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitaje matenki ambayo yalitengenezwa na Serikali na miundombinu yake imeharibika. Ukienda Nyororo kuna tenki moja, Igowole kuna tenki la pili, Ihomasa, Mkangwe, Ikangamwani, Kibao, Sawala, Kasanga, Ihawaga, Nanyigwe; sehemu hizi zote matenki yapo lakini maji hamna, miundombinu imeharibika. Kama kweli tuko *serious* na wananchi tumewaahidi, naomba matenki yale yaweze kutengenezwa wananchi waanze kutumia maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijiji vya Mufindi Kusini havina maji kabisa. Bahati nzuri mimi Mbunge nimechimba visima pale, lakini Serikali kwenye *gravity system* bado haijapeleka. Kwa mfano, ukienda Mninga pale hakuna maji, Mkalala, Ihawaga, Luhunga, Lugema, Kiyowela, Idete, Iholo, Itika, Kitasengwa, Itulituli, Kisasa, Ibatu, Mtambuka, hakuna maji vijiji hivi. Halafu napewa shilingi bilioni mbili ambayo ni ya mradi mmoja wa mwaka 2016 au mradi wa kijiji wa Kata ya Mtwanga. Mwaka huu sijapewa hela yoyote. Sasa mimi Mbunge ninayewakilisha wananchi nakuja hapa, naona sijapewa hela yoyote. Hii inakuwaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Mheshimiwa Waziri nimeshamwambia, kwamba kwenye Jimbo langu hujapanga bajeti yoyote na ameniagiza, amesema nimwambie Mkurugenzi waandike *proposal* waweze kuleta. Ninavyoongea hivi, kama Mkurugenzi ananisikia, kesho aandike *proposal* hiyo, kesho kutwa nimpe afanye *amendment*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sehemu nyingine ukiangalia kwenye kitabu hiki, unaweza ukaona kuna maeneo matano, Wilaya moja imepewa fedha shilingi bilioni 200; mimi napewa shilingi shilingi bilioni mbili. Kweli hiyo inakuja hiyo? Yaani Wilaya moja ukijumlisha hela za wafadhili, ukijumlisha hela za ndani, ukijumlisha na hela nyingine sijui miradi maalum wanapewa wilaya moja shilingi bilioni 200, sisi kule hatujapewa hela. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli tunakuja ndani ya Bunge, tunataka usawa tujadili vizuri, tunaomba miradi ya maji ifuate utaratibu. Hilo litakuwa ni suala la msingi sana, kila wilaya iweze kupewa fedha. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais; alisema kwamba ikifika mwaka 2020 masuala ya maji, asilimia kubwa atakuwa ametatua. Sasa atatatuaje kama wilaya moja ndiyo inapewa fedha nyingi, Wilaya nyingine hazipewi? Hii italeta tatizo kubwa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, katika kugawa fedha afanye *analysis* vizuri, agawe sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tulisema kila kijiji kitapewa shilingi milioni 50, kwa nini asiseme kila kijiji kitapewa shilingi milioni 200 kwa ajili ya kutatua masuala ya maji ili tuwe sawa? Kuna watu wengine hapa wanashingilia wamepewa hela nyingi sana; anafika hapa anaanza kushangilia. Mimi nitashangiliaje kama Wilaya yangu hatujapewa fedha? Mimi nitakuwa Mbunge mwenye akili kweli! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja lakini lazima nitamletea Mheshimiwa Waziri *proposal* ili Jimbo langu la Mufindi Kusini liweze kupewa maji. Kama halitapewa maji,

basi nitamwandikia Mheshimiwa Rais, nimwambie mimi hapa nitafanyeje? Sasa katika kuongoza, nitafanyeje mikutano pale kama hakuna maji? Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kusema kwamba Serikali yetu inafanya vibaya. Serikali ina malengo mazuri safi kabisa, lakini Watendaji wanatuangusha katika kugawa mahesabu. Kama wanashindwa, sisi Wabunge tugawe mahesabu kwa kila Wilaya. Haiwezekani wilaya moja ikapewa shilingi bilioni 600, shilingi bilioni 200, shilingi bilioni 100 na wengine wanapewa shilingi bilioni moja au shilingi milioni 500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Mafinga nimesoma wamepewa shilingi milioni 500. Sasa mwingine anapewa shilingi bilioni 200, hii haiwezekani jamani! Hata kama kiasi ni kidogo, tunajua sawa ni ndogo, tugawane sawa basi! Tunajua kama fedha ni ndogo, hiyo ni *collection ya revenue* kwa mwaka, hatuwezi kupinga, lakini kile tunachokipata tugawanye sawa kila mmoja aridhike. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa Kigola, ahsante sana.

Mheshimiwa Alex Gashaza atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Sannda na Mheshimiwa Yosepher Komba ajiandae.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba maji ni tatizo nchi nzima kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kuchangia wameeleza. Natambua jitihada za Serikali katika kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji kama mahitaji muhimu.

Maji ni kila kitu. Bila kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto za maji katika maeneo yetu, hata baadhi ya mipango mingine ya maendeleo kwa ajili ya nchi yetu yanaweza yakakwama. Maji ni viwanda, maji ni kilimo, maji ni afya, maji ni mazingira na maji ni uhai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana mkono na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kusema kwamba bajeti hii ya Wizara iweze kuongezewa fedha angalau kuweza kufikia bajeti ya mwaka 2016. Ni kwa nini nasema hivi? Kwa bajeti ya mwaka unaoishia sasa 2016/2017, katika Jimbo langu la Ngara nilikuwa nimetengewa shilingi 2,000,045,000 kwa ajili ya mradi wa maji, kukamilisha miradi ambayo ilikuwa ikiendelea na ikiwezekana kuanzisha miradi mipya. Mpaka dakika hii ninavyoongea ni shilingi milioni zisizozidi 400 ambazo zimeshapelekwa kati ya shilingi 2,000,045,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye umwagiliaji zilikuwa zimetengwa shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu katika mabonde mawili; Bonde la Mgozi na Bonde la Mhongo, lakini mpaka dakika hii hakuna hata senti moja ambayo imekwenda kule. Kwa hiyo, naishauri Serikali kwamba ni vizuri tukaangalia kuongeza bajeti hii ili tuweze kuangalia mahali ambapo bado panahitaji kupata huduma hii ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji ukurasa wa 122, amekiri kupungua kwa rasilimali za maji katika maeneo mbalimbali; lakini ameendelea akakiri kwamba yapo maeneo ambayo yana maji mengi na maeneo mengine hayana maji. Nashauri kwamba kama kuna maeneo ambayo yana rasilimali kubwa ya maji, basi maeneo haya yaweze kupewa kipaumbele kwa ajili ya kujenga miundombinu ya maji na vyanzo vya maji viimarishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba usambazi wa maji ni endelevu kulingana na ongezeko la idadi ya watu, lakini tukishajenga katika maeneo yale ambayo tunaamini kwamba vyanzo ni *reliable*, maji ni mengi halafu tukaendelea

kusambaza taratibu kwa kadri tunavyopata fedha, tutaweza ku--cover maeneo mengi ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkutano wa sita, niliuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji nikasema Jimbo la Ngara ni Jimbo ambalo lina vyanzo vingi vya maji. Tuna mito miwili, Mto kagera na Ruvuvu ambayo halkauki; ni maji mengi ambayo yakitumiwa vizuri yanaweza yakasambazwa kwenye mikoa mitatu, Mkoa wa Kagera, Geita na Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na jiografia ya Jimbo la Ngara kwamba liko kwenye mwinuko wa juu, *actual* ni kati ya mita 1,200 mpaka 1,800, kiasi kwamba ukiweza kuweka chanzo cha maji pale ukajenga matenki makubwa, tuna mlima mrefu kuliko milima yote Mkoa wa Kagera. Unaweza ukapeleka maji kutoka pale kwa mtiririko kwa gharama nafuu ukasambaza katika mikoa hiyo mitatu niliyoitaja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme na naendelea kusisitiza Mheshimiwa Waziri kwamba ajisumbue na siyo kujisumbua ni kutekeleza wajibu wake kwamba tunapomaliza Bunge hili, hebu atume *team* yake ya wataalam kufika Jimbo la Ngara waone vyanzo vilivyopo. Bahati nzuri Naibu Waziri, TAMISEMI tarehe 30, Desemba mwaka 2016 alifika katika Jimbo la Ngara akaona, nikamwonesha mito ile, nikamwonesha mlima huo, nikasema ukitumia vyanzo hivi tutatatua tatizo kubwa la maji katika eneo kubwa la nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado yapo maeneo ambayo mengine hayahitaji pesa nyingi, lakini unakuta ni kero ya muda mrefu. Kwa mfano, kuna eneo la K9 ambalo nimekuwa nikiomba maji kwa muda mrefu, linahitaji shilingi milioni 26 tu kwa ajili ya mtambo wa kusukuma maji na

kusaidia jamii ya wananchi waliopo pale. Kuna taasisi mbalimbali; Sekondari mbili, Kambi ya Jeshi na wananchi walioko pale. Ikipatikana shilingi milioni 26 mtambo unapatikana, unasukuma maji, kero inaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa umwagiliaji, hakuna namna ambavyo tunaweza tukaongeza uzalishaji kama tusipoweza kuboresha *scheme* za umwagiliaji. Jimbo la Ngara ni jimbo ambalo lina utajiri wa mabonde oevu na tayari kuna mabonde matano ambayo yaliainishwa na Serikali kwa ajili ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, bonde moja lilishaanza *scheme* ya umwagiliaji; Bonde la Bigombo tangu mwaka 2012. Mradi huu ulikuwa ukamilike 2013, lakini mpaka sasa hivi mradi ule haujakamilika na inaonekana hata Wizara imesahau kabisa kwamba mradi huo upo kwa sababu Mkoa wa Kagera ni wilaya mbili tu; ya Muleba na Karagwe ambayo imeonesha kutengewa fedha kwa ajili ya kukamilisha miradi inayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Jimbo la Ngara kwenye mradi huu wa Bigombo hakuna hata senti iliyotengwa na wala haiko hata kwenye *program*, maana yake ilikuwa imesahaulika. Kwa hiyo, naiomba Wizara kwa sababu tayari tumeshawekeza pesa shilingi milioni 715 zilitengwa kwa ajili ya mradi huu na karibu zote zimesha-*exhaust* lakini bado mradi haujakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Wizara husika iweze kufuatilia na kuona ni namna gani ambavyo inaweza ikakamilisha mradi huu kwa sababu tumesha-*dump* pesa pale na wananchi wanahitaji kunufaika na mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara na nimeanza na Mhandisi wa Maji wa Wilaya, kwamba lazima

tutengeneze *profile* za maji katika maeneo yetu. Najua kwamba jiografia inatofautiana hata kwenye Halmashauri zetu kati ya kijiji na kijiji, kati ya kata na kata. Kuna mahali unaweza ukatumia *scheme* ya maji ya mtiririko, kuna mahali huwezi, inabidi utumie visima.

Mheshimiwa Naibu Spika,asa tukitengeneza *profile* hizi, tukajua kwamba mahitaji ni nini kwenye kila kijiji na kata, uwezekano wa *scheme* ipi itumike katika maeneo hayo, tukawa na *profile* hii na pengine tukawa hata na makadirio *roughly* itaweza kutusaidia katika kupanga na kuonesha vipaumbele ili kusudi kile kinachowezekana, kama ni kijiji kina *scheme* ya kisima, shilingi milioni 20 au 30 zinatoshwa, basi hilo lifanyike na ndipo hapo ambapo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Muda wako umekwisha.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naunga mkono hoja, lakini naomba kwamba suala la kuongeza bajeti ya Wizara hii lizingatiwe. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Edwin Sannda, atafuatiwa na Mheshimiwa Yosepher Komba ambaye muda wake atagawana na Mheshimiwa Aida Khenani, halafu Mheshimiwa Qambalo Willy ajiandae.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza kabisa naipongeza Wizara kwa kazi nzuri ambayo imeendelea kufanya chini ya Waziri wetu na timu yake yote. Kabla sijachangia yale ambayo ningependa kusema, ningependa nitoe maoni yangu ya ujumla kuhusiana na bajeti ya Wizara hii ambayo imewasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, sijui niombe ombi la tofauti kidogo? Tumwombe *Chief Whip* wetu anipatie dakika 15 kwa sababu, ninayo mengi hapa, ikiwezekana hiyo tukatengua Kanuni, itakuwa nzuri zaidi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza maoni yangu ya jumla, pamoja na mawazo ya wengi ambayo yamekuwepo kuhusiana na kuongeza bajeti hii, mimi nimejaribu kuitafakari. Mwaka 2015/2016, tulikuwa na karibu shilingi bilioni 130 halafu mwaka 2016/2017 tukaruka sana mpaka shilingi bilioni 900 mwaka huu 2017/2018 tumekwenda chini kidogo mpaka shilingi bilioni 600. Wengi wamedhani kwamba ni vizuri tungeweza kuongeza bajeti ifikie angalau lengo la mwaka jana. Mimi nafikiri tulipofanya maoteo ya shilingi bilioni 900 labda hatukuwa sahihi sana ndiyo maana hawa wenzetu wakarudi nyuma wakawa *realistic* zaidi na kurudi kwenye shilingi bilioni 600. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wenyewe Wabunge, tumekuwa tukisimama hapa kila siku tunasema bajeti za Serikali zije za uhalisia, leo wamerudi nyuma wamekuwa halisia, tunawaambia warudi kule. Nataka niwaambie, katika shilingi bilioni 900 *plus*, utekelezaji mpaka Machi ni shilingi milioni 181, kweli! Asilimia 19.8 halafu tunataka turudi kule? Tunawaambia Watanzania ukweli au tunataka kuwafurahisha? Kwa maoni yangu ya jumla, hapa ambapo mmepaweka ni sawa. Hatuna sababu ya kurudi kwenda kuibadilisha bajeti kwa sababu tunataka kuwa wahalisia zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye maoni yangu. Kwanza kabisa napenda niungane na wenzangu wengi ambao wamechangia kwamba tupate lile ongezeko la shilingi 50 kwenye Mfuko wa Maji ili tufikie shilingi 100, nina uhakika Mfuko wetu wa Maji utatusaidia sana. Kwa hiyo, nami naungana na wenzangu katika hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niongezee tena zaidi, pamoja na kwamba tunafikiria tuongeze shilingi 50 kwenye mafuta lakini hata kwenye masuala ya vinywaji tunaweza

kufanya hivyo. Kuna mmoja wetu hapa alizungumza hili, tukizungumzia vinywaji na bidhaa nyingine ambazo tunatumia kama sigara na kadhalika tukaongeza pale kasenti, tutapata hela ya kwenda kwenye maji, maji mijini na vijijini yatapatikana. Katika kilio kikubwa kuliko vilio vyote, nafikiri hii Wizara ndiyo kilio kikubwa kwetu Wabunge wote. Kwa hiyo, napenda sana niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine kuhusu Mfuko wa Maji tuutunishe zaidi uweze kusaidia kwenye suala hili la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala zima la umwagiliaji. Nimeangalia ile Tume ya Umwagiliaji ina shilingi bilioni 20 sijui kati ya hiyo shilingi bilioni 600. Tumesema tunataka Tanzania inayoelekea kwenye uchumi wa kati. Uchumi wa kati kwa mpango wetu utakwenda kufanikishwa na uchumi wa viwanda lakini uchumi wa viwanda unataka mapinduzi ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi mapinduzi ya kilimo tutayaleta kwa kutegemea mvua au kwa hii shilingi bilioni 20 iliyotengwa, kweli? Mapinduzi ya kilimo yatafanikiwa pale tu tutakapoamua kuwekeza zaidi kwenye kilimo cha umwagiliaji. Viwanda vyetu vitawezeshwa na malighafi za ndani. Malighafi za ndani zinalimwa hapa na ili zilimwe sawasawa ni lazima kilimo kiwe kilimo chenye tija, endelevu, cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya umwagiliaji kwa kweli hairidhishi. Hata ile Tume ya Umwagiliaji bajeti iliyotengewa Mheshimiwa Waziri pale hatupo sawa sana. Pale nitapenda sana kutofautiana na ninyi. Niombe anaporudi atuambie, maana shilingi bilioni 20 kwa shilingi bilioni 600 unazungumzia chini ya 10% ya bajeti yote inaenda kwenye *infrastructure* na mambo mengine yote kuhusiana na umwagiliaji, kweli hapa ndiyo tutapata mapinduzi ya kilimo? Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze kidogo pia kuhusiana na suala zima la Jimboni kwangu. Suala la umwagiliaji tuliwahi kuwasilisha maombi muda mrefu kidogo

ya Bwawa moja la Umwagiliaji la Mongoroma ambalo lina ekari 3,000. Ekari 3,000 kama tungeweza kuwekeza, hela iliyohitajika ni kama shilingi bilioni mbili, hela iliyohitajika ingeweza kuwekwa pale ni watu takribani 12,000 wanguenufaika. Hebu niambie *nimultiplication effect* ya kiasi gani, *ripple effect* ya kiasi gani wananchi wangepata kiuchumi kutokana na kilimo cha umwagiliaji chenye uhakika kwa staili hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri na timu yake, naomba hii miradi ya umwagiliaji tuiangalie sana. Mabwawa kama Mongoroma yangeweza kutusaidia kweli. Nimeona kwenye ripoti ziko sehemu nyingi amezungumzia lakini hebu na kule kwetu mkutazame. Mongoroma andiko letu lina zaidi ya miaka mitatu na tija yake ni kubwa, hata uchumi baadaye ungeongezeka sana kule Kondo, Warangi wanguenza kufurahi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye masuala hayahaya ya mabwawa, Bwawa la Munguri pale Kondo ambalo kwa kiwango kikubwa lingeweza kusaidia kupunguza upungufu wa maji Kondo Mjini na maeneo ya pembezoni lina muda mrefu tumelisemea, limeandikiwa, limefuatiliwa lakini inaonekana kama Serikali imekuwa na kigugumizi kuanza kufanya mchakato wa kushughulikia bwawa lile liweze kupata maji ili wananchi wa Kondo wanufaike. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, aah, vipi tena?

NAIBU SPIKA: Muda umekwisha Mheshimiwa?

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, basi nashukuru kwa hayo. Nilitamani kumalizia kidogo, lakini naunga mkono hoja, naomba mzingatie hayo niliyoyaeleza. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Yosepher Komba kwa dakika tano, Mheshimiwa Aida Khenani dakika tano halafu atafuatia Mheshimiwa Willy Qambalo. (*Makofi*)

MHE. YOSEPHER F. KOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa, naomba niwape pole wafiwa wote wa ajali ya watoto kule Arusha, lakini pia niwape pole wananchi wa Mkoa wa Tanga, hasa maeneo ya Muheza, Korogwe, Tanga Mjini, Pangani ambao wamepata madhara makubwa kutokana na mvua zinazoendelea. Vile vile, niwape pole familia ya mtoto wa miaka 12 pale Kata ya Genge-Muheza ambaye alifariki juzi kwa kudondokewa na ukuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie machache kwenye Wizara hii ya Maji. Ukiangalia kwenye Kitabu cha Waziri, ukiangalia yaliyoandikwa humu, bado hawajawa *serious* kuhakikisha kwamba wanamtua mama ndoo kichwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najaribu kufikiria msemu wenu wa kumtua mama ndoo kichwani, sidhani kama mnamaanisha. Kwa sababu, kwa Kiswahili cha kawaida, huwezi kutua kitu ambacho hakipo. Kwa hiyo, mnataka kusema mwanamke aendelee kubeba ndoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuwaambia na kuwaomba, nchi ilipofikia tangu tupate uhuru hatutaki kusikia ndoo kichwani, tunataka kusikia mama anabeba maji si zaidi ya mita 400, tunataka kusikia mtoto wa kike anaenda shule bila kufikiria maji, tunataka kusikia watoto wa chini ya miaka mitano hawafi kwa magonjwa yanayotokana na shida za maji, tunataka kusikia akinamama wajawazito wanapoenda kujifungua hawaendi na ndoo za maji hospitalini, tunataka kusikia na kuona mnafanya mambo ambayo yanaendana na umri wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zilizoendelea sasa hivi wame-*advance* kutengeneza *ATM* za maji, Tanzania bado

tunafikiria ndoo za maji vichwani, ni aibu! Nimepitia bajeti ya maendeleo mmezidi kuipunguza kutoka shilingi bilioni 900 mpaka shilingi bilioni 600, sijui lengo lenu ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba nichangie kidogo kuhusu Mfuko wa Maji. Tunajua faida zinazotokana na mfuko huu ambao mliutengeneza kwa sheria hapa Bungeni mkiamini kwamba tozo ya shilingi 50 kwenye mafuta itasaidia kwenye miradi ya maji. Cha kushangaza tozo imeenda vizuri lakini matumizi mmeanza ku-*diverge*. Matumizi mengi ya mfuko huu yameonekana yameenda kwenye *administration* kuliko kwenye miradi halisi. Niwaombe muongeze shilingi 50 kwenye mfuko huu iwe shilingi 100 ili miradi ya maji iweze kutekelezwa kwa kiwango kinachotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naunga mkono huu Mfuko wa Maji uendelee kuongezwa hela kwa sababu, kwenye Wilaya ya Muheza tuna Mradi wa Zigi - Pongwe ambao ni *almost* shilingi bilioni 2.7 na mfuko huu ndiyo chanzo kikubwa cha fedha kwenye huu mradi na fedha zimeanza kutolewa. Kuna miradi mingi inaanzishwa lakini inashia katikati, niendelee kuwaomba Serikali muutendee haki mradi huu kwa sababu hali ya maji Muheza ni mbaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba mtutendee haki katika mradi huu kwa sababu mpaka ninavyoongea Muheza Mjini ambapo tumeshaanza kuanzisha Mamlaka ya Mji Mdogo tuna asilimia isiyozidi 25 ya wananchi wanaopata maji safi na salama. Niwaombe sana muutendee haki mradi huu kupitia mfuko huu kwa kuongeza Sh.50/= ili iwe Sh.100/= ili angalau 70% iende vijijini, 30% ibakie mjini. Pia kwa kutengeneza mfuko haitoshi, tunaomba kuwe na utaratibu mzuri wa kusambaza hela hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kitu kingine naomba niongelee ukosefu wa *emergency plan*. Tumeona kuna mafuriko yanaendelea maeneo mbalimbali ya nchi lakini hakuna *plan* yoyote ya Wizara ya Maji kwa ajili ya ku-*control* hali hii. Mafuriko yanatokea mabomba yanaziba, hivi sasa

ninavyoongea maji ya Mkoa wa Tanga katika maeneo mengi, Tanga Mjini, Muheza, Korogwe na maeneo mengine ni kama chai ya rangi, lakini kama mngokuwa na *emergency plan, treatment plan* na *strainer* za kuchuja maji ingesaidia sana inapotokea mvua na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia miundombinu ya maji kwenye nchi hii imechakaa.

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Yosepher muda wako umekwisha. Tunaendelea na Mheshimiwa Aida Khenani atafuatiwa na Mheshimiwa Qambalo Willy na Mheshimiwa Suzana Mgonokulima ajiandae.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nami naungana na wachangiaji wote waliopita kwa suala la kuanzisha Wakala wa Maji Vijijini. Tusipoanzisha Wakala wa Maji Vijijini, tutaimba nyimbo za siku zote ambazo hazitapatiwa majibu. Tukianzisha wakala tutaepusha malalamiko mengi ambayo yanajitokeza kwenye vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo ambayo ni vigumu sana kuweza kuyakamilisha kwa sababu suala la maji linahitajika maeneo yote. Wanafunzi hawawezi kukaa darasani kwa muda wote kama maji hayapo. Pia, kilimo tunachokisema kila siku kama uti wa mgongo na majina mengi ambayo tumejipa, hatuwezi kukidhi malengo kama suala la maji halitapewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Serikali, unajua tumekuwa na vipaumbele vingi, hebu tukae tuangalie kipaumbele ambacho Watanzania wanakizungumza. Leo kama maji ni kipaumbele cha nchi hii, hatuwezi kupunguza bajeti, tungeongeza bajeti. Inaonesha ni jinsi gani mambo tunayoyazungumza hapa ni kama kuna watu wengine washauri tena tofauti na Bunge. Suala la maji tulizungumza,

tunazungumza tena, lakini kuna mambo ambayo yanapewa vipaumbele nje na yale ambayo Wabunge wanazungumza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Serikali, ni vyema wakazingatia basi yale ambayo tunayazungumza. Ukitazama hili suala la maji haliko upinzani, haliko chama tawala, wote tunazungumza maji, maji, maji. Tunaomba basi tupate mikakati ya Serikali, angalau basi wawe wanatusikia na kutusikia ni pale wanapojibu yale tunayoyazungumza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia vyeti *fake*, kuna bili *fake*, sijui kama Waziri anajua. Kama maji hayapo lakini bili zinasoma, zinasomaje? Kwa hiyo, kipindi wenziwe wanazungumzia vyeti *fake*, yeye ajue kuna bili *fake*! Naomba aje hapa atuambie kama maji hayapo bili zinakujaje? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye Mkoa wa Rukwa lazima wakae pamoja Wizara tatu, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji na Mazingira. Mkoa wa Rukwa hatujawahi kulia njaa hata mwaka mmoja lakini kinachotokea saa hizi kwa ajili ya kufurahishana, yaani anakuja mtu wa mazingira, wananchi wamelima mahindi, anawaambia wakate wamelima kwenye vyanzo vya maji. Ni kweli hatukubali kulima kwenye vyanzo vya maji lakini watuambieni Serikali wametenga eneo gani mbadala wananchi wakalime? Hatulimi bangi bali mazao ya chakula. Tunahitaji wakae pamoja waje na majibu ya kueleweka ya kuwasaidia Watanzania. Ni kweli wanaepusha vyanzo vya maji visiharibiwe lakini wanataka watu wafe na njaa? Waje watupe majibu ya uhakika Watanzania wa Rukwa wajue. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba nimwambie kwa taarifa tu Mheshimiwa Waziri, mwaka jana tu wanawake 12 wamepoteza maisha kwa kufuata maji umbali mrefu. Leo tunazungumzia maji hayohayo tena tayari bajeti imepungua wakati maji bado hawajapata. Leo mimi nakujaje

namshangilia hapa Mheshimiwa Waziri wakati wanawake walionipigia kura wanapoteza maisha na bado hana mikakati yoyote ya kuonesha mazingira rafiki ya kuwasaidia maji. Tunaomba majibu ya kuridhisha ambayo yatawasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huu tunazungumza kuna wanawake ambao wamefariki, kuna wanawake ambao wamebakwa, kuna wanawake ambao wameathirika kuhusiana na ndoa zao, kuna wanawake ambao wamepoteza mapato, huu muda wanaofuata maji wanashindwa kufanya biashara wanaanza kuhangaikia maji. Mheshimiwa Waziri tunaomba na Waziri anayehusika na upande wa watoto, Wizara ya Afya, hakuna kitu kitawezekana bila maji. Kwa hiyo, wanapokaa pamoja waangalie basi, maji ni kipaumbele hakuna mambo mengine. Nakushukuru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Qambalo Willy atafuatiwa na Mheshimiwa Suzana Mgonokulima na Mheshimiwa Gibson Blasius Ole-Meiseyeki ajiandae.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ili na mimi niweze kuchangia juu ya sekta hii muhimu katika maisha na maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kutoa pole nyingi sana kwa wazazi, wanafunzi na Walimu na Watanzania kwa ujumla kwa ajili ya ile ajali mbaya iliyotokea kule Karatu, iliyochukua maisha ya wanafunzi wetu wengi na Walimu. Mwenyezi Mungu aweke roho zao mahali pema peponi. *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Amina.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna ubishi juu ya suala la umuhimu wa maji. Kila mtu anafahamu, wanyama wafugwao wanafahamu hata wale

wa porini wanafahamu umuhimu wa suala hili. Hata Vitabu Vitakatifu vya Mungu vimeeleza juu ya umuhimu wa maji kwa maisha ya mwanadamu tangu uumbaji. Kwa hiyo, naomba tusilifanyie mzaha na mchezo suala la maji kwa maisha ya watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kitabu cha Waziri. Ukienda ukurasa wa saba imeandikwa 72.5% ya Watanzania waishio vijijini wanapata maji safi na salama katika umbali wa mita 400. Mheshimiwa Waziri takwimu hizi amezitoa wapi? Uhakika wa takwimu hizi ameufanyia kazi kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe pia umekuwa ukikaa kwenye Kiti hicho mara nyingine asubuhi, katika Kipindi cha Maswali pale asubuhi, kukiwa na swali la maji, Wabunge tunabanana kupata nafasi hiyo, hicho ni kiashiria cha kutosha kwamba eneo hili la maji lina matatizo makubwa. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri, hizi takwimu zake hebu azirejee kama kweli ziko sahihi. Haiwezekani kama 72% ya Watanzania waishio vijijini wanapata maji, Wabunge wangepaza sauti zao kiasi hiki humu ndani, isingewezekana! Kwa hiyo, takwimu hizi nina wasiwasi hazina usahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tena wanasema ndani ya mita 400. Wengi tulioko humu ndani tunatoka vijijini, hizi mita 400 zimesemwa kwenye sera lakini nadhani si kweli kwamba asilimia hiyo inapata maji kwa kiasi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana tumewasilishiwa bajeti hapa ambayo mwaka jana tulipoipitisha, leo hadi mwezi wa tatu utekelezaji wake ni 19.8%. Naamini kwenye jambo hili kuna mkono wa mtu. Haiwezekani kwenye bidhaa muhimu kama maji tunapata asilimia ndogo kiasi hicho. Nawaomba ndugu zangu Mawaziri hapo mjitizame na mjipime kama kweli mko sahihi kuwa hapo kwenye Wizara hii muhimu namna hii, hii asilimia ni ndogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Watanzania tujiandae kushuhudia sasa migogoro mingi ikitokea kwenye

vyanzo vya maji kwa sababu vyanzo vya maji ni vichache. Watoto wetu waende shule asubuhi wamebeba vidumu vya maji kwa sababu shule hazina maji. Akinamama wetu watembea kilomita nyingi kutafuta maji kwa sababu maji hakuna. Afya ya Watanzania iendelee kuwa rehani kwa sababu ya kutumia maji yasiyo safi na salama na yale mengine ambayo yanafanana na hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wale ambao wanasema tuongeze tozo kwenye fedha za mafuta. Ukiangalia katika zile fedha ambazo zimetolewa shilingi bilioni 181, asilimia 57 ya fedha hii imetokana na Mfuko wa Maji. Kama tumeweza kupata asilimia 57 kutoka kwenye Mfuko wa Maji, naamini tukiongeza mara mbili tunaweza kupunguza tatizo hili la maji kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia najjuliza tulikuwa tumetoka kwenye ule Mpango wa Progamu ya Maji - *WSDP I* sasa tumeingia kwenye *WSDP II* na tumeaminishwa siku za nyuma kwamba hizi ni fedha za Benki ya Dunia. Hizi fedha za Benki ya Dunia zipo wapi kama miradi tunatekeleza na fedha za Mfuko wa Maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda katika bajeti ya mwaka 2017/2018, asilimia ndiyo hiyo imeshuka kutoka shilingi bilioni 900 sasa tumekwenda shilingi bilioni 600. Bajeti ya mwaka jana, Wilaya ya Karatu tulikuwa tumetengewa shilingi bilioni 1.4 lakini hadi sasa tunavyoongea tumepata shilingi milioni 540, bado shilingi milioni 610. Mheshimiwa Naibu Waziri yuko kwenye Kiti hapo naomba sasa wakati wanajumuisha watuambie, naamini tatizo hili la kutokupeleka fedha za mwaka jana haliko kwenye Jimbo la Karatu peke yake bali ni maeneo yote, katika miezi hii miwili iliyobaki fedha hizi wanazipeleka lini. Miradi haikamiliki kwa sababu fedha hawazileti. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye jedwali 5(a) ambapo fedha zimetengwa kwa kila wilaya au kwa kila jimbo, pale utaona mambo ya ajabu sana. Ziko wilaya mwaka jana zilipewa shilingi bilioni mbili, tatu na kadhalika

na safari hii zimepewa hivyo hivyo. Ziko wilaya zimepata mgao wa shilingi milioni 500, 600 au 700, kwa nini tunatofautiana namna hii? Kama sungura ni mdogo basi tugawane wote ili kila mtu apate hicho kidogo. Mbona wakati wa vile vijiji kumi vya ule Mradi wa Benki ya Dunia tulipewa kila mtu vijiji kumi kumi! Kwa nini leo hii wengine wana mabilioni na wengine wana milioni tena chache sana? Hili ni jambo ambalo halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sitakuwa nimewatendea haki wananchi wa Bonde la Eyasi kama sitasema kuhusu mradi wao wa umwagiliaji. Nashukuru Naibu Waziri upo hapo na ulifika katika bonde lile, tuna mgogoro mkubwa wa uhifadhi wa chanzo cha maji Qangeded. Bahati nzuri Waziri Mkuu alifanya ziara kule Mangola mwezi wa kumi na mbili, wananchi walimlilia kiongozi wao na kiongozi wao akawasikiliza. Waziri Mkuu alitoa kauli ya Serikali kwa kusema chanzo kile cha Qangeded kihifadhiwe kwa umbali wa mita 500 na mashine zote zilizowekwa kwenye mto ziondolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha hadi leo tunavyoongea bado mashine zile ziko kule mtoni zinachukua maji mengi na wananchi wanaokaa chini hawapati bidhaa hiyo. Bado zile mita zilisemwa na Waziri Mkuu hazijafanyiwa kazi. Naomba kufahamu, hivi ni nani wa kutekeleza kauli hii ya Waziri Mkuu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mangola walimsifu na walimpongeza sana Waziri wao Mkuu kwa kutambua kero yao lakini viongozi wale wa chini wameshindwa kufanya kazi ya kupima mita zile zilizowekwa kuanzia kwenye chanzo hadi kwenye ziwa. Kwa hiyo, wakati watakopojumuisha naomba walizungumzie hili suala la chanzo cha Qangeded katika Bonde la Eyasi. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Qambalo muda wako umekwisha. Mheshimiwa Suzana Mgonokulima

atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Gekul na Mheshimiwa Esther Matiko watachangia dakika tano tano nafasi ya Mheshimiwa Gibson Ole-Meiseyeki.

MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia jioni ya leo Wizara ya Maji. Maji ni uhai wa kila kitu, ikitokea jambo lolote hapa mtu mwingine ameanguka ghafla hapa Bungeni akifika pale hospitalini Madaktari wataanza kumwongeza *drip* la maji. Hivyo, tuone umuhimu wa maji unavyotakiwa katika maisha ya mwanadamu. Hata magari, meli, ndege vyote hivyo vinahitaji maji. Hata sasa hivi moto ukitokea jengo lolote utaona tunasema gari la zimamoto liko wapi, maji yaje ili waweze kuzima moto. Kama kweli maji ni uhai basi ifikie wakati muafaka wa kuona Serikali inaona jambo hili ni la umuhimu kitaifa na wazingatie kwamba kwa kukosa maji ni kukosa kuwa na maendeleo katika Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sera yetu inasema tunataka kumtua mwanamke ndoo ya maji kichwani. Imeonekana suala la maji siyo tatizo la kifamilia ila ni tatizo la mwanamke ambapo si kweli. Tatizo la maji ni tatizo la kitaifa na hivyo tulijue kama ni tatizo la kifamilia ni janga la kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba kutokana na kuwa mwaka jana tulikuwa tumeweka ongezeko la bei ya mafuta ya dizeli na petroli kwa ajili ya kuhakikisha maji yanafika vijijini lakini imeonekana ongezeko ya bei ya mafuta haya limetatua changamoto ya maji kwenye miji yetu. Changamoto ya maji kwenye miji si kubwa kama ilivyo kwenye vijiji. Hivyo basi katika bajeti hii naomba Wabunge wote tuombe tuwe na ongezeko tena la tozo kwenye mafuta tufikie Sh.100, basi asilimia 70 iende vijijini na asilimia 30 iende mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla suala la maji ameachiwa mwanamke utaona hata wakati wa uzinduzi, Waziri anakinga maji kwenye ndoo anamtwisha mwanamke kwa nini basi akikinga maji asimtwishe mwanaume wakati

suala hili ni tatizo la kifamilia? Naomba tuelewe kwamba suala la maji siyo tatizo la mwanamke ni la kifamilia, hivyo basi, kama ni tatizo la kifamilia, isionekane ni kumtua ndoo mwanamke kichwani bali ni pamoja na waume zetu tuliokuwa nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niingie kuzungumzia Mkoa wangu wa Iringa, mkoa wenye neema na uliobarikiwa ambao una vyanzo vya maji, tuna Bwawa la Kihansi, Bwawa la Mtera, Mto Lukosi, Mto Mtitu na Mto mdogo Ruaha. Cha ajabu pamoja na kuwa tuna vyanzo vyote hivyo kuna vijiji vina shida ya kuliko mtu anavyoweza kufikiria. Vijiji hivyo ni Nyakavangalala, Lyamgungwe, Lupembelwasenga, Luhota, Mkalanga, Usolanga na vingine vingi katika mkoa huu pamoja na Mji Mdogo wetu wa Ilula ambapo chemchem ya Ibofye iko jirani sana na nafikiri ni kama mita za mraba zisizopungua arobani na tano. Tumeshindwa kuweka miundombinu ili watu wa Mji Mdogo Ilula waweze kupata maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi navyozungumza Mji Mdogo wa Ilula wanauziwa maji ndoo ya lita ishirini kwa Sh.500. Huo ni Mji Mdogo tena uko kwenye barabara kuu inayotoka Dar es Salaam kuelekea Zambia. Naomba Mawaziri wenye Wizara hii washughulikie tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo hicho cha Ibofye kwanza kabisa kwenye bajeti ya mwaka 2000-2005, Bunge hili lilipitisha bajeti ili waende kufanya kazi ya miundombinu katika chanzo hicho, wakati huo akiwa Mheshimiwa Mbunge Mlawa. Hadi leo navyozungumza sielewi hata hizo fedha zilikoishia. Naomba Mawaziri wahusika walifuatilie suala hili ili waelewe. Ndiyo maana tunasema tutakapoweka ongezeko kwenye bei ya mafuta kuwe na bodi maalum itakayofuatilia ongezeko la fedha hizi ili ziende kwenye miradi tuliokusudia wa kupunguza uhaba wa maji kwa wananchi katika taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Iringa ni kati ya mikoa ile minne inayozalisha sana chakula nchini Tanzania.

Nataka niseme njaa tunaitaka kwa makusudi kwa sababu ya kutokuwa na mbinu mbadala kwa wakati muafaka wakati nchi yetu ina wataalam waliosomea na kubobea. Tatizo letu ni kwamba wakati wa mvua hatuna mabwawa ya kutunza maji ya mvua ili wakati wote tuweze kuendelea na kilimo cha umwagiliaji. Kutokana na hilo, tuone ni wakati sasa wa kuhakikisha bajeti hii inayokuja kuombwa na Waziri mwenye dhamana imeongezeka ili tuweze kujenga mabwawa maeneo hayo ambayo nasema ni lazima tuwe na mabwawa yanayotunza maji ya mvua tuweze kuondokana na tatizo la maji. *(Makofi)*

Katika Mkoa wangu wa Iringa akinamama wengi wajasiriamali ni wakulima wa mazao ya mbogamboga. Hivyo kukosa mifereji ya umwagiliaji iliyo bora wanashindwa kumudu shughuli zao za kilimo na kuweza kujikwamua katika dimbwi la umasikini walilokuwa nalo ukizingatia kazi kubwa ya kulea familia ni ya mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri mwenye dhamana katika Mkoa wangu wa Iringa katika maeneo haya yote niliyoelekeza na vijiji ambavyo sikuorodhesha hapa kutokana na wanawake wale walivyo na juhudi kwenye kilimo ahakikishe amepeleka mradi wa maji ili waweze kuendelea na shughuli zao za kilimo cha mbogamboga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Kata yetu ya Mahenge...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni dakika saba, nilikuwa naangalia, nilinde. *(Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Mimi pia hapa mbele sina saa wenye saa ni watu wanaonisaidia, kwa hiyo, muda wako umekwisha Mheshimiwa.

MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, basi naunga mkono hoja ya Upinzani asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Suzana. Mheshimiwa Pauline Gekul atafuatiwa na Esther Matiko dakika tano tano, halafu Mheshimiwa Salma Mwasa ajiandae.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwakunipa dakika tano angalau niseme machache kwa ajili ya Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiukweli kama kuna Mbunge atasimama kwenye Bunge hili na kusema bajeti ya maji isiongezwe basi huyo Mbunge labda alipata Ubunge kwa kupendelewa na alipewa zawadi tu, hakutafuta kura, lakini kama alikwenda kwa wananchi akaona kero zao hatathubutu akasimama na kusema bajeti hii ziongezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja za Wabunge wote wanaosema kwamba ile Sh.50 iongezwe mpaka Sh.100 ili wananchi wetu wapate maji. Wale ambao majimbo yao, miko ya yao ina maji, tafadhali mtuache sisi ambao bado wananchi wetu hawana maji ili tuunge mkono hoja hii ya kwamba fedha ziongezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hili kwa sababu mimi niko Jimbo la Babati Mjini lakini nina Kata nzima ya Sigino yenye vijiji vinne haina maji. Asubuhi nilikuwa naongea na Mbunge mmoja ananiambia Mheshimiwa Mbunge inawezekana sana fedha hizi zisiongezwe au zikaongezwa, nikamwambia lakini hebu tupige picha siku moja Wabunge tukae wiki nzima humu ndani tusioge na tusiwe na maji itakuwaje? Akaniambia hivi, tutanunua maji ya Kilimanjaro tutaoga. Nikamwambia *okay*, una uwezo wa kununua maji ya Kilimanjaro lakini mama na bibi yako uliyemwacha kijijini kule hana uwezo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tusiweke itikadi zetu katika suala hili. Niombe Serikali isikilize kilio hiki cha Wabunge wote kwamba fedha hizi ziongezwe ili wananchi wangu wa kata ya Sigino, Jimbo la Babati Mjini wapate maji. Mheshimiwa Naibu Waziri alifika, wale akinamama walimvika mpaka na mgoroli akawaahidi kwamba katika bajeti hii fedha zitakwenda katika Vijiji vya Sigino, Singu, Dagailoi na Imbilli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwenye kitabu zimetengwa shilingi milioni 600 tu hazitatosha, lakini fedha zikiongezwa tutapata shilingi 2,700,000,000 ambazo tumeziomba. Kwa hiyo, niunge mkono kabisa hoja ya Wabunge kwamba fedha hizi ziongezwe na wananchi wa Tanzania wapate maji. Ni aibu, akinamama wanateseka, wanachota maji kongoroni, ndoo zao zinavunjika, wengine wanarudi usiku, wengine wanabakwa, wanahangaika wanatafuta maji halafu sisi wanawake humu ndani tuseme fedha zisiongezwe, inasikitisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kabisa Serikali kama mnaona tozo ya mafuta haitoshi twendeni hata kwenye mitandao ya simu, tuna 0.03 ya *service charge* ambayo siku zote wamekuwa hawalipi. Tumekuwa tukizungumza hata kwenye TAMISEMI hizi fedha haziendi. Hebu Serikali kaeni chini muangalie fedha hizi hata kama ni shilingi 20, 30, 50 tuzipeleke kwenye Mfuko wa Maji ili zipeleke maji kwa wananchi wetu. Wananchihawa wamevumilia kwa miaka hamsini, kwa nini tusiwatendee haki fedha zikaenda wakapelekelewa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sina ugomvi na Mawaziri, wao wamepelekewa asilimia 19, lakini Serikali kama mngepeleka asilimia 100 ya shilingi bilioni 900 ambazo zilipangwa maana yake kero hizi zingepungua. Kwa hiyo pia niombe Waziri wa Fedha pamoja na Serikali kwa ujumla wake Wizara ya Maji wapelekeni pesa. Pamoja na kwamba tunaomba fedha hizi ziongezwe, lakini fedha zile zilizopangwa ambapo miradi iko kwenye mchakato pia ziende.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano kwenye Jimbo langu la Babati Mjini, Vijiji vya Haraa na Imbilili tulishampelekea Mheshimiwa Waziri bado kusaini tu mikataba, lakini tunaambiwa zimeenda asilimia 19 tu, bajeti ya Wizara ya Maji ilitakiwa ziende asilimia hata 50, 60, 70 au 80 mbona Wizara ya Ujenzi fedha zimeenda? Kwa nini Wizara ya Maji ambayo inamgusa kila mwanamke katika nchi hii msipeleke fedha?Wangapi waonapita kwenye barabara zenu za lami mnapeleka asilimia zaidi ya 70 au 80 lakini akinamama hawawezi wakapelekewa fedha zao?Kwa hiyo, niunge mkono hoja hii lazima Wabunge tuwe *serious* kwamba Wizara hii waongezewe fedha.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Esther Matiko atafuatiwa na Mheshimiwa Salma Mwasa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ajiandae.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipatia fursa na mimi nichangie kwenye Wizara hii muhimu sana kwa maisha ya Watanzania na hasa kwa sisi wahanga ambao ni wanawake ambao tunatembea kilomita nyingi kutafuta maji licha ya Sera ya Maji kusema kwamba tutakuwa tunapata maji ndani ya mita 400.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kabisa zaidi ya asilimia 80 ya Wabunge waliopo humu ndani watakubaliana na ukweli kwamba maji imekuwa ni tatizo na inapelekea tunakuwa na vifo vingi. Mwanamke akienda hospitalini kujifungua bila maji kwa kweli sidhani hata kama zoezi litaweza kukamilika kama inavyotakiwa na katika hali ya usafi na afya. Zaidi mtakubaliana na mimi kwamba watoto wetu wa kike wengine wanarudi majumbani kutoka shuleni au hawaendi kabisa kwa sababu ya kukosa maji hasa wakiwa kwenye zile siku zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na kulaani wale Wabunge waliosema kwamba tusingeze fedha. Ni ajabu sana kuona kwamba fedha za maendeleo zilizokwenda kwenye sekta hii ya maji ni asilimia 19 tu ilhali kwenye sekta ya ujenzi fedha zilienda zaidi ya asilimia 100 tulizozipanga kwenye bajeti iliyopita. Kwa hiyo, naomba sana Serikali kwa mapendekezo ambayo tumeyatoa hapa Bungeni tuongeze kutoka shilingi 50 mpaka shilingi 100 kwa sababu hizi fedha zipo *ring-fenced*, tuziongeze zifikie hapo tuweze kutatua matatizo ya maji vijijini na mijini pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi sasa kwenye Jimbo langu la Tarime. Tarime tuna Hospitali ya Wilaya na kuna kipindi tunakosa maji kabisa, wagonjwa wakienda pale inakuwa shida na mtafutano. Tuna Gereza la Tarime linahitaji maji na lina shida kubwa sana, tuna taasisi zingine mbalimbali zahanati na vitu kama hivyo vina tatizo hili la maji. Katika Mji wangu wa Tarime licha ya kwamba ni mjini ni chini ya asilimia kumi tu ya wakazi wa Tarime ndio wanapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati najaribu kupitia hiki kitabu kwa kweli nimesikitika sana. Nimekisoma na kugundua katika miji mikuu ambayo imepata maji Tarime haipo licha ya kwamba nilishauliza maswali mengi sana hapa ndani na Waziri akaniahidi kabisa kwenye bajeti hii atakwenda kutenga fedha na kuhakikisha kwamba anatatua tatizo la maji Tarime. Nikasema kwa mfano mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda mpaka Tarime na Sirari tayari mwaka 2012 walishafanya upembuzi yakinifu na Benki ya Maendeleo ya Ufaransa ilishajitolea kufadhili mradi huu na Waziri akaniahidi kwamba watatenga bajeti, nimeangalia sijaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Tarime wanateseka na maji. Wanapoteza muda mwingi ambao wangeenda kufanya shughuli za kimaendeleo kutafuta maji. Akinamama wajawazito wanatembea kilomita nyingi kutafuta maji. Kwa hiyo, naomba sana mnisaidie kwa kuweka fedha ili kutatua tatizo la maji katika Mji wa Tarime. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarime pia tuna Bwawa la Nyanduruma, lile bwawa ni la enzi za Mjerumani lakini mpaka leo hii halijaboreshwa. Napenda sana Serikali muwekeze fedha pale kwani bwawa lile tukiliboresha zaidi litakwenda kutoa mtandao wa maji ambayo yataenea kwenye Mji wa Tarime na kusaidia kutatua tatizo la maji wakati tukisubiria maji ambayo yatatoka Ziwa Viktoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, linguine, kuna mradi ambao ulikuwa ni msaada kwenye Kata ya Nyandoto, mradi wa Kemangeumekamilika lakini bado hamjaleta fedha kuweza kuweka sasa mtandao wa maji kuwafikia wananchi. Tenki limeshajengwa, tunahitaji kupata fedha ili kuweka *network* ili wananchi wa Tarime waweze kupata maji. Nishauri hii sio kwa Tarime tu hata huko kingine unakuta wakati mwingine tuna visima vya asili ambavyo tukiviboresha vinaweza kusaidia kutatua tatizo la maji kwa muda mfupi wakati tukisubiria mjipange kwa mipango ambayo inatekelezeka kwa kutumika kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana Wabunge tukatae hii bajeti...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa Esther Matiko. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Salma Mwasa, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka na Mheshimiwa Margaret Sitta ajiandae.

MHE. SALMA M. MWASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza, napenda kuwapa pole wananchi wangu wote wa Dar es Salaam waliopata adha za mvua. Wengi wamepata mafuriko na nyumba zao hazikaliki, nawapa pole sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchangia Wizara hii ya Maji. Kwanza niseme maji ni kilio. Maji ni mateso

kwa mwanamke, mtoto na baba wa Kitanzania. Kwa kukosa maji kwa kweli wanapata mateso makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hivyo ndivyo kwanza niuongeleee Mfuko wa Maji. Mfuko huu wa Maji naona ndiyo pekee ambao unatakiwa kutukombooa kwa kuona kwamba bajeti ya maji sasa inafeli. Mfuko huu wa Maji mpaka sasa unachangiwa kwenye mafuta Sh.50 tu, ningeeomba uongezwe hiyo Sh.50 nyingine au ikionekana kwenye mafuta kunaleta *inflation* basi iongezwe kwenye pombe au tuangalie kwenye Mfuko wa Barabara kama tunaweza kutoa asilimia 10 iongezwe kwenye huu Mfuko wa Maji. Maana inavyoonekana *the only solution* ya kumsaidia Mtanzania sasa hivi ni huu Mfuko wa Maji ambao ndiyo unaweza kusaidia Taifa kwa *hundred percent*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo niongelee miundombinu ya maji chakavu Dar es Salaam. Kwa kweli miundombinu ya maji Dar es Salaam inahitaji ukarabati mkubwa. Miundombinu mingi imechakaa, Waziri ni shahidi kwa sababu anaishi Dar es Salaam na asilimia 90 ya Wabunge wote hapa mnaishi Dar es Salaam, mnayaona mabomba yanavyopasuka na kuleta *disturbance* kubwa hasa kwenye barabara. Unakuta barabara zote zimejaa maji utafikiri kuna mvua yaani saa zote Dar es Salaam ni mafuriko kwa sababu ya miundombinu ya maji kuchakaa. Naomba kabisa Waziri anapokuja kuhitimisha atuambie kwa bajeti hiyo aliyoitenga huo uchakavu ataurekebisha vipi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niongelee bajeti ya maji. Wizara hii naona kama vile haipewi kipaumbele kwa sababu tumeona bajeti ya maendeleo imetekelezwa kwa asilimia 19 tu. Kwanza atueleze kwa nini bajeti imepungua kutoka shilingi bilioni 900 mpaka shilingi bilioni 600? Vilevile atueleze kwamba hii Wizara kumbe siyo kipaumbele? Kama siyo kipaumbele basi na Waziri ni mshauri wa Rais amuulize kwamba hii Wizara mimi unanifanyaje? Kwa nini kati ya shilingi bilioni 900 za maendeleo apewe shilingi bilioni 150 ambayo sawa na asilimia 19 na wakati anaona kabisa tatizo la maji linavyokuwa kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Wizara ya Miundombinu hapa imepewa asilimia 84, kumbe kuna Wizara ambazo zinapewa bajeti kubwa na kipaumbele. Hii miundombinu inapewa kipaumbele sio vibaya, lakini maji nayo yapewe kipaumbele. Kwa sababu Wizara ya Miundombinu na Uchukuzi ndio mnanunua ndege, kujenga barabara, sawa ndege ni nzuri kupanda lakini utapandaje ndege kama hujaoga? Hivi kweli utapanda ndege kama hujaoga hiyo ndege itakuwaje? Utapita kwenye barabara hujaoga? Mimi nashangaa hiyo *Bombardier* kama tunapanda hatujaoga inabidi sasa tuwe na *perfume* ndani kwa sababu maji hayatoki na maeneo mengine ndio maji hakuna kabisa. Sawa ndege sisi imetu-*savesana* lakini inakuwaje tupande kule bila kuoga. Mimi naona hiyo bajeti iangaliwe upya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee pia miradi mingi ya maji kutegemea fedha za wahisani. Kwanza, sasa hivi naona kabisa mahusiano ya sisi na wahisani siyo mazuri na wala hawatuletei hela. Sasa mnavyotuongia hizi pesa nyingi tutegemee miradi ya wahisani, kwa mfano, huo mradi unaoendelea Dar es Salaam umetengewa dola za Kimarekani bilioni 32 wanasema hizo fedha zinatoka *World Bank*, je, zitakuja?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimeona kwenye Kitabu cha IV cha maendeleo naona kabisa Mkoa wa Dar es Salaam mmeandika *water and sanitation* shilingi milioni 900 lakini zote ni fedha za nje, hivi unategemeaje hela kutoka kwa mwenzio? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa mkubwa kama ule maana wote mnakaa kule Dar es Salaam lakini hela za ndani hamna mnategemea hela za nje tu, shilingi milioni 900 zote zitoke nje, kama wasipoleta? Sasa hivi wana vikwazo kibao hawaleti sasa hivi. Sasa nyie mnavyotegemea hela hizo shilingi milioni 900 zitoke nje inakuwaje? Sasa wasipoleta Waziri atatueleza kwa sababu miradi yetu itakuwa inakwama, yeye anategemea tu wafadhili, awaulize kwa nini hawamtengei fedha za ndani? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niende pia kwenye miradi hii iliyoainishwa kwenye ukurasa wa 72 na 73, uchimbaji wa visima Mpera na Kimbiji. Hivi visima toka vianze kuchimbwa sasa hivi ni miaka saba, hiyo miradi kwa nini inasuasua namna hiyo? Mimi mwenyewe nikiwa kama Mthamini, tulishathamini kule mwaka 2007 ili watu waondoke ili vile visima vichimbwe, leo ni miaka mingapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anaendelea kutuambia hapa Kimbiji na Mpera sijui vita-save Gongo la Mboto, Chanika, Keko, hii siyo kweli, huu mradi unakamilika lini mpaka leo haujakamilika? Miaka saba sasa huu mradi anatuambia tu unakamilika, upembuzi yakinifu umekuwa sawa na anatafuta hela. Naomba atafute hela sehemu nyingine tuelewe, huko anakotafuta sasa hivi siko. Atafute sehemu nyingine atuambie anazitafuta wapi na atuambie huu mradi unakamilika lini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna mradi huu wa ukarabati na upanuzi wa mfumo wa kusambaza maji safi, hapa amesema kabisa kwamba sehemu ambayo hakuna miundombinu hiyo atasambaza na amesema umetengewa dola za Kimarekani milioni 32. Vijiji alivyovitaja ni Changanyikeni, Makongo Juu, Kiluvya, Makabe, Msakuzi na vingine vingi lakini anategemea hela ya Benki ya Dunia, yaleyale yanakuja, asipozipata? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi sisi tunashangaa utekelezaji wa huu mradi unakuwaje? Huu mradi unatakiwa utekelezwe mwaka huu na sisi tunakaa huko huko na hatujaona hata hilo bomba lenyewe, lakini hapa anatuambia anaanza kujenga matanki na kadhalika. Sisi tunasema kabisa bwana kama huo mradi umefeli atueleze tuelewe kwa sababu mambo ya kuanza kutudanganya hapa hapana. Akija hapa kuhitimisha atuambie kabisa kwamba huu mradi bwana mpaka sasa hivi tunaendelea kutafuta hela tujue na sisi tutaendaje kutafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niendeleo kusema kwamba, inaonekana kabisa bajeti ya maji hapa ni tatizo

na kama ni tatizo basi wananchi wafundishwe njia nyingine sasa za kuvuna maji ya mvua. Vibali vya ujenzi vyote vielekeze nyumba kuwa na mfumo wa kuvuna maji ya mvua la sivyo mtu asijenge...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salma Mwasa muda wako umekwisha. Tunaendelea na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Sitta na Mheshimiwa Kiswaga Boniventura Destery ajiandae.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo na mimi nichangie Wizara hii ya Maji. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuniwezesha jioni hii kusimama hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye Mfuko wa Maji. Wachangiaji walio wengi hapa wameongelea kuhusu Mfuko wa Maji uongezewe fedha kutoka shilingi 50 kwenda shilingi 100 na mimi naunga mkono. Hata hivyo, naunga mkono lakini kwa upande mwingine nasikitika. Nasikitika kwa sababu nimeangalia kwenye hiki kitabu cha Mheshimiwa Waziri kwenye huu Mfuko wa Maji kwangu mimi sijatengewa pesa hata shilingi. Kwa hiyo, pamoja na kuomba kwamba uongezewe fedha lakini kwangu mimi ni majanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifungua ukurasa wa 159 - 164 pale pameorodheshwa watu waliotengewa fedha zinazotokana na mradi wa maji katika Miji Midogo lakini Liwale haijatajwa. Kwa bahati mbaya zaidi ikaja ikatajwa ukurasa wa 164, namba 32 pale pametajwa Halmashauri 14 ambazo zimetengewa shilingi bilioni 3.5. Hivi mimi kama mwakilishi wa wananchi wa Liwale pesa hizi zisipofika nazifuatilia wapi? Huoni uwezekano nitakavyokwenda kufuatilia pesa hizi naweza nikaambiwa zimeenda Chato, Mkuranga ama sehemu fulani kwa sababu pale

zimerundikwa Halmashauri zaidi ya 14, nashindwa kuelewa.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika Halmashauri yangu ya Wilaya ya Liwale nimeshakwenda kwa Waziri mara kumi kidogo. Nimemwambia kuna mradi wa kutafuta chanzo cha maji mbadala kwa Mji wa Liwale, umeshakula shilingi milioni 200 lakini mpaka leo mradi ule umekufa na maji Liwale hatuna. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hapa atuambie hatua gani imefikia mpaka mradi ule umekufa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye Mradi wa Maji Vijijini ambao unafadhiliwa na *World Bank*, awamu ya kwanza ilikuwa ni vijiji kumi lakini kwenye Halmashauri yangu nina vijiji saba tu lakini bado mpaka leo hii Vijiji vya Kipule, Mihumo na Ngongowele visima vile vimeachwa, vimeishia ardhini hakuna maji mpaka leo. Mheshimiwa Waziri atakaporudi hapa kuhitimisha hoja hii naomba atueleze ni nini hatima ya mradi ule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio hivyo tu, nashukuru, *Alhamdulillah*, Kijiji cha Mpigamiti mpaka sasa hivi kimepata maji lakini kuna Vijiji vya Ngolongopa, Naujombo, Kitogolo, Mtawambo, Mkutano, Makata, Mikunya, Ngunja, Mkundi na Nandimba havina maji kabisa. Kwa hiyo, kwa heshima na taadhima namwomba Mheshimiwa Waziri awahurumie watu wa Liwale. Kama takwimu zinaonyesha kwamba Liwale tuko watu wachache kama ambavyo nimewahi kusema hatustahili kupata maji hayo niyasikie leo. Kama tuko wachache basi watuwekee koki moja moja kila kijiji kuliko kutunyima maji kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naingia kwenye skimu ya umwagiliaji. Nimeshaongea na Mheshimiwa Waziri mara nyingi, kuna miradi mitatu ya skimu ya umwagiliaji Wilaya ya Liwale imegharimu nchi hii zaidi ya shilingi bilioni nne lakini mpaka leo hii ni mwaka wa saba hakuna senti hata moja iliyorudi kutoka kwenye miradi ile. Kwa maana kwamba hakuna mkulima aliyenufaika na miradi ile hasa hasa mradi

wa Ngongowele. Niameangalia kwenye kitabu chake ametaja mradi mmoja tu wa Mtawango, mradi wa Ngongowele hautajwi kabisa na huu mradi wa Ngongowele ukienda pale ni ardhi tupu mpaka leo. Nafikiri nimeshakwenda kwake zaidi ya mara tatu. Kama Liwale hawaithamini basi hata hizi pesa za Serikali nazo hawazithamini, shilingi bilioni nne zimeteketea pale hakuna chochote kilichoalishwa nchi hii, tunafikiria kufanya kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa miradi hasa ya umwagiliaji, nashindwa kuelewa, tukienda kwenye Halmashauri tunaambiwa miradi hii inasimamiwa na Kanda kwamba sisi watu wa Halmashauri hatutakiwi kuhoji chochote. Sasa inapofikia miradi ile haikamiliki nani wa kumfuata? Mheshimiwa Waziri nimeshakwenda kwake zaidi ya mara tatu naulizia, atupe ufafanuzi hii miradi nani afuatwe, watu wa Kanda au watu wa Halmashauri lakini hakuna majibu yoyote ambayo ameweza kunipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo basi, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa kuhitimisha anieleze tatizo la maji linatokana na nini hasa Mkoa wa Lindi. Hata kwenye bajeti mkoa ambao umepata bajeti ndogo zaidi ni Mkoa wa Lindi, tatizo liko wapi? Au ile dhana ya Kusini bado mnaiondeleza? Mnataka ile hadithi niliyowapa hapa iwe ya kweli? Jamani naomba tuiangalie Kusini, tuiangalie Lindi. Lindi tunahitaji maji hata kama tuko wachache hao wachache wanahitaji maji, maji hayana wingi wala uchache wa mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana kama upande wa hospitali unaweza kusema kwa sababu tunahudumia watu wachache Madaktari wawili wanatosha, lakini maji nayo je? Tunaomba Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba Wabunge wengi wamesema kwamba Wizara hii ya Maji iongezewe bajeti, naomba atakapoongezewa bajeti kama hili litakubalika basi autazame Mkoa wa Lindi maana bajeti yetu ni ndogo sana. Tena hizo fedha kidogo tulizotengewa ni za wafadhili na siyo za ndani. Kama fedha za ndani hatuna

tunategemea fedha za wafadhili itakuwa shida wasipoleta. Mkoa wa Lindi bajeti yetu asilimia kubwa ni ya wafadhili maana yake wafadhili wasipotoa pesa Mkoa wa Lindi tumeambulia patupu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijagongewa kengele ya pili, nilikuwa na hayo machache ya kumweleza Mheshimiwa Waziri. Tena kwa bahati mbaya zaidi kwa sababu ya matatizo ya usafiri nimekosa Mawaziri watatu mwezi wa Kwanza na wa Pili kuja Liwale kutembelea ile Wilaya, Naibu Waziri na Waziri wa Miundombinu ni wamojawapo, walipanga kuja Liwale lakini wameshindwa kuja kwa sababu ya usafiri, barabara chafu na mbaya. Nataka niseme kama Mawaziri hawatakuja nitaendelea kupiga kelele hapa na Mungu anawaona. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Margaret Sitta atafuatiwa na Mheshimiwa Kiswaga Boniventura Destery na Mheshimiwa Kapt. George Mkuchuka ajiandae.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie katika hoja iliyopo mezani. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na nawashukuru pia wananchi wa Urambo kwa kunipa ushirikiano. Aidha, naipongeza Serikali ya Mheshimiwa Rais Magufuli kwa kazi kubwa wanayofanya akisaidiana na Mawaziri wake, hongereni Mawaziri kwa kazi kubwa. Vilevile pia nawapongeza wanawake wenzangu walioshinda uchaguzi jana, hongereni akinamama mnaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwenye maji. Naomba nianze mchango wangu kwa kuuliza maswali manne. Kila ninapozungumzia suala la uhaba wa maji Urambo naambiwa subiri mradi wa maji kutoka Malagarasi kilomita 200 kutoka Urambo. Swali la kwanza, Mheshimiwa Waziri anayehusika aniambie ni hatua gani za dharura zitachukuliwa ili wananchi wa Urambo wapate maji wakati wakisubiri mradi kutoka kilomita 200? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kama kweli mradi wa Malagarasi umetiliwa maanani, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*wind up* aniambie ametenga shilingi ngapi za kuanza mradi huu katika mwaka huu wa fedha 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la tatu, je, Serikali haioni kwamba ni rahisi kuchukua maji kutoka *Lake Victoria* kuyapeleka Tabora na kuyafikisha Urambo kilometa 92 badala ya kusubiri maji kutoka kilometa 200? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la nne, kama kweli Wizara imejipanga kutatua tatizo la maji, naomba waniambie kwa nini hadi leo shilingi milioni 647 zilizotengwa kwa ajili ya kutafuta vyanzo vingine vya maji na mradi maalum wa Kijiji cha Izimbili mpaka leo hazijapatikana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeuliza maswali hayo kwa makusudi kwa lengo zuri tu la kuonesha kwamba tukisubiri utaratibu wa fedha uliozoeleka kila siku hatuwezi kupata maji. Ndiyo maana ukiangalia bajeti ya mwaka jana shilingi bilioni 900 zilitengwa hatimaye tukapata shilingi bilioni 181 tu na kati ya hizo shilingi milioni zipatazo 90 zilitokana na Mfuko wa Maji. Ndiyo maana unaona Wabunge wengine wote waliochangia wanasema hivi, tutunishe Mfuko wa Maji kwa kuongeza Sh.50 ziwe Sh.100 kwa sababu kwa bajeti ya kawaida imeshindikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, natoa ombi kwa Serikali, kwanza ianzishe Mfuko wa Maji Vijijini kama ilivyo umeme. Tunaamini kukiwa na Mfuko wa Maji Vijijini itakuwa rahisi kusambaza maji. Kwa msingi huo, Serikali ikikubali kupata shilingi 50 zaidi kutoka kwenye petroli au dizeli, sawa, cha maana hapa tupate tu shilingi 100 kuchangia Mfuko wa Maji. Hata hivyo, iwapo Serikali itaona kutoa shilingi 50 kwenye petroli na dizeliinaweza kuathiri sehemu nyingine basi ile shilingi 50 itokane na Mfuko wa *REA* tuchukue kidogo na Mfuko wa Barabara ili tupate Mfuko wa Maji Vijijini wenye fedha ambazo zimechangwiwa kwa shilingi 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna asiyefahamu umuhimu wa maji, kila mtu anafahamu umuhimu wa maji. Kwa msingi huo, naomba Waziri atakapokuwa ana-*wind-up* hebu atoe kauli ya kuwapa moyo wananchi wa Urambo kwamba mwaka huu ni nini kitafanyika ili wapate maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la tatizo la maji la kudumu katika shule za msingi. Shule za msingi na sekondari nyingi ukipita, mimi juzi nimezungukia kwenye shule hawana maji. Sasa napendekeza, hii nipamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia waone umuhimu wa kutokusajili shule hadi pale shule imeshawekewa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua pamoja na taasisi nyingine. Kwa sababu kwa utaratibu ulivyo hata kama maji yatatoka *Lake Victoria*, Malagarasi mpaka maji yafike kwenye shule na nyingine ziko mbali sana, kwa kweli ufumbuzi wa kudumu ni kwamba shule au taasisi za aina hiyo zisipate usajili mpaka zioneshe miundombinu ya kutega maji ya mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia napenda kusema kwamba Serikali ikikubali ombi la kuongeza Sh.50 ili kutunisha Mfuko wa Maji. Pia ianzishe Mfuko wa Maji Vijijini ili kumtua mwanamke ndoo. Bila hivyo kwa bajeti ya kawaida imeonekana haiwezekani. Naamini Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Magufuli ni sikivu kwa upande wa maji mtakubali hilo kuwe na Mfuko wa Maji Vijijini. Hii itasaidia wanawake kuondokana na kubeba maji kutoka mbali jambo ambalo linawasababisha washindwe kufanya kazi nyingine za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Kiswaga Boniventura Destery atafuatiwa na Mheshimiwa Kapt. George Mkuchuka na Mheshimiwa Omary Mgumba ajiandae.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwakunipa nafasi hii ya kuchangia. Nianze kwanza kwa kutoa shukrani kwa Wizara hii ya Maji kwa maana ya Mawaziri wote na Watendaji Wakuu wa Wizara kwa namna ambavyo wanafanya kazi. Wako watu asubuhi walisema Mawaziri hawa ni wazee, lakini nataka niseme aliyewateua bahati nzuri amefanya nao kazi, hawa ni Mawaziri makini kwelikweli na ni wachapakazi kweli. Ukienda ofisini kwao, ukiwaita jimboni wanakuja haraka kuja kuona shida ulizonazo. Kwa hiyo, kwa kweli nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimpongeze Mheshimiwa Rais. Wakati anaomba kura alifika Magu akasema hapa shida moja ni maji na mimi wakati naomba kura niliwaeleza wanachi kama maji hayatapatikana sirudi 2020. Bahati nzuri wakati anazunguka hivi karibuni kwenda Simiyu alipita Magu akasema nakwenda kumuagiza Waziri wa Maji ili aweze kuja kusaini mkataba haraka na wakandarasi wawe *site*. Hivi ninavyozungumza mkataba ule tuliusaini hadharani kule Nyasaka ambapo utahudumu kata nne kule mjini Jimbo la Ilemela pamoja na kata tatu Jimbo la Nyamagana lakini mradi huu unaunganisha pia na Lamadi na Misungwi. Magu wakandarasi wako *site*. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa ahadi yake ya kweli na Wanamagu watapata maji, Magu ilikuwa imesahaulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo mengi, mradi huu wa Magu Mjini utahudumia wananchi 46,000 lakini Tarafa ya Ndagalu ambayo haina bwawa, haina mto, vijiji 21 wakazi 86,000 wana hali mbaya kutokana na kukosa huduma ya maji. Kwa hiyo, pamoja na kwamba bajeti hii inasemwa haitoshi na mimi nikisema hii inatosha maana yake tarafa hii haitaingizwa. Hata hivyo, niendeleo kusema tunapokuwa na shilingi bilioni 600 zikaenda zote shilingi bilioni 600 mwaka huo tunahama hapo, tukiongeza ifike shilingi bilioni 900 halafu hatuna uwezo wa kuwa nazo haitusaidii. Mimi niombe shilingi bilioni 600 hizi ziende zote, wale ambao mmepangiwa miradi tutahama kwenda maeneo mengine. Pamoja na hayo,

tuuongeze huu mfuko wa shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta ifike shilingi 100 ili usaidie kuharakisha kutekeleza miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarafa ya Ndagalu na Tarafa ya Sanjo wana hali mbaya kama nilivyosema. Hawana mito, hawana mabwawa na bahati mbaya kabisa wanakwenda kuchota maji kilometa 58 wengine, wanaamka saa tisa za usiku. Nazungumza haya kwa sababu Mheshimiwa InjniaLwenge ameshawahi kufanya kazi kule Mwanza na Magu anaijua vizuri, Ndugu Kalobelo anaijua vizuri Magu. Wanaamka saa tisa na unajua Wasukuma muda ule wa mapema baba mwenye mji anakaa kwenye kimunya anachunga ng'ombe kwa hiyo kuingia kulala ni saa saba, naye amechoka, anafika kwenye kitanda puu, akiamka saa tisa amuangalie mwenzake ili atafute mtoto hayupo yuko kwenye maji. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana tuwahurumie hawa wananchi, ni tatizo kubwa. Kwa hiyo, muone kwamba wazalishaji wakubwa wa uchumi ni akinamama, muda mwingi wanaumaliza kuchota maji kuliko kuzalisha. Niombe, kama tutaongeza Mfuko wa Maji, Tarafa za Ndagalu na Sanjo ziangaliwe kwa umakini wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu hapa bado wanabeza Serikali hii ya Awamu ya Tano na bado wanasema 2020 haitarudi. Nataka niwahakikishie kwamba Serikali hii inarudi kwa kishindo kifua mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya maneno yanathibitishwa na Biblia Takatifu. Wakorintho 10:23, inasema, vitu vyote ni halali bali si vitu vyote vifaavyo. Ikaongeza, vitu vyote ni halali bali si vitu vyote vijengavyo. Vyama vyote ni halali lakini chama kinachoweza kujenga ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Vyama vyote ni halali lakini chama ambacho kinaweza kuwa kizuri ni Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mnazungumza kwamba mmemeza demokrasia kwenda kuwaeleza watu mtaenda mkaeleze nini? Kama ni demokrasia, juzi MAREHEMU Mheshimiwa Dkt. Macha amefariki tukatarajia mtaleta mtu yuleyule (mlemavu), hamkuleta mlemavu, ninyi mna demokrasia gani?

Mlituletea hapa wagombea wawili tukasema waongezeni, mkaleta sita mkawanyima kura hata ninyi, hata Makamu Mwenyekiti mmemnyima kura, hao wote wangejuzulu wakarudi CCM. *(Makofi)*

MHE. ESTHER N. MATIKO: Taarifa.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, msiseme kwamba hakuna demokrasia.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba watuvumilie kidogo, tuwe na uvumilivu wa kisiasa ili tuelewane kidogo, ninyi mmezungumza asubuhi hapa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kiswaga, naomba ukae usubiri taarifa. Sasa mmesimama watu watatu wote mnataka kutoa taarifa moja. Mheshimiwa Esther Matiko.

MBUNGE FULANI: Na mimi Mheshimiwa Naibu Spika.

NAIBU SPIKA: Mmoja tu atatoa taarifa, Mheshimiwa Esther Matiko.

T A A R I F A

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumwambia ndugu yangu, kaka yangu wa Magu, kama *point* zimeisha bora akae.

Mheshimiwa Naibu Spika, kaka yangu wa Magu asijaribu kupotosha umma kwa kusema kwamba alitarajia pale alipofariki mama yangu...

MBUNGE FULANI: Taja Kanuni.

MHE. ESTHER N. MATIKO: ...Mheshimiwa Dkt. Elly Macha angeletwa mlemavu. Inaonesha kwamba hata utaratibu wa nchi hii haufahamu wakati naye ni Mbunge. Zaidi mliyomuondoa Mama Sophia Simba, Mwenyekiti wa UWT alikuja Mheshimiwa Mama Rwakatara ambaye siyo Mwenyekiti wa UWT CCM. Kwa hiyo, changia *point* kama zimeisha kaa chini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther, ulisema kwamba unataka kumpa Taarifa, naona sasa unatoa Taarifa kwa namna ambayo na wewe unachangia wakati muda wako wa kuchangia ulishamaliza. Mheshimiwa Kiswaga, endelea.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza taarifa si kubali kwa sababu chama kina mamlaka ya kubadilisha. *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii Rais Dkt. Magufuli, kama ni upele umepata mkunaji sasa. Unajua ili uwe jemedari lazima upigane vita, huwezi kuwa jemedari bila kupigana vita. Rais Dkt. Magufuli amepigana vita ya ufisadi, rushwa, vyeti hewa na mambo mengi, kwa hiyo, amefanya kazi ambayo alikusudia. *(Makofi)*

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Naibu Spika, Rais Dkt. Magufuli wakati...

NAIBU SPIKA: Naomba ukae Mheshimiwa muache amalize muda wake.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Yeye atafanya kazi, hatajali chama...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwakajoka naomba ukae amalizie muda wake.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Wale ambao wanatoka vyama vya upinzani tutapata wapi Rais wa namna hii? Kwa hiyo, naomba niwaambie Wabunge wenzangu wajue kwamba dereva mliyenaye atawafikisha salama na CCM itashinda mwaka 2020. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kiswaga, muda wako umekwisha, ahsante sana.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Hiyo CCM miaka 50 ndiyo haikuleta maji.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Naibu Spika,...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Gekul mlishakatazwa humu ndani kuwasha *microphone* kabla hujaruhusiwa kuzungumza, tafadhali. Mheshimiwa Kiswaga, muda wako umemalizika.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja lakini tuvumiliane kisiasa, tuwe na ngozi nene. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Mheshimiwa Kepteni George atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Mgumba na Mheshimiwa Almas Maige ajiandae.

MHE. KEPT. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

NAIBU SPIKA: Upande wa pili naomba utulivu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

NAIBU SPIKA: Naomba mtulie tafadhali. Mkianza kuzungumza namna hii hilo Bunge halitakuwa linaweza kufanya kazi zake. Mheshimiwa Esther Matiko, tafadhali. Mheshimiwa Kepteni Mkuchika, naomba uendelee.

MHE. KEPT. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Napenda kuchukua nafasi hii kwanza kumpongeza Rais wetu John Pombe Magufuli anavyoiendesha nchi hii. Wapo ndugu zetu walikuwa wanapiga kelele za ufisadi, ufisadi, amewafungulia Mahakama ya Ufisadi. Wale waliokuwa wanasema kwamba huyu fulani fisadi wamewachukua, tulateeni kwenye Mahakama ya Ufisadi tuwashughulikie. *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kunti Majala, tafadhali, utulivu. Mheshimiwa Kepteni Mkuchika endelea.

MHE. KEPT. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuunga mkono hoja ya Wizara ya Maji. Nataka niwakumbushe Wabunge wenzangu Kanuni zetu zinasema Kamati Ndogo ya Bunge ya Kudumu inapofanya kazi ni sawasawa na Spika amekaa anaendesha Bunge. Bajeti tuliyoletewa hapa imefanyiwa kazi na wenzetu wa Kamati inayohusika na suala la maji. Kwa hiyo, unapokuja hapa tu ghafla bin vuu ukasema tufumue, turudishe, tufanyeje, mbona mnawadharau Wajumbe wenzetu wa Kamati waliofanya kazi hii?

Mimi naungana na wenzangu wanaosema tutafute namna ya kuboresha Mfuko wa Maji, yale mawazo yanakaribishwa, lakini wewe unasema tufumue, tukatae, darasa hilo sisi wanafunzi tunalikataa, darasa la kukataa bajeti sisi tunalikataa, bajeti hii itapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nataka nianze kwa kuwapongeza wapigakura wangu wa Jimbo la Newala. Kule kwetu Newala tuna ustaarabu wa kuvuna maji ya mvua, kila nyumba ya bati utakayoona ina kisima kimechimbwa na kwa sababu kule kwetu *water table* iko *very low* tunachimba mpaka futi 14, tunajenga kwa zege, tunajenga kwa tofali, tunakinga maji ya mvua ya kutosha familiaile mwaka mzima. Ndiyo maana hali ya maji Newala unafuu upo kidogo, si kwa sababu ya maji ya bomba ya Serikali, hapana, tunakinga maji ya mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tusingekinga maji ya mvua hali yetu ingekuwa mbaya sana. Nataka nitoe mfano na hili mimi nataka niiseme Serikali yangu, mnapofanya vizuri nawapongeza, mnapoharibu nawasema. Hivi mradi wa maji wa Makonde kwa muda wa miezi miwili mmewakatia umeme, watu wa Newala tupate wapi maji ya bomba ya kunywa?

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. KEPT. GEORGE H. MKUCHIKA: Nimeambiwa umeme juzi umerudi, naomba jambo hili lisirudiwe tena. Mheshimiwa Rais aliposema kata umeme amewahimiza Maafisa wa Serikali mnaotakiwa kulipa maana yake mlipe kwa wakati siyo mnazembea kulipa halafu wanakwenda kuadhibiwa wananchi ambao kila mwezi mkiwapelekea ankara wanalipa. *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. KEPT. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa pili ule hata ukawaelimishe namna gani, huyo anayeongea...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zitto Kabwe, tafadhali, jamani tuwe watulivu mwenzetu anapochangia. Mkianza kujibizana, muda wetu unakwenda tunapotezeana muda humu ndani, tafadhali. Mheshimiwa Kepteni Mkuchika endelea.

MHE. KEPT. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, huyo anayeongea alituhamasisha humu tukatae bajeti, mimi sikukubaliana naye lakini nilikaa kimya, ndiyo ustaarabu wa humu ndani. Ndiyo maana tunawaambia nchi hii CCM itatawala ninyi mtabaki tu kama mnyama fulani anaona mkono wa binadamu unatembea anasema unadondoka kesho, unadondoka kesho, ndiyo mlivyo, tunakamata Serikali kesho, kesho, kama mwendo wenu ni huo hampati kushika nchi hii. (*Makofi/Kicheko*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zitto Kabwe unataarifiwa hii ni mara ya mwisho, tafadhali fuata utaratibu, Kanuni unazifahamu. Mheshimiwa Mkuchika endelea.

MHE. KEPT. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka wale ambao hamuifahamu Newala, Waziri anaifahamu, Naibu Waziri anaifahamu, sisi tunaishi mahali kunaitwa *Makonde Plateau*. Wale wanaokumbuka *geography Makonde Plateau definition* yake wanasema *a raised flat piece of land* (kipande cha ardhi kilichonyanyuka), ukiwa kwenye *plateau* maana yake umekaa kwenye meza, ndivyo ilivyo Newala na Tandahimba. Tuko juu kwa hiyo *water table* iko chini sana, hakuna mahali tunapoweza kuchimba tukapata maji na ndiyo maana tunategemea sana maji ya bomba na ndiyo maana kwenye miaka ya 1950 watu wa Newala wenyewe tukaanzisha Kampuni inaitwa *Makonde Water Corporation*, tukakopa hela Uingereza tukaanzisha mradi wa maji Makonde, tukawa tunauza maji, tunatengeneza pesa, watu wanapata maji ya kunywa. Serikali baada ya uhuru ikatuhurumia, ikauchukua ule mradi ikaufanya mradi wa maji wa kitaifa. Nakuomba ndugu yangu

Wenje, aah nakuombandugu yangu Lwenge... *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu Wabunge ni yale yale ya kutokujua, mimi nilidhani upande wa pili wanaelewa kwamba ulimi hauna mfupa kumbe hawajui. Mimi nimewasamehe maana tumefundishwa, baba uwasamehe maana hawajui watendalo, mimi nimewasamehe. *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. KEPT. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ile ya Makondeko ilichukuliwa na Serikali, ukafanywa ndiyo mradi mkubwa wa kitaifa. Mheshimiwa Naibu Waziri, mradi wetu ule wa kitaifa unasuasua kwa sababu upatikanaji wa maji siyo mzuri, miundombinu imechakaa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kepteni Mkuchika muda wako umekwisha.

MHE. KEPT. GEORGE H. MKUCHIKA: Nilipewa dakika 10 na walini-*interrupt* sana hawa jamaa. *(Kicheko)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

NAIBU SPIKA: Muda umekwisha Mheshimiwa.

MHE. KEPT. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu upande wa Wizara yale mambo ambayo nilitaka kuyamalizia nitawaandikia, mimi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Omary Mgumba atafuatiwa na Mheshimiwa Almas Maiga na Mheshimiwa Saada Mkuya, ajiandae.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi hii ili nichangie katika Wizara hii ya Maji.

Kwanza, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa uhai na uzima nimefika siku ya leo. Pili, niishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa inayofanya hasa kwa hiki kidogo ambacho kimekuja. Wengi hapa tumesimama tunalaumu kweli pesa ni ndogo, ni kweli nami nakubaliana kabisa pesa ni ndogo, hata ile bajeti tuliopanga haijaenda ni kweli lakini nilikuwa najua kwa sababu pesa ni ndogo basi tungekuja na mawazo mengi zaidi ya kuishauri Serikali namna gani inaweza kuongeza pesa. Kwa kusema hayo, nami niungane na wenzangu waliotangulia, pamoja na mambo yote kutokana na umuhimu wa maji ni vizuri tukaongeza bajeti katika mafuta ile ya shilingi 50 kwa lita ili tuongeze Mfuko wa Maji uweze kuwa na fedha ya kutosha twende tukaongeze bajeti ya maji ili kutatua tatizo la maji nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo niende kwenye ukurasa wa 71 wa kitabu cha Waziri kuhusu Bwawa la Kidunda. Hili Bwawa la Kidunda mwaka jana tulipitisha bajeti hapa na tullilitengea shilingi bilioni 17 na baada ya kufuatilia mimi mwenyewe Hazina walishatoa shilingi bilioni 10. Madhumuni makubwa ya hiyo shilingi bilioni 17 ilikuwa ni kujenga ile barabara ya Ngerengere - Kidunda kwenda kwenye mradi lakini pia kulipa fidia ya shilingi bilioni nne kwa watu walioathirika kupisha barabara na sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana, mpaka hivi tunavyoongea pesa hizo zimetolewa Hazina lakini hata senti tano haijalipwa kwa hao waathirika wa Kidunda, Chanyumbu na sehemu nyingine.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri akija anieleze, bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri ni shahidi, wiki mbili zilizopita watu walikuwa hawaamini kama Mbunge wao anafuatilia fedha hizi, walikuja hapa bila taarifa mpaka

Wizara ya Maji kufuatilia hela hizi. Tulikutana na Waziri tunamshukuru sana alitupa ushirikiano na alitumbia kwamba zipo hela nusu shilingi bilioni mbili. Cha kushangaza mwaka jana tulikwenda Wizara ya Maji, tuliambiwa ziko nusu shilingi bilioni mbili hizo hizo, mwaka huu tena mwezi wa tatu tumefika ziko shilingi bilioni mbili hizo hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba Serikali ije ituambie kwamba hizi shilingi bilioni mbili zitapatikana lini na hawa watu watalipwa lini ili waweze kuendelea na shughuli zingine na pia hizi shilingi bilioni mbili zilizobaki Serikali ituambie itatoa lini ili mradi huu uweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya fidia hiyo kulipwa, pia huu mradi ni wa muda mrefu sana na una umuhimu mkubwa sana kitaifa, ni vizuri sasa tupate kauli ya Serikali. Kila kitabu cha bajeti kinachokuja, cha mwaka jana kimekuja wanasema tunatafuta fedha, mwaka huu kimekuja wanasema tunatafuta fedha, fedha zipo kwa watu binafsi. Kama pesa hakuna, tuishauri Serikali ikaingia ubia na *private sector* kutekeleza hii miradi mikubwa kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nasema hivyo mradi huu umeanzishwa tangu mwaka 1955 na wakoloni. Baada ya kupata uhuru mwaka 1962, Mwalimu Nyerere kutokana na umuhimu wake aliona tuendelee na mradi huu. Mwaka 1982 likaja tena andiko tuendelee, nashangaa sana mwaka 1994 Serikali kwanza imeupunguza mradi wenyewe kwa sababu wakati ule mradi huu ulikuwa ni zaidi ya lita milioni 430 leo umepunguzwa ni lita milioni 190.

Naomba niishauri Serikali, kutokana na umuhimu wa maji, kutokana na kilimo cha kubahatisha, kutokana na mabadiliko ya tabianchi ni vizuri tukazingatia andiko lile lile la mwanzoni ili huu mradi uwe *multi-purpose* badala ya *single use* kwa ajili ya matumizi tu ya binadamu. Ni vizuri tukarudisha kule ili tuweze kutumia kwa ajili ya umwagiliaji pamoja na matumizi ya binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niende sasa kwenye suala la Jimbo, hii ilikuwa ni mradi wa kitaifa. Sisi mwaka jana hapa tunashukuru Serikali tulipata mradi mmoja pale Mikese ambao ulikuwa unachukua zaidi ya shilingi bilioni mbili na mwongozo Serikali ikautoa yenyewe wakasema hawawezi kutuma pesa mpaka kwanza mkandarasi aanze. Tunamshukuru sana huyu mkandarasi ameshafanya kazi zaidi ya asilimia 40 na juzi ameshusha zaidi ya *semi-trailer* tatu ya mabomba yote ya mradi ule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Serikali, tushaandika *certificate* zaidi ya tatu lakini bado hatujapata majibu, Mkurugenzi wangu hajapata majibu na pesa hazijakuja. Nimeona kwenye kitabu cha Waziri kwenye bajeti mwaka huu imeshushwa hii bajeti imewekwa shilingi bilioni 1.7 wakati mradi ule peke yake una shilingi bilioni mbili.

Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu Tukufu, ni vizuri tukaleta hela hizi mapema kabla hii bajeti haijaisha kwa sababu kama hizi hela hazijaletwa kabla bajeti haijaisha mkandarasi atasimama baadaye mtakuja kutuletea hizi hela shilingi bilioni 1.7 kama zitapatikana mwakani zitakuwa haziwezi kutosheleza kutekeleza mradi huu wala miradi mingine. Kwa sababu hii tunayotumia ni *cash budget*, naomba sana Serikali ikazileta hela hizi za kumlipa huyu mkandarasi ili ule mradi wa Mikese aumalizie kabla ya mwaka huu wa fedha haujaisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nataka nichangie kwenye mradi wa Chalinze Awamu ya Tatu. Mradi wa Chalinze Awamu ya Tatu na sisi watu wa Morogoro Kusini Mashariki na Morogoro Vijijini ni wanufaika kwani kuna vijiji kama saba vitapata maji katika mradi huu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa malizia sentensi yako muda wako umeisha.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, nataka kujua tu Serikali mradi huu itaumaliza lini ili vijiji vyangu vya Bwawani, Ngerengere, Kidunda na Kidugalo na kambi zetu zote zile za Jeshi kwa maana ya Kinonko zipate maji.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Almas Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Saada Mkuya muda wetu ukituruhusu atachangia Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi pia naomba nikushukuru sana kuniruhusu nichangie bajeti hii ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wote humu ndani, naomba niwashauri tu kwamba wampe pongezi Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya na Mawaziri hawa ambao ni vigogo. Siyo kweli kwamba Mawaziri hawafanyi kazi, lakini Wabunge wote imekuwa tunataka maji hata kama tungepewa ng'ombe tugawane hatoshi, kinachotolewa sasa kinatosha sana. Mimi naomba niwashukuru sana Mawaziri ninyi wawili na hasa mpelekeeni salaam Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa miradi mitatu ambayo iko Jimboni kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, mradi ule wa umwagiliaji katika kata ya Shitage, unaenda vizuri lakini naomba muusimamie vizuri umalizike. Vilevile hivi karibuni tumesaini mkataba wa bomba la maji kutoka Ziwa Victoria kuleta maji Uyui na kupeleka Tabora. Mabilioni ya fedha yamewekwa pale, tungepata wapi kama siyo Rais Mheshimiwa Dkt. Magufuli? Pia tume-*comission* mradi mkubwa wa maji pale Mabama kwa niaba ya Mkoa mzima wa Tabora uliosaidiwa na Japan, mradi mkubwa vijiji 31 katika kata zangu vinapata maji, tungepata wapi mtu kama Mheshimiwaw Dkt. Magufuli? Aidha, uko mradi nimeuona umeanzishwa kutoka Malagarasi kuleta maji Urambo na Kaliua unapita pia mpaka kata zangu za Ndonu pale lolangulu. Mradi huu mmeutengea shilingi bilioni mbili,

naona Mheshimiwa Mama Sitta hakuwa ameiona hiyo lakini naomba muanze ili tuweze kuufanikisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako matatizo katika Wizara hii ambayo kwa kweli mimi sidhani kama yanatokana na wao wenyewe. Tumeona bajeti haitoshi, tunawashauri wakachukue shilingi 50 za mafuta waziweke kwenye mradi wa Mfuko wa Maji ili akina mama hawa wapumzike. Ni kweli akina baba wanawakosa akina mama asubuhi, hii hairuhusiwi. Nashauri tuimarisha suala hili ili watoto waende shule wameoga na akina mama wateke maji maeneo ya karibu. Wabunge wote tumeomba humu ndani ya Bunge Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kubalini hilo tupate hela za mfuko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mnisikilize vizuri sana Mawaziri, katika Jimbo langu katika kijiji cha Majengo lilijengwa bwawa, wananchi wakafurahi, wakaanza kuvua samaki, wakamwagilia, bwawa likapasuka baada ya miaka miwili; huu ni mwaka wa tano hamjarudi tena kurekebisha bwawa lile. Mheshimiwa Waziri kama husemi vizuri kuhusu bwawa hili na mimi nitatoa shilingi. Bwawa la Majengo katika kata ya Ikongolo mliligenga limefanya kazi vizuri miaka mitatu limepasuka, mwaka wa tano hamjarudi wala hamjasema sababu kuwaambia wananchi kwa nini hamrudi, naomba mrudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wangu wanakesha wanatafuta maji, nimelipa Serikalini hela nyingi kuwaita Wakala wa Maji na Mabwawa na Wachimba Visima wakapima maji yapo chini, cha kusikitisha, huu ni mwezi wa tano nakutafuta Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Halmashauri wameleta ripoti maji yapo chini tena ya kutosha kwenye vijiji viwili vile vya Inonelwa pamoja na Ikongolo ambako ndiyo hakuna maji, maji yapo chini mengi. Mimi Mbunge nimelipia hela zangu, nataka mje mchimbe kwa sababu maji yapo. Namuomba Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri mnipe majibu kwa nini hamji kuchimba maji ambayo nimegharamia kuyatafuta na yapo chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, mmeutaja mradi huu wa Shitage mwaka wa tatu huu eti wamefanya mita 170, mradi hauendi. Wananchi wanategemea kumwagilia mpunga tupate mpunga pale kwa nini hauendi? Naomba mtakapokuja tena mniambie kwa nini mradi huu wa Shitage umekwama?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunagombania muda hapa, mimi naunga mkono hoja na nakushukuru sana kuniruhusu nichangie hoja hii ya Wizara ya Maji, ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Saada Mkuya tutamalizia na Mheshimiwa Ritta Kabati dakika tano, tano.

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Na mimi nachukua fursa hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na menejimenti yote ya Wizara, kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Maana tukisema kwamba hawafanyi kazi vitu vingine vinakuwa siyo katika *disposal* yao kwa hivyo nadhani hapa tulipo wamejitahidi sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sekta ya maji changamoto zipo nyingi, kuna kurasa ambazo Mheshimiwa Waziri amendika, kurasa 128, 129 na 130 anapongeza zile taasisi za kimataifa na mashirika pamoja na *NGO's* ambazo zinasaidia sekta ya maji, ni nyingi kweli. Mimi nadhani tukiangalia kwenye *assessment*, sekta ambayo inapata *support* kutoka mashirika ya nje na ya ndani ni sekta ya maji, tuna karibu mashirika 62.

Hata hivyo, tukiangalia fedha ambazo zimepatikana katika kipindi cha bajeti ambayo tunakamilisha mpaka Machi ni fedha ndogo sana shilingi bilioni 181 ambayo ni sawa na asilimia 19 lakini wachangiaji wako wengi kweli. Hapa sasa lazima tujikite katika kuhakikisha kwamba tunaweka mikakati ya kuona kwamba fedha zetu sisi wenyewe za ndani ndizo zitakazokwenda ku-*finance* sekta ya maji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, *issue* hapa wala siyo kuongeza bajeti, maana ukisema unakwenda kuongeza bajeti *you just increase the numbers and then what?* Hakuna hela, *it is not about* Hazina atoe hela, Hazina hana hela ni lazima aende akazitafute. Kwa hiyo, lazima tutafute chanzo ambacho kitakuwa *sustainable* ili kuweza kuona kwamba maji yanapatikana. Shilingi 50 kwa mimi ninavyoona tumepata shilingi bilioni 95 ambayo imekwenda kusaidia kwa kiasi kikubwa, tuongeze shilingi 50 nyingine kwenye lita hizo za mafuta. Hata hivyo, tunaweza tukaenda *further* tukaangalia vyanzo vingine, zile *products* ambazo zinatokana na maji zinaweza zikatozwa kwa asilimia fulani hata shilingi mbili kwa kila lita ili kusaidia kwenye Mfuko wa Maji, mimi nadhani hatua hiyo inaweza ikatusogeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya maji ina changamoto kubwa na ni sekta ambayo inategemewa karibu na kila sekta nyingine kwa mfano afya, elimu, ujenzi, kilimo na utalii. Sekta hii yenyewe ni lazima iweze kupeleka huduma katika sekta nyingine, hizi sekta nyingine zenyewe haziwezi kusaidia katika sekta ya maji. Kwa hiyo, tunaona kwamba hii ni changamoto na hapa tunaweza tukamsema Waziri, wewe Waziri sijui kizee, sijui nini, *no, it is not about that*, hii ni changamoto ya Taifa. Kila mtu anasimama labda anamshambulia Waziri, hii siyo katika *disposal* yake. Kwa hiyo, wakati tunachangia ni lazima tuone tunaisaidia vipi Serikali kupata chanzo cha fedha ambacho ni endelevu, kiko *reliable* kuweza kusaidia sekta ya maji. Shilingi bilioni 95 zilizopatikana kutokana na shilingi 50 ni asilimia 53 ya fedha ambazo imetolewa, ni hatua kubwa. Kwa hiyo, tukiongeza na nyingine nadhani Mheshimiwa Waziri tutakapokuja hapa mwaka kesho tukifanya tathmini ya sekta ya maji nadhani tutakuwa tumepata mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa zaidi lakini siyo kwa umuhimu kwamba nalisema mwisho kwa sababu ya muda, Mheshimiwa Waziri utakapokuja lazima utueleze fedha zinazotoka *Exim Bank* ya India ambazo mwaka jana ulizisema kwa mbwembwe zote na sisi Wabunge tunaotoka Zanzibar tulishangilia kweli, tukafanya kikao kuzipangia

matumizi. Leo hatujaona kitu chochote, *31 million dollars*, ni fedha nyingi sana na zinaweza zikabadilisha hali ya maji kule Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimboni kwangu tulitegemea sana fedha hizi mwaka huu ziende zikarekebisha miundombinu ambayo imechakaa mno na tuna dhiki kubwa ya maji, lakini safari hii naona hatujakusikia. Nadhani umesoma *a line one or two* lakini hatujajua *process* hii imefikia wapi, tunataka utupe maelezo ya kina. Tunajua kwamba masuala ya *mobilization* siyo yako, lakini kwa sababu umelizungumza Mheshimiwa Waziri ni lazima ulitolee majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Nabu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba hii ambayo ni muhimu sana kwa sisi akina mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Mawaziri wake ambao wako katika Wizara hii. Vilevile nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama Samia ambaye alikuja Iringa kwa ajili ya kukagua vyanzo vya maji. Niiombe tu Serikali iangalie yale maagizo aliyoyatoa siku zile alivyokuwa Iringa basi yazingatiwe. Tuna imani kwamba kama yatazingatiwa angalau Iringa na sisi vile vyanzo vinaweza vikawasaidia wanawake wa Iringa na wananchi kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niunge mkono Wabunge wote waliochangia kuhusu Mfuko ule wa Maji uongezewe kutoka kwenye shilingi 50 mpaka shilingi 100. Nina imani kabisa ili mwanamke atuliwe ndoo kichwani ni muhimu mfuko huu ukaongezewa kiasi hicho. Pia tuangalie kwenye

vyanzo vingine vya mapato kama wenzetu wengine walivyosema ili tu Mfuko wa Maji upate fedha. Kama walivyosema wenzangu na mimi nawaunga mkono kwamba maji ni kitu muhimu sana katika maisha ya binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu katika Mkoa wetu wa Iringa tumekuwa na matatizo makubwa sana, tumekuwa na vifo vingi sana vinavyosababishwa na ukosefu wa maji. Nitatoa mifano miwili ambayo imetugusa sana wananchi wa Iringa. Kwanza, kuna mwanamke ambaye alikuwa amejifungua watoto mapacha akaenda kwenye Mto Lukosi kwenda kuchota maji yule mama akauawa na mamba. Hili ni jambo ambalo kwa kweli linatumiza, aliacha watoto wadogo sana.

La pili, juzi tu hata mwezi haujaisha, kuna mtoto wa shule ya sekondari ya Lukosi alikwenda pale kuchota maji akatokea mbakaji mmoja akamchukua yule mtoto kutaka akambakie upande wa pili. Watu walipotokeza akamtupa kwenye maji yule mtoto akafa. Kwa kweli ilitusikitisha sana kwa sababu yule binti alikuwa bado mdogo. Kwa hiyo, tunaomba sana Mkoa wa Iringa unauhitaji mkubwa sana wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika vituo vya afya vingi vilivyopo vijijini bado maji ni tatizo, inasababisha akina mama wakati wanajifungua wanapata mateso makubwa sana. Aidha, mama anaamka asubuhi kwenda kwenye shughuli ya kutafuta maji badala ya kwenda kwenye shughuli ya maendeleo. Hii pia inamkosesha mama kuendelea na miradi aliyonayo, kutwa nzima anatafuta maji, anamuacha pia hata mzee, hata ndoa nyumbani zinavunjika kwetu Iringa kwa sababu ya maji kwa sababu mama anaondoka saa 9.00 za usiku kwenda kutafuta maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nisisahau kuwazungumzia wananchi wa Mji Mdogo wa Ilula. Bahati nzuri Mheshimiwa Rais alipokuja kuomba kura alikuja kwenye Wilaya ya Kilolo, lakini kwenye Mji Mdogo wa Ilula. Ule mji

kama alivyosema Mheshimiwa Mgonokulima kwa kweli maji ni tatizo kubwa sana. Siku ile wananchi walikuwa wana mabango ynayozungumzia tatizo la maji wakimwambia Rais wanavyopata shida ya maji. Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba angeweza kuleta maji baada tu ya kuchaguliwa na akatuambia kwamba Waziri atakayemchangua atakuja mara moja kuja kusikiliza tatizo la maji. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri hebu aende Kilolo pale Ilula ukawaeleze kwa nini mpaka leo maji hayajaletwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mkoa wa Iringa hauna tatizo la maji bali ni usambazaji wa maji. Tunavyo vyanzo vingi sana vya mito kama Mto Ruaha, Mto Lukosi, Mto Mtitu na kadhalika, ni kwa nini Serikali isitumie mito hiyo kutatua tatizo hili la maji kwa sababu tumeona miradi mingi sana ya visima haifanyi kazi. Nilishauliza hata swali, tunayo mito mingi kama Mto Lukosi umezunguka maeneo mengi sana, lakini mpaka leo hii haujaweza kutumika ili uweze kuwasaidia wananchi wa Iringa kutatua tatizo la maji linalowakabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba tu nipate majibu, katika mji huo huo wa Ilula, kulikuwa kuna wafadhili wa Austria. Je, ule mradi umefikia wapi kwa sababu tulijua kwamba ungeweza kuwasaidia wananchi wa pale Ilula?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja lakini nitaandika kwa maandishi kwa sababu mengi sana sijayazungumza. Nashukuru sana kwa kupata nafasi hii. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ritta Kabati.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa michango yetu mchana wa leo. Kwa maana ya uwiano, majina yote yamekwisha lakini majina ya CCM yalikuja mengi zaidi, kwa hivyo, kuna ambao hawajapata fursa ya kuchangia leo wataungana na uwiano wa kesho. Naomba hawa watakaoanza kesho ambao ni Mheshimiwa Aisharose Matembe, Mheshimiwa Emmanuel Papian, Mheshimiwa

NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Hawa Ghasia, Mheshimiwa Esther Midimu, Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa Njalu Silanga, Mheshimiwa Sebastian Kapufi, Mheshimiwa Mahmoud Mгимwa, Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani, Mheshimiwa Abdallah Bulembo, Mheshimiwa Hassan Masala na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mawili, tangazo la kwanza ni la kuhusu Kukaimu nafasi ya Mkuu wa shughuli za Serikai Bungeni. Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi ambaye ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi atakuwa akikaimu nafasi hiyo mpaka Mheshimiwa Waziri Mkuu atakaporejea Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine, wakati jana tukitangaza wageni wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo alikuwa hayupo, sasa ameshafika nadhani kesho atapata fursa ya kutambulishwa saa ya wageni, lakini tutambue uwepo wa Profesa Kitila Mkumbo ameshawasili Dodoma kwa ajili ya bajeti ya Wizara yake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 12 Mei, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*